# شرح العقيدة الواسطية

# *Sharh al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah*

*Mwandishi:*

**Shaykh-ul-Islaam Ahmad bin Taymiyyah**

*Mshereheshaji:*

**Imaam ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah bin Baaz**

*Tarjama:*

**Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush**

# YALIYOMO

00. Dibaji ya Shaykh ´Abdul-´Aziyz bin Baaz ....7

01. Dibaji ya Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah ....8

02. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ndio Firqat-un-Naajiyah ....10

03. Nguzo ya 01: Kumuamini Allaah ....12

04. Nguzo ya 02: Kuamini Malaika Wake ....13

05. Ni nani bora kati ya Malaika na muumini? ....14

06. Nguzo ya 03: Kuamini Vitabu ....15

07. Nguzo ya 04: Kuamini Mitume ....16

08. Sababu ya Nuuh (´alayhis-Salaam) kuitwa kuwa ndio Mtume wa kwanza ....17

09. Nguzo ya 05: Kuamini siku ya Mwisho ....18

10. Nguzo ya 06: Kuamini Qadar ....20

11. Uwajibu wa kuamini na kuthibitisha majina na sifa za Allaah ....22

12. Tunazipitisha sifa za Allaah kama zilivyokuja ....25

13. Mitume ni wakweli katika yale waliyoeleza juu ya Allaah ....26

14. Uwajibu wa kuamini yale waliyokuja nayo Mitume ....28

15. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan I ....31

16. Hii ndio njia wanayofuata Ahl-us-Sunnah al-Jamaa´ah ....34

17. Allaah ametakasika na mapungufu na kasoro aina zote ....35

*Dalili ya uhai wa Allaah* ....36

18. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan II ....40

*Dalili kwamba Allaah ndiye wa Mwanzo na wa Mwisho* ....42

*Dalili ya Nguvu na Kuruzuku kwa Allaah* ... 43

*Dalili ya Allaah kutolingana na chochote na kuwa na mwenza* ... 44

*Dalili ya Kuona na Kusikia kwa Allaah* ... 44

*Dalili ya Utashi na Matakwa ya Allaah* ... 45

19. Aina mbili za utashi ... 46

20. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan III ... 48

*Dalili ya Kupenda kwa Allaah* ... 50

*Dalili ya Kuridhia na Kughadhibika kwa Allaah* ... 51

21. Maana ya sifa za Allaah inajulikana na namna haijulikani ... 53

22. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan IV ... 55

*Dalili ya Kusamehe, Kurehemu na Uwezo wa Allaah* ... 58

*Dalili ya Kuja na Kuwasili kwa Allaah* ... 59

*Dalili ya Uso wa Allaah* ... 60

*Dalili ya Mikono ya Allaah* ... 60

*Dalili ya Allaah kuwa na Macho* ... 60

*Dalili ya Adhabu na njama za Allaah* ... 61

*Dalili ya Kusikia na Kuona kwa Allaah* ... 61

23. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan V ... 63

*Dalili ya Allaah kutokuwa na wenza na washirika* ... 65

*Dalili ya Allaah kutokuwa na mtoto* ... 67

*Dalili ya Kuumba na Uwezo wa Allaah* ... 68

24. Kuuliza namna ya Sifa za Allaah ni Bid´ah iliyozusha Ahl-ul-Bid´ah ... 69

25. Mu´attwilah na Mumaththilah ni makafiri ... 72

26. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan VI ....73

*Dalili ya kwamba Allaah amelingana juu ya ´Arshi Yake* ....75

*Dalili ya kwamba Allaah yuko juu ya viumbe Vyake kwa dhati Yake* ....75

27. Sifa za Allaah haziuliziwi namna, zinauliziwa maana ....79

28. Upamoja wa Allaah aina mbili ....81

*a) Allaah yuko pamoja na waja Wake wote kwa ujuzi Wake* ....81

*b) Allaah yuko pamoja na waja Wake wema kiujuzi, kwa kuwanusuru na kwa kuwapa nguvu* ....82

29. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan VII ....85

*Dalili ya Maneno na Kuzungumza kwa Allaah* ....88

*Dalili kwamba Qur-aan imeteremshwa kutoka kwa Allaah* ....89

*Allaah anazungumza pale anapotaka* ....89

30. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan VIII ....91

*Dalili kwamba waumini watamuona Mola wao Aakhirah* ....91

31. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Sunnah I ....94

*Dalili ya kwamba Allaah Huteremka katika mbingu ya chini* ....96

*Dalili ya Kucheka kwa Allaah* ....97

*Dalili ya Kustaajabu kwa Allaah* ....97

*Dalili kuwa maneno ya Allaah ni ya Herufi na Sauti* ....97

*Dalili ya Mguu wa Allaah* ....98

*Dalili ya Kufurahi kwa Allaah* ....100

32. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Sunnah II ....102

*Dalili ya Kuzungumza kwa Allaah* ....104

*Dalili ya kwamba Allaah yuko juu* ....................................................104

33. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Sunnah III ....................................................106

*Dalili kwamba Allaah yuko mbele ya mswalaji* ....................................................106

*Dalili ya Allaah kuwa kila mahali kwa ujuzi Wake* ....................................................106

34. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Sunnah IV ....................................................109

*Dalili ya Sifa mbalimbali za Allaah* ....................................................110

*Dalili kwamba waumini watamuona Mola wao Aakhirah* ....................................................111

*Dalili ya Kusikia na Kuona kwa Allaah* ....................................................112

*Dalili ya Allaah kuwa Karibu na waja Wake* ....................................................113

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, watu wa kati kwa kati ....................................................114

*Kati ya Jahmiyyah na Mushabbihah* ....................................................114

*Kati ya Qadariyyah na Jabriyyah* ....................................................115

*Kati ya Murji-ah na Wa´iydiyyah* ....................................................115

*Kati ya Haruuriyyah na Mu´tazilah, na Murji-ah na Jahmiyyah* ....................................................116

*Kati ya Raafidhwah na Khawaarij* ....................................................116

35. Msimamo wa Ahl-us-Sunnah kwa Ahl-ul-Bayt na ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) ...118

36. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah kuhusu Ujuu wa Allaah ....................................................119

37. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya Qur-aan na kwamba haikuumbwa ....................................................124

38. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya kuonekana Allaah Aakhirah ........130

*Makafiri watazuiwa na kumuona Allaah* ....................................................132

39. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya Hodhi na Njia ....................................................138

*Uwajibu wa kujibidisha na njia za salama na uokovu* ....................................................141

40. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya maombezi ........................................ 143

*Nyombezi tatu za Mtume (´alayis-Salaam)* ........................................ 144

41. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya Qadar ........................................ 149

42. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya imani ........................................ 157

43. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya wakeze Mtume, Ahl-ul-Bayt na Maswahabah ........................................ 164

44. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya karama za mawalii ........................................ 172

*Qur-aan, Sunnah kwa ufahamu wa Salaf* ........................................ 175

45. Baadhi ya sifa tukufu za Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ........................................ 176

*Hitimisho* ........................................ 178




## 00. Dibaji ya Shaykh ´Abdul-´Aziyz bin Baaz

Himdi zote anastahiki Allaah, Mola wa walimwengu. Swalah na salaam zimwendee Mtume wetu Muhammad, kizazi chake na mwenye kufuata uongofu wake.

Amma ba´d:

Kitabu hichi chenye thamani kikubwa kwa jina "al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah" kimeandikwa na Shaykh-ul-Islaam Abul-´Abbaas Ahmad bin ´Abdil-Haliym bin ´Abdis-Salaam bin Taymiyyah al-Harraaniy (Rahimahu Allaah). Mtu huyu alikuwa ni Imaam, baba na babu yake pia walikuwa hali kadhalika. Wote walikuwa ni maimamu wa elimu na uongofu. Alizaliwa 661 H na akafariki 728 H. Ina maana aliishi miaka 68.

Aliwakusanyia ´Aqiydah hii watu wa Waasitw upande wa ´Iraaq. Imeitwa kuwa ni "al-Waasitwiyyah" kwa sababu wameandikiwa wao. Kama ambavyo ana kitabu chake kingine kinachoitwa "al-Hamawiyyah" kwa sababu waliandikiwa watu wa Hamaah, kingine kinachoitwa "at-Tadmuriyyah" kwa sababu aliwaandikia watu wa Tadmur. Ni vitabu vitukufu. "at-Tadmuriyyah" ni kitabu kitukufu ijapokuwa ni kikubwa kuliko hiki. Vivyo hivyo "al-Hamawiyyah" ndani yake mna nukuu nyingi kutoka kwa maimamu wa Salaf (Rahimahumu Allaah). Kuhusiana na kitabu hichi "al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah" ni mukhtaswari, chenye faida na cha kijumla. Hatujui kama kuna kitabu mfano wake miongoni mwa vitabu vilivyoandikwa na watu kutokamana na ufupi wake lakini hata hivyo kimekusanya ´Aqiydah ya Salaf-us-Swaalih. Ametumia (Rahimahu Allaah) ibara ambazo ni za wazi na usulubu bora zaidi.

## 01. Dibaji ya Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*"Himdi zote anastahiki Allaah Aliyemtuma Mtume Wake kwa uongofu na kwa dini ya haki ili ipate kushinda dini zote na Allaah anatosha kuwa shahidi.*

*Nashuhudia ya kwamba hakuna mungu mwenye kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allaah Pekee, hali ya kuwa hana mshirika, kwa kukiri hilo na kumpwekesha Yeye Pekee. Nashuhudia vilevile ya kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kizazi chake na Maswahabah zake.*

*Amma ba´d:*

**MAELEZO**

Amemtuma Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa uongofu na dini ya haki. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ

**"Yeye Ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na dini ya haki ili Aidhihirishe juu ya dini zote japo watakirihika washirikina." (09:33)**

Uongofu ni elimu yenye manufaa na maelezo ya kweli. Haya ndio huitwa kuwa ni uongofu. Dini ya haki ni yale maamrisho na makatazo yaliyo salama na adilifu yaliyowekwa katika Shari´ah. Allaah amemtuma (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa elimu yenye manufaa na matendo mema na Shari´ah iliyonyooka bara bara. Amefanya hivo ili iweze kushinda dini zengine zote kutokana na ule uongofu aliyomtumwa kwao. Allaah anatosha kuwa ni shahidi kwa jambo hili kubwa.

**Nashuhudia ya kwamba hakuna mungu mwenye kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allaah Pekee...** - Kukiri ya kwamba Yeye ndiye wa Pekee na Mwenye

kustahiki ´ibaadah, Yeye ndiye wa Pekee katika dhati Yake, Yeye ndiye wa Pekee katika sifa za majina Yake. Hana mshirika, mwenza na anayelingana Naye. Yeye ni wa Pekee katika uola Wake na katika kuwaumba Kwake viumbe. Hakuna mwingine aliyewaumba asiyekuwa Yeye. Yeye ndiye Muumbaji na Mruzukaji. Yeye ni wa Pekee katika uungu Wake. Hakuna mwengine anayestahiki ´ibaadah asiyekuwa Yeye (Jalla wa ´Alaa).

**Kwa kukiri hilo -** Bi maana kwa Tawhiyd hii.

**Kumpwekesha Yeye -** Kumuabudu Allaah peke Yake (Subhaanahu wa Ta´ala).

Baada ya hapo akamsalia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kama ilivyokuja katika Hadiyth. Amemuelekeza (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) mwenye kuomba du´aa aanze kwa kumhimidi kwanza Allaah kisha baada ya hapo amswalie (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Imependekezwa mtu anapoanza kuomba du´aa au kuandika kitabu mtu aanze kwa kumhimidi Allaah, kumsifu, kumshuhudia ustahiki Wake wa ´ibaadah na kumshuhudia Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) utume. Kufanya hivi ni miongoni mwa sababu za kukubaliwa du´aa na ni miongoni vilevile mwa sababu za mafanikio. Kwa ajili hii amesema katika Hadiyth iliyopokea Fadhwaalah bin ´Ubayd (Radhiya Allaahu ´anh):

"Anapoomba mmoja wenu basi aanze kwa kumhimidi na kumsifu Allaah halafu amswalie Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kisha baada ya hapo aombe akitakacho."[1]

**Amma ba´d -** Ni neno linaloletwa ili kutenganisha maneno ya kabla na yanayokuja baada yake. Malengo ni kutoka sehemu kwenda nyingine. Kwa msemo mwingine ama baada ya maneno yaliyotangulia.

[1] Abuu Daawuud (1481) na at-Tirmidhiy (3477) ambaye amesema kuwa Hadiyth ni Hasan Swahiyh.

## 02. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ndio Firqat-un-Naajiyah

*Hii ni I´tiqaad ya al-Firqat-un-Naajiyah al-Mansuurah mpaka kisimame Qiyaamah, Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, nayo ni:*

**MAELEZO**

**Hii ni I´tiqaad... -** Bi maana ninasema kuwa hii nitakayoitaja ndio I´tiqaad.

**al-Firqat-un-Naajiyah al-Mansuurah mpaka kisimame Qiyaamah, Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah -** Kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameeleza kuwa Ummah utagawanyika mapote sabini na tatu na kwamba yote yataingia Motoni isipokuwa moja tu. Kukasemwa: "Ni lipi hilo, ewe Mtume wa Allaah?" Akasema: "Ni mkusanyiko, *al-Jamaa´ah*."[2]

Katika upokezi mwingine imekuja:

"Ni lile linalofuata yale ninayofuata mimi hii leo na Maswahabah zangu."[3]

Hawa ndio Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Wanaitwa pia Firqat-un-Naajiyah. Wanaitwa pia Twaaifat-un-Mansuurah mpaka Qiyaamah kisimame. Hizo zote ni sifa za pote moja. Linaitwa kuwa ni kundi lililonusuriwa mpaka siku ya Qiyaamah, kundi lililookoka, Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah na Ahl-us-Sunnah. Nao ni Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) na wale watakaofuata uongofu wao. Hawa ndio Ahl-us-Sunnah. Hawa ndio Firqat-un-Naajiyah. Ni Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wale wenye kufuata mfumo wao, uongofu wao na wakawaiga. Hawa ndio Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.

Wanatoka katika hao Jahymiyyah, Mu´tazilah, Murji-ah, Qadariyyah na kila mwenye kwenda kinyume na Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum). Kila

[2] Ibn Maajah (3992), Abuu Daawuud (3597) na al-Haakim (443) ambaye ameisahihisha na adh-Dhahabiy akawafikiana naye (01/218).

[3] at-Tirmidhiy (2641), al-Haakim (444) ambaye ameisahihishya na adh-Dhahabiy ameafikiana naye (01/128).

mwenye kwenda kinyume na Maswahabah anakuwa katika mapote sabini na mbili.

Ambaye yuko katika Firqat-un-Naajiyah ni yule anayefuata uongofu wa Maswahabah katika kumpwekesha Allaah, kumtakasia Yeye ´ibaadah, kufuata Shari´ah Yake na kuadhimisha maamrisho Yake na kujiepusha na makatazo Yake kama ilivyokuja katika Kitabu Chake na Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hawa ndio watu wenye Firqat-un-Naajiyah.

## 03. Nguzo ya 01: Kumuamini Allaah

*Kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, kufufuliwa baada ya mauti na kuamini Qadar; kheri yake na shari yake.*

**MAELEZO**

**Kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake... -** ´Aqiydah yao ni kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, siku ya Mwisho. Katika upokezi mwingine imekuja:

"Kuamini kufufuliwa baada ya mauti."

Vilevile inatakiwa kuamini Qadar; kheri na shari yake. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah matawi yake yanatanua katika misingi hii sita:

**Kumuamini Allaah ina maana ni pamoja na kuamini yale aliyojisifia Mwenyewe... -** Inaingia katika kumuamini Allaah kuamini vilevile kuwa Yeye ni Mmoja Pekee, hali ya kuwa hana mshirika. Vilevile inatakiwa kuamini kuwa Allaah alituma Mitume, na akateremsha Vitabu, akaweka Shari´ah. Humo kunaingia nguzo za Uislamu ambazo ni swalah, zakaah, swawm na hajj. Yote haya yanaingia katika kumuamini Allaah na kuamini kuwa Yeye ni Mmoja Pekee na ´ibaadah anastahiki kufanyiwa Pekee. Vilevile kuamini kuwa Yeye ndiye aliyeweka Shari´ah kama swalah, zakaah, swawm, hajj na hukumu nyenginezo.

## 04. Nguzo ya 02: Kuamini Malaika Wake

**... Malaika Wake... -** Bi maana kuamini wale wote ambao Allaah amewataja katika Kitabu Chake au waliothibiti katika Sunnah sahihi. Ahl-us-Sunnah wanawaamini wote hao. Baadhi yao ni Jibriyl, Mikaaiyl, Israafiyl, Malaika wa mauti, mlinzi wa Moto na wengineo. Malaika waliotajwa kwa njia ya ufafanuzi wanawaamini kiufafanuzi. Malaika waliotajwa kwa njia ya ujumla - kama mfano ya wabebaji wa ´Arshi wanaoitwa Kuruubiyyuun na wengineo - Ahl-us-Sunnah wanawaamini kiujumla. Wanaamini kuwa Allaah ana Malaika na miongoni mwao wako wanaobeba ´Arshi ambao ni Kuruubiyyuun, wanaotuchunga, ambao wamepewa kazi juu yetu, Jibriyl, Mikaaiyl, Israafiyl na wengineo. Wakija kiujumla wanawaamini kiujumla. Vilevile wanaamini kuwa Malaika ni waja wa Allaah. Allaah (Ta´ala) amesema:

بَلْ عِبَادٌ مُّكْرَمُونَ لَا يَسْبِقُونَهُ بِالْقَوْلِ وَهُم بِأَمْرِهِ يَعْمَلُونَ

**"Bali ni waja waliokirimiwa. Hawamtangulii kwa kauli nao kwa amri Yake wanafanya." (21:26-27)**

## 05. Ni nani bora kati ya Malaika na muumini?

Malaika ndio viumbe bora kabisa wa Allaah. Lakini hata hivyo Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaonelea kuwa muumini katika wanaadamu ni bora zaidi kuliko Malaika. Hili ni kwa maafikiano ya Ahl-us-Sunnah. Kwa kuwa wao wamewajibishiwa ´ibaadah na hivyo ni wenye kupewa mtihani wa matamanio. Hivyo wao ni bora kwa njia hii ikiwa kama wataamini na kuwa na msimamo.

## 06. Nguzo ya 03: Kuamini Vitabu

**... na Vitabu Vyake... -** Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaamini Vitabu vyote vya Allaah alivyoteremsha kwa Mitume. Wanaamini vile walivyovijua kama Tawraat, Injiyl, Zabuur na Qur-aan. Vilevile wanaamini vile wasivyovijua kwa njia ya ujumla. Amesema (Ta´ala):

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ

**"Kwa yakini Tuliwapeleka Mitume Wetu kwa hoja bayana na Tukateremsha pamoja nao Kitabu na mizani." (57:25)**

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaamini kuwa Allaah ameteremsha Vitabu kwa Mitume na kwamba ni haki. Wanaamini vilevile kuwa Vitabu hivyo ni katika maneno ya Allaah (Jalla wa ´Alaa). Miongoni mwa Vitabu hivyo ni pamoja vilevile na Tawraat, Injiyl, Zabuur na Qur-aan. Hivi ni miongoni mwa Vitabu alivyoteremsha.

## 07. Nguzo ya 04: Kuamini Mitume

**... na Mitume Wake... -** Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanamini Mitume wote na kwamba Allaah ametuma Mitume. Mtume wa kwanza ni Nuuh (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Aadam pia (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) ni Mtume kwa kizazi chake. Mtume wa mwisho ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mitume wote ni haki. Mitume wote wamefikisha ujumbe wa Allaah. Mitume wote wametumwa kwa lengo la kuwalingania watu katika: kumuabudu Allaah peke Yake na kumtii. Sambamba na hilo wanawatahadharisha shirki na maasi. Mitume wote hii ndio ilikuwa kazi yao kuanzia wa mwanzo wao Aadam mpaka wa mwisho wao Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

## 08. Sababu ya Nuuh (´alayhis-Salaam) kuitwa kuwa ndio Mtume wa kwanza

Nuuh (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameitwa kuwa ndio Mtume wa kwanza kwa sababu yeye ndiye alikuwa Mtume wa kwanza kwa waliokuwa katika ardhi baada ya kutokea shirki. Kabla ya hapo walikuwa katika Tawhiyd wakifuata Shari´ah ya Aadam (´alayhis-Swalaatu was-Salaam). Baada ya hapo ndipo kukatokea shirki katika watu wa Nuuh (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) kwa sababu ya kuvuka kwao mipaka kwa Wadd, Suwaa´, Yaghuuth na Nasr[4]. Hapo ndipo Allaah akawatumia Nuuh ili awalinganie katika kumuabudu Allaah peke Yake na kuwatahadharisha na kumshirikisha. Pale walipoendelea na hawakuitikia ndipo Allaah akawaangamiza. Tunamuomba Allaah afya.

[4] Tazama "as-Swahiyh" ya al-Bukhaariy (4920).

## 09. Nguzo ya 05: Kuamini siku ya Mwisho

**... kufufuliwa baada ya mauti... -** Ahl-us-Sunnah wanaamini msingi wa tano ambao ni kuamini siku ya Mwisho au kufufuliwa baada ya kufa. Ahl-us-Sunnah wanaamini kuwa majini na watu watakufa na kwamba watafufuliwa.

Mtu anaweza kusema ´kufufuliwa Aakhirah` na pia mtu anaweza kusema ´siku ya Mwisho`. Yote mawili yamekuja katika maandiko. ´Siku ya mwisho` ni jina limekuja kwa dalili ya Qur-aan na katika baadhi ya Hadiyth kumekuja jina ´kufufuliwa baada kufa`.

Ahl-us-Sunnah wanaamini kuwa wanaadamu na majini watakufa kisha baada ya hapo watafufuliwa. Halafu waende kulipwa kwa ajili ya matendo yao ya kheri na ya shari. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amebainisha hilo pale aliposema:

زَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَن لَّن يُبْعَثُوا ۚ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ۚ وَذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**"Waliokufuru wamedai kwamba hawatofufuliwa kamwe. Sema: "Bali hapana! Naapa kwa Mola wangu, bila shaka mtafufuliwa, kisha mtajulishwa kwa yale yote mliyoyatenda - na hayo kwa Allaah ni mepesi." (64:07)**

Ni lazima watu wafufuliwe na kulipwa.

Kwa hivyo siku ya Mwisho ni kule kufufuliwa baada ya kufa. Hapo ndipo watu watalipwa kwa matendo yao, ambaye alitenda mema atalipwa mema na ambaye alitenda maovu atalipwa maovu. Amesema (Ta´ala):

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسَاءُوا بِمَا عَمِلُوا وَيَجْزِيَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحُسْنَى

**"Na ni vya Allaah Pekee vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ili Awalipe [adhabu ya Moto] wale waliofanya uovu kwa yale waliyoyatenda na ili Awalipe wale waliofanya wema kwa [kuwaingiza] Peponi." (53:31)**

Muumbaji ana miadi ambayo ni siku ya Qiyaamah hata kama duniani anaweza kuwaacha. Ikiwa kuna watu watakufa pasi na kuadhibiwa, basi wana miadi. Amesema (Subhaanah):

وَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ غَافِلًا عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ ۚ إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ الْأَبْصَارُ

**"Na wala usidhanie kwamba Allaah Ameghafilika na yale wanayoyatenda madhalimu. Hakika Anawaakhirisha kwa ajili ya Siku ambayo macho yatadokoka [kwa kiwewe kubwa]." (14:42)**

Bi maana siku ya Qiyaamah.

## 10. Nguzo ya 06: Kuamini Qadar

**… kuamini Qadar; kheri na shari yake -** Inatakiwa kuamini Qadar kwamba Allaah ameyakadiria mambo kabla ya kuumbwa watu. Ni makadirio ambayo yametangulia. Muslim amepokea kupitia kwa ´Abdullaah bin ´Amr bin al-´Aasw (Radhiya Allaahu ´anhumaa) ambaye ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Allaah ameyakadiria makadirio ya waja miaka elfu khamsini kabla kuumba mbingu na ardhi na ´Arshi Yake ilikuwa juu ya maji."[5]

Amesema (Jalla  wa ´Alaa):

إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ

**"Hakika sisi Tumekiumba kila kitu kwa makadirio." (54:49)**

مَا أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن قَبْلِ أَن نَّبْرَأَهَا ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ لِّكَيْلَا تَأْسَوْا عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرَحُوا بِمَا آتَاكُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ

**"Hakuna msiba wowote unaokusibuni katika ardhi au katika nafsi zenu isipokuwa umeandikwa katika Kitabu kabla Hatujauumba [huo msiba]. Hakika hayo kwa Allaah ni mepesi. Ili msisononeke juu ya yale yaliyokuondokeeni na wala msifurahie kwa yale Aliyokupeni; na Allaah Hapendi kila mwenye kujinata, anayejifakharisha." (57:22-23)**

Makadirio ni kitu kimetangulia na kiliandikwa. Amesema (Ta´ala):

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ فِي كِتَابٍ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**"Je, hujui kwamba Allaah Anajua yale yote yaliyomo katika mbingu na ardhi? Hakika hayo yameandikwa katika Kitabu. Hakika hayo kwa Allaah ni mepesi." (22:70)**

[5] Muslim (2653).

Ahl-us-Sunnah wanaamini kuwa Allaah ameyakadiria mambo na kuyaandika miaka elfu khamsini kabla ya kuumba watu na kuumba vitu vyengine vyote. Wakati huo ´Arshi Yake ilikuwa juu ya maji.

Hizi ndio nguzo sita zinazohusiana na imani kwa mujibu wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.

## 11. Uwajibu wa kuamini na kuthibitisha majina na sifa za Allaah

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Kumuamini Allaah ina maana ni pamoja na kuamini yale aliyojisifia Mwenyewe katika Kitabu Chake na kwa yale aliyomsifia kwayo Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) bila ya upotoshaji, ukanushaji, kuzifanyia namna wala kufananisha. Bali wao wanaamini yafuatayo kuhusiana na Allaah (Subhaanah):*

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

*"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)*

*Hawakanushi kutoka Kwake yale ambayo amejisifu Mwenyewe na wala hawapotoshi maana ya maneno kuyatoa mahala pake. Hawaharibu majina ya Allaah na Aayah Zake. Hawaainishi maana Yake halisi, hawazifananishi na kuzilinganisha sifa Zake na sifa za viumbe Wake. Hakika Yeye (Subhaanah) hana mshirika wala mwenza na wala halinganishwi na viumbe Wake (Subhaanahu wa Ta´ala).*

*Kwani, hakika Yeye (Subhaanah) ni Mjuzi zaidi wa kujijua Mwenyewe na wengine na ni Mkweli zaidi kwa Kauli na Maneno yaliyo bora na ya wazi kuliko Viumbe Vyake."*

**MAELEZO**

**Kumuamini Allaah ina maana ni pamoja na kuamini yale aliyojisifia Mwenyewe... -** Kunaingia katika kumuamini Allaah mtu kuamini yale majina ambayo Allaah amejiita kwayo, kwa mfano *al-Hakiym* [Mwingi wa hekima], *al-´Aziyz* [Mwenye nguvu], *Rawuf* [Mpole], *ar-Rahiym* [Mwenye kurehemu], *al-Qadiyr* [Muweza] na mengineyo.

**... na kwa yale aliyomsifia kwayo Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)... -** Vilevile mtu kuamini yale majina na sifa ambazo Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amemsifu kwazo katika Hadiyth Swahiyh. Ni

wajibu kumthibitishia nayo Allaah. Kwa mfano yaliyokuja katika Hadiyth Swahiyh:

"Allaah anawacheka watu wawili ambapo mmoja wao kamuua mwenzake. Halafu wote wawili wanaingia Peponi."[6]

"Hakika Mola Wangu leo amekasirika khasira ambayo hajapatapo kukasirika namna yake hapo kabla na hatokasirika mfano wake baada yake."[7]

Bi maana siku ya Qiyaamah. Kuna sifa nyenginezo nyingi za Allaah (Jalla wa ´Alaa) ambazo zimekuja katika Qur-aan na Sunnah safi. Ahl-us-Sunnah wanaziamini na wakati huo huo wanaziitakidi. Wanaamini kuwa hakuna anayelingana Naye, hana mwenza wala hana mshirika. Vilevile halinganishwi na viumbe Vyake (Subhaanahu wa Ta´ala). Yeye ana majina mazuri na sifa kuu. Ahl-us-Sunnah hawafananishi sifa Zake na sifa za viumbe Vyake (Jalla wa ´Alaa). Wanajua kuwa sifa Zake zinalingana na Yeye na hazifanani na sifa za viumbe Vyake (Subhaanahu wa Ta´ala). Hana mwenye kulingana Naye:

هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

**"Je, unamjua mwenye jina kama Lake?" (19:65)**

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye." (112:04)**

فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

**"Basi msimfanyie Allaah waliolingana naye [washirika] na hali ya kuwa nyinyi mnajua [kuwa hana]." (02:22)**

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanathibitisha sifa na majina ya Allaah kwa njia inayolingana Naye (Subhaanahu wa Ta´ala). Hawazipingi sifa Zake na

[6] al-Bukhaariy (2826) na Muslim (1890).

[7] al-Bukhaariy (3340) na Muslim (194).

hawayapotosho maneno kuyaondosha mahala pake stahiki. Bali wao wanaamini majina na sifa zote zilizokuja katika Qur-aan na Sunnah kwa njia inayolingana na Allaah.

Wanafanya hivo bila pasi na *Tahriyf*, upotoshaji. Upotoshaji maana yake ni kuyapotosha maneno, inafanywa hivo ima kwa kuzidisha au kwa kupunguza.

Wanafanya hivo pasi na kuzikanusha sifa *Ta´twiyl*. Maana yake ni kuikanusha sifa, kuipindisha au kupindisha maana yake.

Wanafanya hivo bila pasi na *Takyiyf*, kuzifanyia namna. Kwa mfano hawasemi "Allaah amelingana namna hii", "Allaah hushuka namna hii", "Allaah hukasirika namna hii".

Wanafanya hivo bila pasi na *Tamthiyl*, kufananisha. Hawasemi "Allaah hukasirika mfano wa hivi", "Allaah amelingana mfano wa hivi", "Allaah husikia mfano wa hivi", "Allaah huona mfano wa hivi".

Badala yake wanamthibitishia Allaah majina na sifa zake kwa njia inayolingana Naye. Hawabadilishi, hawapotoshi, hawampigiii mfano, hawakanushi na hawaainishi namna. Kanuni yao katika hilo ni ifuatayo:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**“Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.” (42:11)**

## 12. Tunazipitisha sifa za Allaah kama zilivyokuja

Wakati Imaam Maalik (Rahimahu Allaah) na wengineo katika Salaf walipoulizwa juu ya hili - namna ya sifa za Allaah - wakasema:

"Kulingana kunajulikana, namna haijulikani, kuamini hilo ni wajibu na kuuliza juu ya hilo ni Bid´ah."[8]

Bali Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) ni mwenye kusifika kwa sifa, kama alivyoeleza Mwenyewe, bila ya kuzidisha wala kupunguza. Nazo ni sifa za kihakika. Kulingana ambako ni kwa hakika. Kusikia kwa hakika. Kuridhia kwa hakika. Kukasirika kwa hakika. Sifa zote hazina *Majaaz*. Bali ni za hakika kwa njia inayolingana na Allaah.

Hatuziwekei namna na kuzipigia mfano, hatuzishabihishi wala kuzipotosha. Bali tunazipitisha kama zilivyo dhahiri yake. Kila kilichothibiti katika andiko tunakipitisha kama kilivyokuja. Kama walivyosema Salaf:

"Zipitisheni kama zilivyokuja."[9]

Bila ya kuzipotosha, kuzikanusha wala kuzifasiri kimakosa, *Ta´wiyl.* Tunazipitisha na wakati huo huo tunaamini kuwa ni za haki na kwamba ni sifa zenye kuthibiti na kwamba Allaah anasifika nazo kihakika. Tunafanya hivo bila ya kushabihisha, kufananisha, kuziwekea namna wala kuzikanusha. Namna hii ndivyo walivyosema Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.

[8] Athar hii imepokelewa na Salaf wengi. Miongoni mwao ni Imaam Maalik, mwalimu wake Rabiy´ah bin Abiy ´Abdir-Rahmaan, Imaam ash-Shaafi´iy, al-Awzaa´iy, ath-Thawriy na wengineo.

[9] al-Khallaal katika "as-Sunnah" (01/243), al-Aajurriy katika "ash-Shariy´ah" (720), "at-Tawhiyd" (794) (03/307), al-Lalakaa´iy katika "Sharh ´Aqiydah Ahl-is-Sunnah wal-Jamaa´ah" (930) (03/527), asw-Swaabuuniy katika "´Aqiydat-us-Salaf wa Aswhaab-il-Hadiyth" (249).

## 13. Mitume ni wakweli katika yale waliyoeleza juu ya Allaah

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Halafu Mitume Wake ni wakweli na ni wenye kusadikishwa, tofauti na wale wanaosema juu Yake yale wasioyajua. Na kwa ajili ya hii ndio maana amesema (Subhaanahu wa Ta´ala):*

سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ وَسَلَامٌ عَلَى الْمُرْسَلِينَ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

*"Ametakasika Mola wako Mola Mtukufu kutokana na yote wanayoelezea na amani iwe juu ya Mitume na himidi zote ni za Mola wa walimwengu."* ***(37:181-182)***

*Hivyo kaelezea kuitakasa nafsi Yake Mwenyewe kwa waliyomuelezea wale waendao kinyume na Mitume, akawasalia Mitume Wake kuonyesha dalili ya usalama wa waliyoyasema katika mapungufu na aibu.*

**MAELEZO**

**Halafu Mitume Wake ni wakweli... -** Amejieleza juu ya Nafsi Yake Mwenyewe, kama ambavyo mwandishi (Rahimahu Allaah) alivyotangulia kutaja kuhusu kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, siku ya Mwisho na Qadar na kwamba Yeye ni mjuzi zaidi juu ya Nafsi Yake na viumbe Wake na kwamba halinganishwi na viumbe Wake (Subhaanahu wa Ta´ala).

Kisha Mitume Wake pia ni wakweli na ni wenye kusadikishwa katika yale waliyoelezea. Yale ambayo Qur-aan inaelezea Mitume pia (´alayhimus-Swalaatu was-Salaam) wameyaelezea. Mbora wao, kiongozi wao na wa mwisho wao ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambaye ameeleza kuwa Yeye (Subhaanah) ndiye yuko juu kabisa, amelingana juu ya ´Arshi, Yeye ndiye mwenye kutoa na kuzuia, Yeye ndiye ambaye juu ya kila kitu ni Muweza na kwamba Yeye ndiye Mwenye kustahiki kuabudiwa. Sunnah imekuja kwa sifa Zake kuu (Subhaanah) na kwamba Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) ndiye Mungu wa haki anayestahiki. Mitume (´alayhimus-Swalaatu was-Salaam) ni wakweli katika yale waliyoelezea kuhusu Allaah.

## 14. Uwajibu wa kuamini yale waliyokuja nayo Mitume

**Halafu Mitume Wake ni wakweli na ni wenye kusadikishwa... -** Ni wajibu kwa kila yule ambaye ´ibaadah ni yenye kumuwajibikia kuwasadikisha. Hawakuleta chochote kutoka kwa Allaah isipokuwa ni cha kweli. Kwa hivyo wao ni wakweli na ni wenye kusadikishwa. Lililo la wajibu kwa kila yule ambaye ´ibaadah ni yenye kumuwajibikia kuwasadikisha na kutendea kazi yale waliyokuja nayo. Kila Ummah unatakiwa utendee kazi yale yaliyoletwa na Mtume wao. Mtume wa Ummah huu ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ni wajibu kwao kufuata yale aliokuja nayo na kunyenyekea Shari´ah yake. Amesema (Ta´ala):

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا

**"Na lolote lile analokupeni Mtume basi lichukueni, na lolote lile analokukatazeni, basi acheni." (59:07)**

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

**"Sema: "Hakika mimi ni Mtume wa Allaah kwenu nyinyi nyote." (07:158)**

Ni wajibu kwa kila ambaye ´ibaadah ni yenye kumuwajibikia kufuata zile hukumu ambazo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amekuja nazo. Sawa hukumu hizo ziwe zinahusiana na mambo ya kufanya au ya kuacha.

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja vilevile na yale aliyoelezea juu ya majina na sifa za Allaah. Ni wajibu kumsadikisha katika hayo na kuamini majina na sifa zote alizoelezea juu ya Allaah. Mtu aamini pasi na kufananisha. Badala yake mtu anatakiwa aamini na wakati huo huo amtakase Allaah na kushabihiana na viumbe Vyake na iwe ni utakaso usiokuwa ndani yake na ukanushaji. Kwa ajili hiyo ndio maana amesema (Rahimahu Allaah):

"... tofauti na wale wanaosema juu Yake yale wasioyajua."

Hawa ni wale makafiri na wajinga. Kwa ajili hii ndio maana ameitakasa nafsi Yake kwa yale waliyosema waongo pale aliposema (Ta´ala):

سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ وَسَلَامٌ عَلَى الْمُرْسَلِينَ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

**"Ametakasika Mola wako Mola Mtukufu kutokana na yote wanayoelezea na amani iwe juu ya Mitume na himidi zote ni za Mola wa walimwengu." (37:181-182)**

Amejihimidi Mwenyewe kwa sababu Yeye ni mkamilifu katika dhati Yake, majina na sifa Zake. Akasema:

وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

**"Na himidi zote ni za Mola wa walimwengu."**

Vilevile amejitakasa Mwenyewe kwa yale waliyosema wale wenye kwenda kinyume na Mitume miongoni mwa maadui zao pale aliposema:

سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ

**"Ametakasika Mola wako Mola Mtukufu kutokana na yote wanayoelezea."**

Bi maana yale ambayo maadui wa Allaah wanamuelezea kwayo katika makafiri ambapo wamemnasibishia mwana, mke na mshirika. Yote haya ni batili. Kwa ajili hiyo ndio maana amejitakasa Mwenyewe. Hakujichukulia mke wala mtoto.

Hakika Yeye (Subhaanah) yupekee na ndiye Mwenye kukusudiwa na hana mshirika. Yeye ndiye Mungu wa haki. Amesema (Ta´ala):

وَإِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ ۖ لَّا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الرَّحْمَٰنُ الرَّحِيمُ

**"Na Mungu wenu ni Allaah Mungu Mmoja Pekee, hapana mungu wa haki ila Yeye. Mwingi wa Rahmah, Mwenye kurehemu." (02:163)**

Halafu akawasalia Mitume kutokana na usalama wa yale mapungu na aibu walizokanusha pale aliposema:

وَسَلَامٌ عَلَى الْمُرْسَلِينَ

**"Na amani iwe juu ya Mitume."**

Amefanya hivi kwa sababu Mitume wamejisalimisha kwa Allaah kutokana na yale aliyowaeleza juu Yake na wakanyenyekea Kwake na hatimaye wakawafikishia watu. Wao wako salama na wamesalimishwa, ni wakweli na wamesadikishwa. Kisha akajihimidi Nafsi Yake pale aliposema:

وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

**"Na himidi zote ni za Mola wa walimwengu."**

kutokana na ukamilifu wa dhati, sifa na matendo Yake (Subhaanahu wa Ta´ala). Yeye ana himdi kamilifu.

## 15. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan I

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Na Yeye (Subhaanah) kwa yale aliyojisifia na kujiita kwayo Nafsi Yake, kajumuisha baina ya ukanushaji na uthibitisho. Hivyo hakuna upotofu wowote kwa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah kwa yale waliyokuja nayo Mitume, kwani hakika ni Njia iliyonyooka; Njia ambayo Kawaneemesha Kwayo waifuatayo, miongoni mwa Manabii, wakweli, mashahidi na waja wema.*

*Kunaingia katika haya yale aliyojisifia Allaah Nafsi Yake Mwenyewe katika Suurah "al-Ikhlaasw", ambayo ni sawa na theluthi ya Qur-aan, ambapo Kasema:*

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ اللَّهُ الصَّمَدُ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

*"Sema: "Yeye ni Allaah Mmoja Pekee. Allaah ambaye ni Mwenye kukusudiwa. Hakuzaa na wala Hakuzaliwa. Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye."***(112:01-04)**

اللَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ۚ لَا تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلَا نَوْمٌ ۚ لَّهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ مَن ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِندَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۚ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ ۖ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ ۚ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ ۖ وَلَا يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا ۚ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ

*"Allaah, hakuna mungu wa haki ila Yeye - Aliyehai daima, Msimamizi wa kila kitu. Haumchukuwi usingizi wala kulala. Ni Vyake pekee vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi. Nani huyu ambaye anashufai [anayeombea] mbele Yake bila ya idhini Yake. Anajua yaliyo mbele yao [viumbe] na yaliyo nyuma yao. Wala hawakizunguki chochote kile katika Elimu Yake isipokuwa kwa Alitakalo. Kursiy Yake imeenea mbingu na ardhi. Wala hakumchoshi kuvihifadhi viwili hivyo. Na Yeye ndiye aliye juu, na ndiye mkuu."***(02:255)**

MAELEZO

**Na Yeye (Subhaanah) kwa yale aliyojisifia na kujiita kwayo Nafsi Yake... -** Bi maana katika Aayah na Hadiyth nyingi. Ukanushaji umekuja kwa njia ya ujumla

na uthibitisho umekuja kwa njia ya upambanuzi. Huu ndio mfumo wa Qur-aan na Sunnah ambapo ukanushaji unakuwa kijumla:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye." (42:11)**

فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

**"Basi msimfanyie Allaah waliolingana naye [washirika] na hali ya kuwa nyinyi mnajua [kuwa hana]." (02:22)**

هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

**"Je, unamjua [mwengine] mwenye Jina kama Lake?" (19:65)**

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye." (112:04)**

Kuna Aayah nyenginezo nyingi.

Uthibitisho unakuwa kwa njia ya upambanuzi:

وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

**"Naye ni Mwenye nguvu kabisa, Mwenye hikmah." (14:04)**

لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ

**"Ni Mwenye huruma mno, Mwenye kurehemu." (02:143)**

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ اللَّهُ الصَّمَدُ

**"Sema: "Yeye ni Allaah Mmoja Pekee. Allaah ni Mwenye kukusudiwa"." (112:01-02)**

غَفُورٌ رَّحِيمٌ

**"Ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu." (02:218)**

هُوَ الْمَلِكُ الْقُدُّوسُ السَّلَامُ

**"Yeye Ndiye ndiye Mfalme, Mtakatifu, Mwenye amani." (59:23)**

Kuna Aayah nyenginezo zilizofafanuliwa kuhusu sifa na majina Yake (Subhnaanahu wa Ta´ala).

Katika Aayah za Qur-aan na Sunnah amekusanya kati ya ukanushaji na uthibitisho. Ukanushaji unakuwa kwa njia ya ujumla ambapo ndani yake unamtakasa Allaah na yale yote ambayo hayalingani Naye na kumtakasa (Subhaanahu wa Ta´ala) kutokana na yale wanayosema maadui wa Mitume (´alayhimus-Salaam). Sambamba na hilo ndani yake kunakuwa kuthibitisha majina na sifa Zake (Subhaanahu wa Ta´ala) kwa njia ya upambanuzi.

## 16. Hii ndio njia wanayofuata Ahl-us-Sunnah al-Jamaa´ah

**Hakuna upotofu wowote kwa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah… -** Hakuna upotofu wowote kwa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah kwa yale waliyokuja nayo Mitume kwa sababu ndio Njia ilinyooka. Njia hiyo ni kumpwekesha Allaah, kumtii, kuamini majina na sifa Zake na kwamba Yeye hana anayeshabihiana Naye, hana anayelingana Naye na wala hana mshirika (Subhaanahu wa Ta´ala). Hii ndio njia iliyonyooka. Njia ambayo Allaah amesema juu yake:

اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ

**"Tuongoze njia iliyonyooka." (02:06)**

Njia hiyo ni:

الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِم مِّنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ

**"Wale Allaah Aliowaneemesha miongoni mwa Manabii na wakweli na mashuhadaa na waja wema." (04:69)**

Njia yao ni kumuamini Allaah na majina na sifa Zake na wakati huo huo mtu amtakase Allaah kufanana na viumbe Wake na badala yake amsifu kwa sifa kamilifu, kutii maamrisho Yake, kujiepisha makatazo Yake na kusimama katika mipaka Yake. Hii ndio njia iliyonyooka. Njia hiyo ni ile:

الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِم مِّنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ

**"Wale Allaah Aliowaneemesha miongoni mwa Manabii na wakweli na Mashuhadaa na waja wema."**

## 17. Allaah ametakasika na mapungufu na kasoro aina zote

**Na Yeye (Subhaanah) kwa yale aliyojisifia na kujiita kwayo... -** Amekusanya kati ya upambanuzi katika kuthibitisha na ujumla katika ukanushaji pale aliposema:

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ اللَّهُ الصَّمَدُ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Sema: "Yeye ni Allaah Mmoja Pekee. Allaah ambaye ni Mwenye kukusudiwa. Hakuzaa na wala Hakuzaliwa. Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye."(112:01-04)**

Amesema kuwa Yeye ndiye Allaah, Mmoja Pekee na ndiye Mwenye kukusudiwa. Halafu akasema:

لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ

**"Hakuzaa na wala Hakuzaliwa."**

Huu ni ufafanuzi maalum ambapo ndani yake amekanusha kuwa na mwana, kwa sababu jambo hilo linapelekea katika mapungufu. Kisha akasema (Ta´ala):

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye." (112:04)**

Ni kama mfano wa maneno Yake (Ta´ala):

هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

**"Je, unamjua [mwengine] mwenye Jina kama Lake?" (19:65)**

فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

**"Basi msimfanyie Allaah waliolingana naye [washirika] na hali ya kuwa nyinyi mnajua [kuwa hana]." (02:22)**

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)**

## *Dalili ya uhai wa Allaah*

اللَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ۚ لَا تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلَا نَوْمٌ

**"Allaah, hakuna mungu wa haki ila Yeye - Aliyehai daima, Msimamizi wa kila kitu. Haumchukuwi usingizi wala kulala." (02:255)**

Amejikanushia kuchukuliwa na usingizi na kulala. Usingizi ni mzito zaidi kuliko kulala. Amejikanushia haya kwa sababu Yeye (Subhaanah) anasifika kuwa na uhai ulio mkamilifu. Kwa sababu ulalaji na usingizi ni upungufu katika uhai. Kwa ajili hiyo Allaah akawa ni mwenye kutakasika na hayo. Yeye ni ambaye yuhai na hafi. Kulala ni aina ya kufa. Hakika Yeye (Subhaanah) yuhai na hafi.

لَّهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

**"Ni Vyake pekee vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi."**

Bi maana Yeye ndiye mfalme wa kila kitu.

مَن ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِندَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ

**"Nani huyu ambaye anashufai mbele Yake bila ya idhini Yake."**

Bi maana hakuna yeyote atayeombea mbele Yake siku ya Qiyaamah isipokuwa kwa idhini Yake. Mitume na waja wema wataombea baada ya kupata idhini Yake (Subhaanahu wa Ta´ala).

Kuhusiana na duniani Allaah (Subhaanah) amewaamrisha watu wote wamuombee Yeye Pekee du´aa na wawaombee uombezi ndugu zao duniani kwa ajili ya Allaah. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa anaombea

pindi anapotakwa uombezi. Pindi mmoja katika watu anapomuomba uombezi na amtatulie tatizo anamuombea (´alayhis-Swalaatu was-Salaam)[10].

Kuhusiana na siku ya Qiyaamah hakuna yeyote atayeombea uombezi isipokuwa kwa idhini Yake (Subhaanahu wa Ta´ala). Ama duniani wanaombea kwa idhini Yake ya kijumla. Kwa sababu ameidhinisha katika Shari´ah waumini kuombeana idhini kati yao. Amesema (Ta´ala):

مَّن يَشْفَعْ شَفَاعَةً حَسَنَةً يَكُن لَّهُ نَصِيبٌ مِّنْهَا ۖ وَمَن يَشْفَعْ شَفَاعَةً سَيِّئَةً يَكُن لَّهُ كِفْلٌ مِّنْهَا

**"Atakayeombea uombezi mzuri atapata fungu lake, na atakayeombea uombezi mbaya atapata sehemu yake." (04:85)**

Amewaidhinisha (Subhaanah) na kuwasisitiza kufanya hivo; wasaidiane katika wema na uchaji Allaah, wapeana nasaha na kuusiana kwa haki. Uombezi unaingia katika kuusiana kwa haki na ni katika kufanya wema. Uombezi unajuzu duniani kwa idhini Yake (Subhaanah) ya kijumla. Ama kuhusu Aakhirah uombezi hautofaa isipokuwa baada ya kupata idhini Yake maalum. Hakuna yeyote atayeombea isipokuwa kwa idhini Yake (Subhaanah). Kwa ajili hii watu siku ya Qiyaamah watamwendea Aadam, Nuuh, Ibraahiym na Muusa, ´Iysaa (´alayhimus-Salaam) ambapo wote wataomba udhuru. Hatimaye waende kwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) asujudu mbele ya Mola Wako chini ya ´Arshi, kisha amhimidi Allaah kwa himdi kubwa na halafu baada ya hapo ndio ampe idhini na kumwambia:

"Ombea utapewa."

Aayah hii ambayo ni Aayat al-Kursiy ndio Aayah kubwa katika Qur-aan. Ndani yake mna uthibitisho na ukanushaji:

اللَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ

**"Allaah, hakuna mungu wa haki ila Yeye - Aliyehai daima, Msimamizi wa kila kitu."**

[10] Tazama al-Bukhaariy (5652) na Muslim (2576).

Huu ni uthibitisho.

لَا تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلَا نَوْمٌ

**"Haumchukuwi usingizi wala kulala."**

Huu ni ukanushaji.

لَّهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

**"Ni Vyake pekee vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi."**

Huu ni uthibitisho.

مَن ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِندَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ

**"Nani huyu ambaye anashufai [anayeombea] mbele Yake bila ya idhini Yake."**

Huu ni uthibitisho.

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ

**"Anajua yaliyo mbele yao [viumbe] na yaliyo nyuma yao."**

Huu ni uthibitisho.

وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ ۚ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ ۖ وَلَا يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا ۚ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ

**"Wala hawakizunguki chochote kile katika Elimu Yake isipokuwa kwa Alitakalo. Kursiy Yake imeenea mbingu na ardhi. Wala hakumchoshi kuvihifadhi viwili hivyo. Na Yeye ndiye aliye juu, na ndiye mkuu."** **(02:255)**

Amebainsiha ukamilifu Wake na kwamba Yeye ni ndiye aliye juu na mkuu na kwamba Yeye ana uhai mkamilifu na kwamba Yeye ni aliye hai na kwamba ndiye Msimamizi wa kila kitu na kwamba Yeye ndiye Mwenye kumiliki kila kitu. Lililo la wajibu ni kunyenyekea Kwake na kumuomba (Subhaanahu wa Ta´ala) na kumwelekea katika kila jambo. Mambo yote yanapitika kupitia Mikono Yake. Ndio maana amesema (Subhaanah):

ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ

**"Niombeni, Nitakuitikieni." (40:60)**

وَاسْأَلُوا اللَّهَ مِن فَضْلِهِ

**"Na muombeni Allaah fadhila Zake." (04:32)**

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ

**"Na watakapokuuliza waja Wangu kuhusu Mimi, basi Mimi Niko karibu Naitikia du'aa ya muombaji anaponiomba." (02:186)**

## 18. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan II

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Amesema (Subhaanah):*

هُوَ الْأَوَّلُ وَالْآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

*"Yeye Ndiye wa Mwanzo na wa Mwisho na Aliye juu na Aliye Karibu, Naye kwa kila kitu ni Mjuzi."* ***(57:03)***

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْحَيِّ الَّذِي لَا يَمُوتُ

*"Na mtegemee Aliye hai Ambaye Hafi."* ***(25:58)***

وَهُوَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ

*"Naye Ndiye Mjuzi, Mwenye hikmah."* ***(66:02)***

وَهُوَ الْحَكِيمُ الْخَبِيرُ

*"Naye ndiye Mwenye hikmah, Mjuzi."* ***(06:18)***

يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنزِلُ مِنَ السَّمَاءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا

*"Anajua yale yote yanayoingia ardhini na yale yote yanayotoka humo, na yale yote yanayoteremka kutoka mbinguni na yale yote yanayopanda huko."* ***(34:02)***

وَعِندَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ ۚ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ ۚ وَمَا تَسْقُطُ مِن وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلُمَاتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ

*"Na Kwake Pekee zipo funguo za ghayb; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Anajua yale yote yaliyomo barani na baharini. Na halianguki jani lolote ila Hulijua. Na wala [haianguki] punje katika viza vya ardhi, na wala [hakianguki] kilichorutubika na wala [hakianguki]*

*kikavu isipokuwa [kimeandikwa] katika Kitabu kinachobainisha.”* ***(06:59)***

وَمَا تَحْمِلُ مِنْ أُنثَىٰ وَلَا تَضَعُ إِلَّا بِعِلْمِهِ

*“Na mwanamke yeyote yule habebi [mimba] na wala hazai isipokuwa kwa ujuzi Wake.”* ***(35:11)***

لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

*”Ili mjue kwamba Allaah juu ya kila kitu ni Muweza na kwamba Allaah Amekwishakizunguka kila kitu kwa ujuzi.”* ***(65:12)***

إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ

*”Hakika Allaah Ndiye Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu kali madhubuti.”* ***(51:58)***

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

*“Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye Ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona.”* ***(42:11)***

إِنَّ اللَّهَ نِعِمَّا يَعِظُكُم بِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ سَمِيعًا بَصِيرًا

*”Hakika [mawaidha] Anayokuwaidhini nayo Allaah ni mazuri kabisa; hakika Allaah ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.”* ***(04:58)***

وَلَوْلَا إِذْ دَخَلْتَ جَنَّتَكَ قُلْتَ مَا شَاءَ اللَّهُ لَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ

*“Na lau ulipoingia bustanini mwako ungelisema: "Ametaka Allaah; hapana nguvu ila kwa Allaah.”* ***(18:39)***

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا اقْتَتَلُوا وَلَٰكِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ

*"Na lau Angelitaka Allaah wasingelipigana lakini Allaah Anafanya Ayatakayo."* ***(02:153)***

أُحِلَّتْ لَكُم بَهِيمَةُ الْأَنْعَامِ إِلَّا مَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ غَيْرَ مُحِلِّي الصَّيْدِ وَأَنتُمْ حُرُمٌ ۗ إِنَّ اللَّهَ يَحْكُمُ مَا يُرِيدُ

*"Imehalalishwa kwenu wanyama wenye miguu minne isipokuwa mnaosomewa [kuwa ni haraam]. Lakini msihalalishe kuwinda hali mkiwa katika Ihraam. Hakika Allaah Anahukumu Atakayo."* ***(05:01)***

فَمَن يُرِدِ اللَّهُ أَن يَهْدِيَهُ يَشْرَحْ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ ۖ وَمَن يُرِدْ أَن يُضِلَّهُ يَجْعَلْ صَدْرَهُ ضَيِّقًا حَرَجًا كَأَنَّمَا يَصَّعَّدُ فِي السَّمَاءِ

*"Basi yule ambaye Allaah Anataka kumwongoza, Humfungulia kifua chake kwa Uislamu. Na yule ambaye Anataka kumpoteza Humjaalia kifua chake kuwa na dhiki chenye kubana kama kwamba anapanda mbinguni kwa tabu."* ***(06:125)***

**MAELEZO**

Aayah hizi Allaah amekusanya ndani yake yale aliyojiita na kujisifu kwayo Mwenyewe baina ya ukanushaji na uthibitisho. Allaah anathibitishiwa sifa kamilifu na anakanushiwa sifa zilizo na mapungufu na aibu. Tumetangulia kuizungumzia Aayat al-Kursiy na Suurah "al-Ikhlaasw" na faida zinazopatikana ndani yake. Amesema (Ta´ala):

## *Dalili kwamba Allaah ndiye wa Mwanzo na wa Mwisho*

هُوَ الْأَوَّلُ وَالْآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

**"Yeye Ndiye wa Mwanzo na wa Mwisho na Aliye juu na Aliye Karibu, Naye kwa kila kitu ni Mjuzi ."(57:03)**

Amethibitisha (Subhaanah) ya kwamba Yeye ni wa Mwanzo ambaye hakuna kitu kabla Yake. Hivyo ndivyo amesema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Ee Allaah! Hakika Wewe ndiye wa Mwanzo na hakuna kitu kabla Yako, Wewe ndiye wa Mwisho na hakuna kitu baada Yako, Wewe ndiye ulie Juu na hakuna kitu juu Yako."[11]

*adhw-Dhwaahir* [Aliye juu], bi maana Yeye ndiye Yuko juu ya viumbe vyote. Kwa msemo mwingine hakuna kitu kilicho juu Yake.

[11] Muslim (2713).

*al-Baatwin* [Aliye karibu], bi maana hakuna kitu kilicho karibu kuliko Yeye. Kwa msemo mwingine anakijua kila kitu. Hakuna chenye kufichikana Kwake.

Kadhalika Aayah nyienginezo baada yake zinazozungumzia juu ya Ujuzi:

وَهُوَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ

**"Naye Ndiye Mjuzi, Mwenye hikmah."(66:02)**

لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

**"Ili mjue kwamba Allaah juu ya kila kitu ni Muweza na kwamba Allaah Amekwishakizunguka kila kitu kwa ujuzi."(65:12)**

Vilevile Aayah nyenginezo ambazo zimetaja Ujuzi na hekima. Kwa mfano:

إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

**"Hakika Allaah ni Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika, Mwenye hikmah." (02:220)**

Aayah zilizotaja riziki na nguzu. Kwa mfano:

## *Dalili ya Nguvu na Kuruzuku kwa Allaah*

إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ

**"Hakika Allaah Ndiye Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu kali madhubuti."(51:58)**

Aayah zilizotaja utashi, matakwa na kadhalika. Zote hizi zinaonyesha ukubwa Wake (Subhaanah), kwamba Yeye ana utashi kamilifu, matakwa kamilifu, elimu kamilifu na uwezo kamilifu. Zote hizi ni sifa Zake (Jalla wa ´Alaa). Lakini hata hivyo zinatakiwa kuthibitishwa kwa njia isiyofanana na viumbe. Bi maana Ana nguvu lakini sio kama nguvu za viumbe. Yeye nguvu Zake ni kamilifu kabisa. Vivyo hivyo inahusiana na sifa Zake zingine zote. Siza Zake zote ni kamilifu. Kwa ajili hii ndio maana amesema:

## *Dalili ya Allaah kutolingana na chochote na kuwa na mwenza*

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye." (42:11)**

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ

**"Basi msimpigie mifano!" (16:74)**

هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

**"Je, unamjua [mwengine] mwenye Jina kama Lake?" (19:65)**

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye." (112:04)**

Elimu Yake ni kamilifu na sio kama elimu ya viumbe. Hakuna chochoye chenye kufichikana Kwake. Vivyo hivyo hekima Yake, uwezo Wake, nguvu Zake, upole Wake, usikizi Wake na uoni Wake. Zote hizi ni sifa kamilifu. Sifa hizi hazina upungufu wowote ndani yake. Hili ni tofauti na sifa za viumbe ambapo zina upungufu na ni dhaifu. Kuhusu Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) sifa Zake zote ni kamilifu. Amesema (Ta´ala):

## *Dalili ya Kuona na Kusikia kwa Allaah*

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye Ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)**

Hili ni kutokana na ukamilifu Wake:

هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

**"Je, unamjua [mwengine] mwenye Jina kama Lake?" (19:65)**

Kwa msemo mwingine hana samiya mwenye kulingana Naye kutokana na ukamilifu Wake.

## *Dalili ya Utashi na Matakwa ya Allaah*

Vilevile Allaah anasifika kuwa na matakwa. Maana yake ni utashi wa kilimwengu. Kwa msemo mwingine matakwa Yake ni yenye kutendeka na hayarudishwi/hayazuiwi na kitu. Kile anachotaka Allaah ndio huwa, sawa iwe ni mauti, uhai, kuwafanya watu fulani wawe na nguvu, kuwafanya watu wengine wawe madhalili, kuwaondoshea watu fulani ufalme, kuwafanya watu fulani wawe na ufalme, kuwafanya watu fulani wapate watoto au kutowapata. Yote hayo ni yenye kutendeka pale Allaah anapotaka. Amesema (Ta´ala):

لِمَن شَاءَ مِنكُمْ أَن يَسْتَقِيمَ وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Kwa yule atakaye miongoni mwenu anyooke. Na hamtotaka isipokuwa Atake Allaah, Mola wa walimwengu." (81:28-29)**

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ

**"Na lau Angetaka Mola wako wasingeliyafanya hayo." (06:112)**

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا اقْتَتَلُوا

**"Na lau Angelitaka Allaah wasingelipigana." (02:253)**

## 19. Aina mbili za utashi

Kuna aina mbili za Utashi:

1- Utashi wa kilimwengu (Kawniyyah). Utashi wa kilimwengu ni kama matakwa. Utashi aina hii ni wenye kutekelezwa na haurudishwi na kitu. Mfano wa maneno Yake (Ta´ala):

فَمَن يُرِدِ اللَّهُ أَن يَهْدِيَهُ يَشْرَحْ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ ۖ وَمَن يُرِدْ أَن يُضِلَّهُ يَجْعَلْ صَدْرَهُ ضَيِّقًا حَرَجًا كَأَنَّمَا يَصَّعَّدُ فِي السَّمَاءِ

**"Basi yule ambaye Allaah Anataka kumwongoza, Humfungulia kifua chake kwa Uislamu. Na yule ambaye Anataka kumpoteza Humjaalia kifua chake kuwa na dhiki chenye kubana kama kwamba anapanda mbinguni kwa tabu."(06:125)**

إِنَّ اللَّهَ يَحْكُمُ مَا يُرِيدُ

**"Hakika Allaah Anahukumu Atakayo." (05:01)**

Huu ni utashi wa kilimwengu wenye kutendeka. Ni kama mfano wa matakwa. Haurudishwi na kitu.

2- Utashi wa kidini (Shar´iyyah). Utashi aina hii maana yake ni kupenda na kuridhia. Utashi huu unaweza kutokea na huenda vilevile usitokee. Mfano wa Kauli Yake (Ta´ala):

يُرِيدُ اللَّهُ لِيُبَيِّنَ لَكُمْ وَيَهْدِيَكُمْ سُنَنَ الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ وَيَتُوبَ عَلَيْكُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ وَاللَّهُ يُرِيدُ أَن يَتُوبَ عَلَيْكُمْ

**"Allaah Anataka kukubainishieni na kukuongozeni nyendo za wale walio kabla yenu na Apokee tawbah kwenu. Na Allaah Mjuzi, Mwenye hikmah. Na Allaah Anataka kupokea tawbah kwenu." (04:26-27)**

Huu ni utashi wa kidini. Unaweza kutokea kama ambavyo vilevile huenda usitokee. Allaah anapenda awaongoze waislamu wote. Allaah anapenda awasamehe. Huu ni utashi wa kidini. Viumbe wengi hawakusamehewa. Viumbe wengi wamekufa juu ya kufuru. Utashi wa kidini unaweza kutokea kama ambavyo vilevile huenda usitokee.

Allaah amependa kidini wanaadamu wakubali haki, wawafuate Mitume na wamtii Allaah. Pamoja na hivyo kuko miongoni mwao ambao wamemtii na wengine wakamuasi. Mwenye kumtii ana Pepo na mwenye kumuasi ana Moto. Amesema (Jalla wa ´Alaa):

تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ ۚ وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ وَذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَتَعَدَّ حُدُودَهُ يُدْخِلْهُ نَارًا خَالِدًا فِيهَا وَلَهُ عَذَابٌ مُّهِينٌ

**"Hiyo ni mipaka ya Allaah. Na yeyote atakayemtii Allaah na Mtume Wake Atamuingiza katika Pepo zipitazo chini yake mito, ni wenye kudumu humo - na huko ndiko kufuzu kukubwa kabisa. Na yeyote atakayemuasi Allaah na Mtume Wake na akapindukia mipaka Yake Atamuingiza Motoni, ni mwenye kudumu humo na atapata adhabu ya kudhalilisha." (04:13-14)**

Wote wamepewa matishio. Mwenye kutii kwa khiyari na kutaka kwake basi ana Pepo. Na yule mwenye kuasi ana Moto. Huu ni utashi wa kidini.

Kuhusiana na utashi hakuna yeyote anaweza kuukwepa. Yale anayotaka Allaah yatokee katika ulimwengu ni lazima yatokee. Kwa mfano Allaah anapotaka kuwaangamiza watu fulani, kuwafanya wawe na nguvu, kumfisha fulani, kumpa uhai, kumhuisha fulani, kumfanya akabaki na mengineyo. Utashi wa kilimwengu ni kama mfano wa matakwa. Matakwa yake ni lazima yatendeke.

## 20. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan III

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Amesema (Ta´ala):*

وَأَحْسِنُوا ۛ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ

*"Na fanyeni wema, Hakika Allaah Anapenda watendao wema."* ***(02:195)***

وَأَقْسِطُوا ۖ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ

*"Na fanyeni haki. Hakika Allaah Anapenda wafanyao haki."* ***(49:09)***

فَمَا اسْتَقَامُوا لَكُمْ فَاسْتَقِيمُوا لَهُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ

*"Basi wakikunyokeeni [kwa uzuri], nanyi wanyokoeeni [kwa uzuri]. Hakika Allaah Anapenda wamchao."* ***(09:07)***

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ

*"Sema: "Mkiwa mnampenda Allaah, basi nifuateni, Atakupendeni Allaah."* ***(03:31)***

فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ

*"Basi Allaah Ataleta watu [badala yao] Atakaowapenda nao watampenda."* ***(05:54)***

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الَّذِينَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِهِ صَفًّا كَأَنَّهُم بُنْيَانٌ مَّرْصُوصٌ

*"Hakika Allaah Anapenda wale wanaopigana katika njia Yake safu kwa safu kama kwamba wao ni jengo linalokamatana barabara."* ***(61:04)***

وَهُوَ الْغَفُورُ الْوَدُودُ

*"Naye ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye mapenzi halisi."* ***(85:14)***

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

*"Kwa Jina la Allaah Mwingi wa Rahmah, Mwenye kurehemu."* ***(27:30)***

رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَّحْمَةً وَعِلْمًا

*"Mola wetu! Umekienea kila kitu kwa Rahmah na elimu."* ***(40:07)***

وَكَانَ بِالْمُؤْمِنِينَ رَحِيمًا

*"Naye daima kwa Waumini ni Mwenye kuwarehemu."* ***(33:43)***

وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ

*"Na Rahmah Yangu imeenea kila kitu."* ***(07:156)***

كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ

*"Mola wenu Amekidhia juu ya Nafsi Yake Rahmah."* ***(06:54)***

وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

*"Naye ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu."* ***(10:107)***

فَاللَّهُ خَيْرٌ حَافِظًا ۖ وَهُوَ أَرْحَمُالرَّاحِمِينَ

*"Basi Allaah ni Mbora wa kuhifadhi, Naye ni Mbora wa kurehemu kuliko wanaorehemu."* ***(12:64)***

رَّضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ

*"Allaah Ataridhika nao, nao wataridhika Naye."* ***(98:08)***

وَمَن يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُّتَعَمِّدًا فَجَزَاؤُهُ جَهَنَّمُ خَالِدًا فِيهَا وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَلَعَنَهُ وَأَعَدَّ لَهُ عَذَابًا عَظِيمًا

*"Na atakayemuua Muumini kwa kusudi, basi jazaa yake ni [Moto wa] Jahannam, atadumu humo na Allaah Atamghadhibikia na Atamlaani na Atamuandalia adhabu kuu."* ***(04:93)***

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمُ اتَّبَعُوا مَا أَسْخَطَ اللَّهَ وَكَرِهُوا رِضْوَانَهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ

*"Hivyo kwa kuwa wao wamefuata yale yanayomghadhibisha Allaah, na wakachukia radhi Zake, basi Akazibatilisha 'amali zao."* ***(47:28)***

فَلَمَّا آسَفُونَا انتَقَمْنَا مِنْهُمْ

*"Basi walipotukasirisha; Tuliwapatiliza."* ***(43:55)***

وَلَٰكِن كَرِهَ اللَّهُ انبِعَاثَهُمْ فَثَبَّطَهُمْ

*"Lakini Allaah Amechukia kutoka kwao, basi Akawazuia."* ***(09:46)***

كَبُرَ مَقْتًا عِندَ اللَّهِ أَن تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ

*"Ni chukizo kubwa mno mbele ya Allaah kwamba mnasema yale msiyoyafanya."* ***(61:03)***

## MAELEZO

Aayah hizi nyingi ndani yake mna sifa ya kupenda. Allaah amejisifu Mwenyewe kwa sifa ya kupenda, kwamba anapenda na kupendwa na kwamba anawapenda wachaji Allaah, watendao wema, wafanyao uadilifu. Amesema (Ta´ala):

### *Dalili ya Kupenda kwa Allaah*

فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ

**"Basi Allaah Ataleta watu [badala yao] Atakaowapenda nao watampenda."(05:54)**

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ

**”Sema: “Mkiwa mnampenda Allaah, basi nifuateni, Atakupendeni Allaah.” (03:31)**

Vilevile Yeye ni Mwingi wa rehema, mwenye kurehemu; Yeye ni mwenye huruma, huruma Wake umeenea kwenye kila kitu, Yeye ni mwenye kusamehe, mwenye mapenzi, huridhia, hughadhibika, huchukia na hukirihika:

## *Dalili ya Kuridhia na Kughadhibika kwa Allaah*

رَّضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ

**”Allaah Ataridhika nao, nao wataridhika Naye.” (98:08)**

غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِم

**"Allaah Ameghadhibika nao." (48:14)**

اتَّبَعُوا مَا أَسْخَطَ اللَّهَ وَكَرِهُوا رِضْوَانَهُ

**"Wamefuata yale yanayomghadhibisha Allaah na wakachukia radhi Zake." (47:28)**

وَلَٰكِن كَرِهَ اللَّهُ انبِعَاثَهُمْ فَثَبَّطَهُمْ

**”Lakini Allaah Amechukia kutoka kwao, basi Akawazuia.” (09:46)**

Zote hizi ni sifa za haki. Radhi, mapenzi, kukasirika na kuchukia. Zote hizi anasifiwa nazo (Jalla wa ´Alaa). Ni kama sifa nyenginezo ambazo zinalingana na Allaah peke Yake. Mtu anatakiwa kuzithibitisha bila ya kupotosha, kukanusha, kuzifanyia namna na kuzipigia mfano. Kupenda Kwake sio kama wanavyopenda viumbe, kuridhia Kwake sio kama kuridhia kwa viumbe, kuchukia Kwake sio kama wanavyochukia viumbe. Vivyo hivyo inahusiana na sifa nyenginezo. Mlango ni ule ule mmoja. Amesema (Ta´ala):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**“Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye Ndiye Mwenye kusikia,**

**Mwenye kuona.” (42:11)**

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**“Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye.” (112:04)**

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

**”Basi msipigie mifano Allaah! Hakika Allaah Anajua nanyi hamjui.” (16:74)**

Bi maana hana anayefanana Naye. Usimpigie Allaah mifano. Kwani Allaah hana mwenza na hana mshirika. Sifa zote mlango wake ni ule ule mmoja: tunasema kuwa tunamuamini Allaah (Jalla wa ´Alaa) na majina Yake mazuri na sifa Zake kuu zilizothibiti katika Qur-aan na Sunnah Swahiyh kwa njia inayolingana na Allaah. Tunafanya hivyo pasi na kupotosha, kukanusha, kuzifanyia namna na kuzilinganisha. Badala yake tunasema kuwa sifa Zake zote ni haki na majina Yake yote ni mazuri. Tunamthibitishia nayo Allaah kama ambavyo Yeye Mwenyewe (Jalla wa ´Alaa) amevyojithibitishia nayo, Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah zake (Radhiya Allaahu ´anhum). Wameyathibitisha kwa njia inayolingana na Yeye. Sifa Zake hazifanani na sifa za viumbe Wake. Majina Yake hayafanani na majina ya viumbe. Yeye (Subhaanah) ana majina mazuri na yana maana kuu. Kwa ajili hii amesema:

وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا

**"Na Allaah Ana Majina mazuri kabisa, basi muombeni kwayo." (07:180)**

Hili ni kutokana na ukamilifu Wake na ukamilifu wa maana yake. Ndio maana Akayaita (Subhaanahu wa Ta´ala) kuwa ni majina mazuri kabisa.

## 21. Maana ya sifa za Allaah inajulikana na namna haijulikani

Hakuna yeyote anayejua namna sifa Zake zilivyo isipokuwa Yeye peke yake (Subhaanahu wa Ta´ala). Anajua tofauti na tunavyojua, anahurumia tofauti na tunavyohurumia, amelingana tofauti na tunavyolingana, hushuka tofauti na tunavyoshuka, huja tofauti na tunavyokuja na hughadhibika tofauti na tunavyoghadhibika. Vivyo hivyo inahusiana na sifa nyenginezo zote:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)**

Kulingana kunajulikana, huruma unajulikana, kughadhibika kunajulikana, kupenda kunajulikana na kutaka kunajulikana, utashi unajulikana. Ama kuhusu namna yake haijulikani. Hatujui namna alivyolingana. Hatujui namna anavyohurumia. Hatujui yote haya. Allaah Pekee ndiye mwenye kujua haya (Subhaanahu wa Ta´ala). Lakini hata hivyo tunajua kuwa kupenda sio kuchukia, kukasirika sio kuridhia, kuridhia sio kusamehe na kadhalika. Maana ya sifa inajulikana. Lakini haya hivyo namna yake hakuna mwenye kuijua isipokuwa Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala).

Kughadhibika kunajulikana ambako ni kinyume na kuridhia, kupenda ni kinyume na kukasirika, huruma ni kinyume na kupatiliza. Allaah anasifa nazo. Allaah huwahurumia baadhi ya watu na akawaadhibu wengine na wengine akawapatiliza. Huwahurumia watu wenye kupigana katika njia Yake na wengine akawaghadhikia na kuwapatiliza kwa kumuasi na kumkufuru. Hali ni namna hii ambapo Allaah anawapenda baadhi ya watu na wengine anawachukia, anawapa baadhi na wengine anawanyima. Yeye ndiye mwenye kuzuia na kutoa (Jalla wa ´Alaa). Huu ndio mfumo wa Ahl-us-Sunnah. Wanaziamini sifa na wakati huo huo wanaamini kuwa ni haki na kwamba zinalingana na Allaah na kwamba maana yake ni haki. Lakini hakuna anayejua namna yake isipokuwa Yeye Mwenyewe (Subhaanahu wa Ta´ala).

## 22. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan IV

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Amesema (Ta´ala):*

هَلْ يَنظُرُونَ إِلَّا أَن يَأْتِيَهُمُ اللَّهُ فِي ظُلَلٍ مِّنَ الْغَمَامِ وَالْمَلَائِكَةُ وَقُضِيَ الْأَمْرُ

*"Je, wanangojea [nini] isipokuwa Allaah Awajie katika vivuli vya mawingu pamoja na Malaika na itolewe hukumu?"* ***(02:210)***

هَلْ يَنظُرُونَ إِلَّا أَن تَأْتِيَهُمُ الْمَلَائِكَةُ أَوْ يَأْتِيَ رَبُّكَ أَوْ يَأْتِيَ بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ

*"Je, wanangojea jingine [lolote] isipokuwa wawafikie Malaika [kuwatoa roho] au awafikie Mola wako au ziwajie baadhi za alama za Mola wako?"* ***(06:158)***

كَلَّا إِذَا دُكَّتِ الْأَرْضُ دَكًّا دَكًّا وَجَاءَ رَبُّكَ وَالْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا

*"Sivyo hivyo! [Kumbukeni pale] ardhi itakapovunjwavunjwa. Na Atakapokuja Mola wako, na Malaika safu kwa safu."* ***(89:21-22)***

وَيَوْمَ تَشَقَّقُ السَّمَاءُ بِالْغَمَامِ وَنُزِّلَ الْمَلَائِكَةُ تَنزِيلًا

*"Na [kumbusha] Siku itakayopasuka mbingu kwa [kutoa] mawingu; na Malaika watateremshwa mteremsho wa wingi."* ***(25:25)***

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ وَيَبْقَىٰ وَجْهُ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

*"Kila aliyekuwa humo [mbinguni na ardhini] ni mwenye kutoweka. Na utabakia Uso wa Mola wako Mwenye Utukufu na Ukarimu."* ***(55:27)***

كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ

*"Kila kitu ni chenye kuhiliki isipokuwa Uso Wake."* ***(28:88)***

مَا مَنَعَكَ أَن تَسْجُدَ لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ

*"Nini kilichokuzuia usimsujudie Niliyemuumba kwa Mikono Yangu?"* ***(38:75)***

وَقَالَتِ الْيَهُودُ يَدُ اللَّهِ مَغْلُولَةٌ ۚ غُلَّتْ أَيْدِيهِمْ وَلُعِنُوا بِمَا قَالُوا ۘ بَلْ يَدَاهُ مَبْسُوطَتَانِ يُنفِقُ كَيْفَ يَشَاءُ

*"Na Mayahudi wakasema: "Mkono wa Allaah umefumbwa." [Siyo, bali] mikono yao ndio iliyofumbwa; na wamelaaniwa kwa yale waliyoyasema. Bali Mikono Yake imefumbuliwa Hutoa Atakavyo."* ***(05:64)***

وَاصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ فَإِنَّكَ بِأَعْيُنِنَا

*"Na subiri kwa hukumu ya Mola wako, kwani hakika wewe uko kwenye Macho yetu."* ***(52:48)***

وَحَمَلْنَاهُ عَلَىٰ ذَاتِ أَلْوَاحٍ وَدُسُرٍ تَجْرِي بِأَعْيُنِنَا

*"Na Tukambeba kwenye ile [jahazi] iliyo [tengenezwa] kwa mbao na misumari. Inatembea kwa Macho Yetu."* ***(54:13-14)***

وَأَلْقَيْتُ عَلَيْكَ مَحَبَّةً مِّنِّي وَلِتُصْنَعَ عَلَىٰ عَيْنِي

*"Na Nikakutilia mahaba kutoka Kwangu na ili ulelewe Machoni Mwangu."* ***(20:39)***

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا ۚ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ

*"Allaah Amekwishasikia kauli ya yule [mwanamke] anayejadiliana nawe kuhusu mumewe na anamshitakia Allaah; na Allaah Anayasikia majibizano yenu. Hakika Allaah ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona."* ***(58:01)***

لَّقَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ فَقِيرٌ وَنَحْنُ أَغْنِيَاءُ

*"Kwa yakini Allaah Ameisikia kauli ya wale [Mayahudi] ambao wamesema: "Hakika*

*Allaah ni fakiri na sisi ni matajiri".”* ***(03:181)***

أَمْ يَحْسَبُونَ أَنَّا لَا نَسْمَعُ سِرَّهُمْ وَنَجْوَاهُم ۚ بَلَىٰ وَرُسُلُنَا لَدَيْهِمْ يَكْتُبُونَ

*”Au wanadhania kwamba Sisi Hatusikii siri zao na minong'ono yao? Sivyo! [Tunasikia!] Na Wajumbe wetu wako kwao wanaandika.”* ***(43:80)***

إِنَّنِي مَعَكُمَا أَسْمَعُ وَأَرَىٰ

*”Hakika Mimi Niko pamoja nanyi, Nasikia na Naona.”* ***(20:46)***

أَلَمْ يَعْلَم بِأَنَّ اللَّهَ يَرَىٰ

*”Je, hajui kwamba Allaah Anaona?”* ***(96:14)***

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ الَّذِي يَرَاكَ حِينَ تَقُومُ

*”Na mtegemee Mwenye nguvu kabisa, Mwenye kurehemu - Ambaye Anakuona wakati unaposimama.”* ***(26:217-218)***

وَقُلِ اعْمَلُوا فَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ

*”Na sema [uwaambie]: Fanyeni [mtakavyo]. Allaah Ataona 'amali zenu na Mtume Wake, na Waumini.”* ***(09:105)***

وَهُوَ شَدِيدُ الْمِحَالِ

*”Naye ni Mkali wa kusibu misiba na maangamizi.”* ***(13:13)***

وَمَكَرُوا وَمَكَرَ اللَّهُ ۖ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَاكِرِينَ

*”Na wakapanga njama, lakini Allaah Akapanga [kuwalipiza] njama. Na Allaah ni Mbora wa kurudisha njama za wenye kupanga njama.”* ***(03:54)***

وَمَكَرُوا مَكْرًا وَمَكَرْنَا مَكْرًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ

*"Wakapanga njama Nasi Tukapanga mipango ya kuvurumisha njama [zao kwa kuwaadhibu], nao huku hawatambui."* ***(27:50)***

إِنَّهُمْ يَكِيدُونَ كَيْدًاوَأَكِيدُ كَيْدًا

*"Hakika wao wanapanga njama Nami napanga mipango [ya kuvunja na kupindua njama zao]."* ***(86:15-16)***

## Dalili ya Kusamehe, Kurehemu na Uwezo wa Allaah

إِن تُبْدُوا خَيْرًا أَوْ تُخْفُوهُ أَوْ تَعْفُوا عَن سُوءٍ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفُوًّا قَدِيرًا

*"Mkidhihirisha kheri au mkiificha au mkisamehe uovu; basi hakika Allaah ni Mwingi wa kusamehe, Muweza."* ***(04:149)***

وَلْيَعْفُوا وَلْيَصْفَحُوا ۗ أَلَا تُحِبُّونَ أَن يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

*"Na wasamehe na waachilie mbali. Je, [nyinyi] hampendi Allaah Akusameheni? Na Allaah ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu."* ***(24:22)***

وَلِلَّهِ الْعِزَّةُ وَلِرَسُولِهِ وَلِلْمُؤْمِنِينَ

*"Na hali utukufu ni wa Allaah na wa Mtume Wake na wa Waumini."* ***(63:08)***

فَبِعِزَّتِكَ لَأُغْوِيَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ

*"Naapa kwa Utukufu Wako, bila shaka nitawapotosha wote."****(38:82)***

تَبَارَكَ اسْمُ رَبِّكَ ذِي الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

*"Limebarikika Jina la Mola wako - Mwenye Utukufu na Ukarimu."****(55:78)***

فَاعْبُدْهُ وَاصْطَبِرْ لِعِبَادَتِهِ ۚ هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

*"Basi mwabudu Yeye tu na dumisha subira katika 'ibaadah Yake. Je, unamjua [mwengine] mwenye Jina Lake?* ***(19:65)***

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

*"Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye."* ***(112:04)***

**MAELEZO**

Aayah zote hizi tukufu ndani yake mna jumla ya sifa kwa Mola (´Azza wa Jall). Ni wajibu kumthibitishia nazo Allaah (Subhaanah) kwa njia inayolingana Naye pasi na upotoshaji, ukanushaji, kuzifanyia namna wala kuzilinganisha. Miongoni mwazo ni pamoja na Kauli Yake (Jalla wa ´Alaa):

## *Dalili ya Kuja na Kuwasili kwa Allaah*

هَلْ يَنظُرُونَ إِلَّا أَن يَأْتِيَهُمُ اللَّهُ فِي ظُلَلٍ مِّنَ الْغَمَامِ وَالْمَلَائِكَةُ وَقُضِيَ الْأَمْرُ

**"Je, wanangojea [nini] isipokuwa Allaah Awajie katika vivuli vya mawingu pamoja na Malaika na itolewe hukumu?" (02:210)**

وَجَاءَ رَبُّكَ وَالْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا

**"Na Atakapokuja Mola wako na Malaika safu kwa safu."(89:22)**

Ni kuhusu kuja kwa Allaah siku ya Qiyaamah. Kuja siku ya Qiyaamah ni haki kwa njia inayolingana na Allaah. Allaah hashabihiani na viumbe Vyake kwa chochote katika sifa Zake. Amesema (Ta´ala):

أَوْ يَأْتِيَ رَبُّكَ

**"... au ziwajie baadhi za alama za Mola wako"(06:158)**

Ni kuchomoza kwa jua kutoka magharibi.

## *Dalili ya Uso wa Allaah*

وَيَبْقَىٰ وَجْهُ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

**"Na utabakia Uso wa Mola wako - Mwenye Utukufu na Ukarimu."(55:27)**

كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ

**"Kila kitu ni chenye kuhiliki isipokuwa Uso Wake." (28:88)**

Hapa kuna uthibitisho wa Uso wa haki. Ni Uso mtukufu.

## *Dalili ya Mikono ya Allaah*

بَلْ يَدَاهُ مَبْسُوطَتَانِ

**"Bali Mikono Yake imefumbuliwa." (05:64)**

Allaah anasifika kuwa na mikono kama ambavyo vilevile Ana uso mtukufu (Jalla wa ´Alaa).

## *Dalili ya Allaah kuwa na Macho*

Kadhalika anasifika kuwa na macho. Amesema (Ta´ala):

وَلِتُصْنَعَ عَلَىٰ عَيْنِي

**"Na ili ulelewe Machoni Mwangu."(20:39)**

تَجْرِي بِأَعْيُنِنَا

**"Inatembea kwa Macho Yetu." (54:14)**

Anasifika kuwa na macho na usikizi kwa njia inayolingana na Yeye (Subhaanah). Sifa zote hizi ni wajibu kumthibitishia nazo Allaah kwa njia inayolingana Naye.

Vivyo hivyo inahusiana na kufanya njama. Ni jambo limefungamanishwa na mkabala:

### *Dalili ya Adhabu na njama za Allaah*

وَمَكَرُوا وَمَكَرَ اللَّهُ

**"Na wakapanga njama, lakini Allaah Akapanga [kuwalipiza] njama." (03:54)**

إِنَّهُمْ يَكِيدُونَ كَيْدًاوَأَكِيدُ كَيْدًا

**"Hakika wao wanapanga njama Nami napanga mipango [ya kuvunja na kupindua njama zao]." (86:15-16)**

Ni njama zinazolingana na Allaah. Hafanani na viumbe Wake katika kupanga Kwake njama Zake.

Vivyo hivyo inahusiana na usikizi. Amesema (Ta´ala):

### *Dalili ya Kusikia na Kuona kwa Allaah*

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا

**"Allaah Amekwishasikia kauli ya yule [mwanamke] anayejadiliana nawe kuhusu mumewe na anamshitakia Allaah; na Allaah Anayasikia majibizano yenu." (58:01)**

إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

**"Hakika Allaah ni Mwenye kusikia yote, Mjuzi." (02:181)**

إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ

**"Hakika Allaah ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (58:01)**

Kuna Aayah nyenginezo nyingi zenye kuthibitisha usikizi, ujuzi na uoni.

Vilevile kuna Aayah nyingi zenye kuthibitisha kupenda. Zote hizo ni haki na ni wajibu kumthibitishia nazo Allaah kwa njia yenye kulingana Naye.

هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

**"Je, unamjua [mwengine] mwenye Jina kama Lake?" (19:65)**

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye." (112:04)**

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

**"Basi msipigie mifano Allaah! Hakika Allaah Anajua nanyi hamjui."(16:74)**

Zote hizi ni [sifa za] haki na ni wajibu kumthibitishia nazo Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) kwa njia inayolingana na Allaah pasi na upotoshaji, ukanushaji na kuzipindisha maana. Ana usikizi na sio kama usikizi wetu, ana uoni na sio kama uoni wetu, macho sio kama macho yetu, mkono sio kama mkono wetu, nguvu na sio kama nguvu zetu. Hali kadhalika inahusiana na sifa zingine zote. Anasema (Subhaanah):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)**

Sifa zake ni haki na ni zenye kulingana na Yeye. Sifa Zake hazifananishwi na viumbe Vyake (Jalla wa ´Alaa). Ni wajibu kumthibitishia nazo Allaah kwa njia yenye kulingana Naye bila ya kupotosha, kukanusha, kuzifanyia namna wala kuzifananisha. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaona kuwa mlango ni mmoja. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wale wenye kuwafuata kwa wema mpaka siku ya Qiyaamah.

## 23. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan V

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Amesema (Ta´ala):*

فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

*"Basi msimfanyie Allaah waliolingana naye [washirika] na hali ya kuwa nyinyi mnajua [kuwa hana]."* ***(02:22)***

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ اللَّهِ أَندَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ

*"Na miongoni mwa watu wako waaowafanya badala ya Allaah kuwa ni mungu mshirika; wanawapenda kama mapenzi [yapasavyo] ya kumpenda Allaah."* ***(02:165)***

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ وَلَمْ يَكُن لَّهُ وَلِيٌّ مِّنَ الذُّلِّ ۖ وَكَبِّرْهُ تَكْبِيرًا

*"Na sema: "Sifa njema zote ni za Allaah Ambaye Hakujifanyia mwana, na wala Hakuwa na mshirika katika ufalme, na wala hakuwa dhaifu hata awe [ahitaji] msaidizi; basi mtukuze matukuzo makubwa kabisa."* ***(17:111)***

يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۖ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

*Vinamtakasa Allaah [vyote] vilivyomo mbinguni na [vyote] vilivyomo ardhini - ufalme ni Wake na Sifa njema ni Zake - Naye juu ya kila kitu ni Muweza."* ***(64:01)***

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَىٰ عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًاالَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَّرَهُ تَقْدِيرًا

*"Ametukuka kwa Baraka Yule Ambaye Ameteremsha Pambanuzi kwa mja Wake ili awe muonyaji kwa walimwengu. Ambaye ni Wake Pekee ufalme wa mbingu na ardhi, na hakujichukulia mtoto na wala hakuwa na mshirika katika ufalme, na Ameumba kila kitu;*

*kisha Akakikadiria kipimo sawa sawa.”* ***(25:01-02)***

مَا اتَّخَذَ اللَّهُ مِن وَلَدٍ وَمَا كَانَ مَعَهُ مِنْ إِلَٰهٍ ۚ إِذًا لَّذَهَبَ كُلُّ إِلَٰهٍ بِمَا خَلَقَ وَلَعَلَا بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۚ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يَصِفُونَ عَالِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَتَعَالَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ

*”Allaah Hakuchukua mtoto yeyote na wala hakukuwa pamoja Naye mungu mwengine - hapo bila shaka kila mungu angelichukua vile alivyoviumba, na bila shaka baadhi yao wangeliwashinda wengineo. Ametakasika Allaah kutokana na yale yote wanayoyaelezea. Ni Mjuzi wa ghayb na ya dhahiri. Basi Ametukuka kutokana na yale wanayomshirikisha.”* ***(23:91-92)***

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

*”Basi msipigie mifano Allaah - Hakika Allaah Anajua nanyi hamjui.”* ***(16:74)***

قُلْ إِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّيَ الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ وَالْإِثْمَ وَالْبَغْيَ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَأَن تُشْرِكُوا بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهِ سُلْطَانًا وَأَن تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ

*”Sema: “Hakika Mola wangu Ameharamisha machafu yaliyodhihirika na yaliyo ya siri, na dhambi, ukandamizaji bila ya haki, na kumshirikisha Allaah kwa chochote kile ambayo Hakukiteremshia dalili, na kusema juu ya Allaah yale ambayo hamyajui”.”* ***(07:33)***

الرَّحْمَٰنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَىٰ

*”Mwingi wa Rahmah amelingana juu ya ´Arshi."* ***(20:05)***

ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ

*“Kisha Akalingana juu ya ‘Arshi.”* ***(07:54)***

*Aayah zimekuja kwa sampuli hii mahali saba: al-A´raaf:54, Yuunus:03, ar-Ra´d:02, al-Furqaan:59, as-Sajdah:04 na al-Hadiyd:04.*

## MAELEZO

Aayah zote hizi ni zenye kubainisha baadhi ya sifa za Allaah (´Azza wa Jall) kama zile zilizotangulia. Mfumo wa Ahl-us-Sunnah kwazo inatakiwa kuziamini na kuzithibitisha kama zilivyokuja kwa njia inayolingana na Allaah. Inatakiwa kufanya hivyo pasi na upotoshaji, ukanushaji, kuzifanyia namna wala kuzifananisha.

Hali kadhalika inahusiana na zile sifa za Allaah zilizokuja katika Sunnah Swahiyh. Zote ni kwa mfumo huu: ni wajibu kumthibitishia nazo Allaah kwa njia inayolingana na Allaah pasi na upotoshaji, ukanushaji, kuzifanyia namna wala kuzifananisha. Miongoni mwazo ni maneno Yake (Jalla wa ´Alaa):

## *Dalili ya Allaah kutokuwa na wenza na washirika*

فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

**"Basi msimfanyie Allaah waliolingana naye [washirika] na hali ya kuwa nyinyi mnajua [kuwa hana]." (02:22)**

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ اللَّهِ أَندَادًا

**″Na miongoni mwa watu wako waaowafanya badala ya Allaah kuwa ni mungu mshirika." (02:165)**

Bi maana wenza na washirika. Allaah hana wenza wala washirika. Amesema:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ اللَّهِ أَندَادًا

**″Na miongoni mwa watu wako waaowafanya badala ya Allaah kuwa ni mungu mshirika."**

kwa njia ya makemeo. Kwa msemo mwingine kuna watu wenye kumfanyia Allaah washirika. Nao si wengine ni washirikina. Ndipo akakataza hili pale aliposema:

فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

**"Basi msimfanyie Allaah waliolingana naye [washirika] na hali ya kuwa nyinyi mnajua [kuwa hana]." (02:22)**

Bi maana msiwaabudu walioko ndani ya makaburi, Mitume, Malaika, majini na mawe. Vyote hivyo kuviabudu ni batili. Amesema (Ta´ala):

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِ هُوَ الْبَاطِلُ

**"Hivyo ni kwa kuwa Allaah Ndiye wa Kweli na wale wanaowaomba badala Yake ndiyo batili." (22:62)**

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِ الْبَاطِلُ

**"Hivyo ni kwa kuwa Allaah Ndiye wa Kweli na wale wanaowaomba badala Yake ni batili." (31:30)**

Ni wajibu kwa kila kiumbe ambaye ´ibaadah ni yenye kumuwajibikia kumuabudu Yeye Mmoja wa Pekee na wawakanushe wenza. Wanatakiwa kutambua kwa yakini ya kwamba hana mwenza, mwenye kulinhgana Naye na mshirika na wakati huo huo waamini hilo. Amesema (Ta´ala):

لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Hakuzaa na wala Hakuzaliwa. Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye."(112:03-04)**

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

**"Basi msipigie mifano Allaah! Hakika Allaah Anajua nanyi hamjui."(16:74)**

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)**

Amesema (Ta´ala):

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ وَلَمْ يَكُن لَّهُ وَلِيٌّ مِّنَ الذُّلِّ ۖ وَكَبِّرْهُ تَكْبِيرًا

**"Na sema: "Sifa njema zote ni za Allaah Ambaye Hakujifanyia mwana, na wala**

**Hakuwa na mshirika katika ufalme, na wala hakuwa dhaifu hata awe [ahitaji] msaidizi; basi mtukuze matukuzo makubwa kabisa."(17:111)**

Allaah hana mshirika katika ufalme. Allaah ana mawalii. Lakini hata hivyo sio wasaidizi katika ufalme Wake. Yeye ni Mwenye kujitosheleza na kila asiyekuwa Yeye. Yeye ndiye Mwenye nguvu, Aliye juu na Mshindi. Hana washirika katika ufalme. Pamoja na hivyo ana mawalii Anaowapenda na wao wanampenda. Yule mwenye kumtii na kumcha ndio walii Wake kwa njia ya kwamba Allaah anakuwa ni mwenye kuwapenda na kuwakaribia, kwa sababu wamemtii na kuadhimisha maamrisho Yake. Amesema (Ta´ala):

أَلَا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ

**"Tanabahi! Hakika mawalii wa Allaah hawana khofu juu yao na wala hawatohuzunika. Ambao wameamini na wakawa wana taqwa." (10:62:63)**

Hawa ndio mawalii wa Allaah. Lakini hata hivyo sio wasaidizi katika ufalme. Ni mawalii kwa njia ya mapenzi, kwa sababu wamemtii na kufuata Shari´ah ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Vilevile inahusiana na Aayah nyenginezo zenye kutaja ufalme, sifa kamilifu na uwezo. Hakika Yeye ndiye Mfalme juu ya kila kitu, Muumbaji wa kila kitu, Muweza juu ya kila kitu na ni Mjuzi wa hali zote za waja. Yote haya ni haki. Miongozi mwazo ni pamoja na:

## *Dalili ya Allaah kutokuwa na mtoto*

وَلَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا

**"... na hakujichukulia mtoto." (25:02)**

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye." (112:04)**

Sifa zote hizi ni zimethibiti Kwake (Jalla wa ´Alaa). Yeye ndiye Muumbaji wa kila kitu:

## *Dalili ya Kuumba na Uwezo wa Allaah*

وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَّرَهُ تَقْدِيرًا

**"... na Ameumba kila kitu; kisha Akakikadiria kipimo sawa sawa." (25:02)**

لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**"... ufalme ni Wake na Sifa njema ni Zake. Naye juu ya kila kitu ni Muweza."(64:01)**

## 24. Kuuliza namna ya Sifa za Allaah ni Bid´ah iliyozusha Ahl-ul-Bid´ah

Vilevile Allaah anasifika kulingana juu ya ´Arshi. Hili limetajwa sehemu saba katika Qur-aan; Twaaha, al-A´raaf, Yuunus, ar-Ra´d, al-Israa´, Luqmaan, as-Sajdah na al-Hadiyd. Zote zimethibiti.

Kulingana (al-Istiwaa´) maana yake ni kuwa juu na kungatika. Kulingana juu ya ´Arshi maana yake ni kwamba yuko juu na amengatika kwenye ´Arshi. Yeye Ndiye ambaye yuko juu ya viumbe Wake wote. ´Arshi ndio sakafu ya viumbe. Yeye Allaah (Subhaanah) yuko juu ya ´Arshi. Ni kulingana ambako kunalingana na utukufu Wake. Hakuna anayejua namna yake isipokuwa Yeye Pekee (Subhaanahu wa Ta´ala). Wakati Imaam Maalik bin Anas (Rahimahu Allaah), ambaye alikuwa ni mwanachuoni mkubwa wa al-Madiynah katika wakati wake na mmoja katika maimamu wane, alipoulizwa: "Ee Abu ´Abdillaah!

الرَّحْمَٰنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَىٰ

**"Mwingi wa Rahmah amelingana juu ya ´Arshi."** **(20:05)**

Amelingana namna gani?" Ghafla uso wake ukageuka kwa mshangao mkubwa aliopata juu ya swali hili. Kisha baada ya hapo akasema:

"Kulingana kunajulikana… "

Bi maana kulingana kunajulikana kwamba ni kuwa juu na kungatika.

"… namna haijulikani. Kuamini hilo ni wajibu na kuulizia hilo ni Bid´ah. Mimi naona kuwa wewe ni mtu muovu" kisha baada ya hapo akaamrisha atolewe."[12]

Vivyo hivyo ndivyo alivyosema Sufyaan ath-Thawriy, al-Awzaa´iy, Imaam Ahmad, Imaam ash-Shaafi´iy, Ishaaq bin Raahuuyah na maimamu wengine wa Uislamu. Mlango ni ule ule mmoja: maana ya kulingana inajulikana. Maana yake

[12] ad-Daarimiy katika "ar-Radd ´alaa al-Jahmiyyah", uk.33, al-Lalakaa´iy katika "Sharh Usuul I´tiqaad Ahl-is-Sunnah wal-Jamaa´ah" (02/398), al-Bayhaqiy katika "Asmaa´ was-Swifaat" (867), Ibn ´Abdi-Barr katika "at-Tamhiyd" (07/151). Haafidhw Ibn Hajar amesema katika "Fath-ul-Baariy" (13/407) ya kwamba mlolongo wa wapokezi wake ni nzuri (Jayyid).

ni kuwa juu na kungatika. Namna haijulikani. Kwa msemo mwingine hakuna anayejua namna alivyolingana isipokuwa Yeye Pekee (Subhaanahu wa Ta´ala). Kuamini hilo ni wajibu, kwa sababu Allaah ndiye amejielezea Mwenyewe. Kuulizia namna ni Bid´ah iliyozuliwa na wanafalsafa miongoni mwa Jahmiyyah, Mu´tazilah na wengineo.

Hali kadhalika inatakiwa kusema juu ya sifa zingine ya kwamba huruma, radhi, ghadhabu, uwezo, mkono na mguu vyote vinajulikana. Kuhusu namna yake haijulikani. Hatujui namna ya huruma Wake ulivyo, ghadhabu Zake, mkono Wake, mguu Wake na macho Yake vyote hatujui namna vilivyo na wala hatuviingilii kwa ndani. Bali tunavithibitisha na kuvipitisha kama vilivyokuja. Tunasema kuwa Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona, tunasema kuwa ni Mwenye mikono miwil kama alivyosema (Ta´ala):

بَلْ يَدَاهُ مَبْسُوطَتَانِ

**"Bali Mikono Yake imekunjuliwa." (05:64)**

مَا مَنَعَكَ أَن تَسْجُدَ لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ

**"Nini kilichokuzuia usimsujudie Niliyemuumba kwa Mikono Yangu?" (38:75)**

Vilevile imekuja katika Hadiyth Swahiyh inayosema:

"Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) aliyetukuka Aweke Mguu Wake kisha pawe sawa. Hapo ndio itasema “Inatosha! Inatosha!”[13]

Vilevile Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) ameeleza kuwa anamghadhibikia yule mwenye kumuasi na humridhia yule mwenye kumtii na anawarehemu waja Wake. Zote hizi ni katika sifa Zake (Jalla wa ´Alaa):

“Allaah Anawacheka watu wawili ambapo mmoja wao kamuua mwenzake. Halafu wote wawili wanaingia Peponi.”[14]

[13] al-Bukhaariy (4849) na Muslim (2846).

Kughadhibika Kwake, kuridhia Kwake, kusikia Kwake, kuona Kwake na sifa zake zingine zote zinalingana na Yeye peke yake na wala hashabihiani na viumbe Vyake kwa chochote katika hayo kutokana na kanuni isemayo:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)**

Ahls-Sunnah wal-Jamaa´ah wanathibitisha Aayah na Hadiyth zinazozungumzia sifa, uthibitishaji ambao hamna ndani yake ufananishaji na wakati huo huo wanamtakasa Allaah (Jalla wa ´Alaa) kufanana na viumbe Wake utakaso usiokuwa ndani yake na ukanushaji. Inahusiana na ukanushaji ulioambatana na uthibitishaji.

[14] al-Bukhaariy (2826) na Muslim (1890).

## 25. Mu´attwilah na Mumaththilah ni makafiri

Ahl-ul-Bid´ah wanafanya tofauti na mfumo huu. Wamegawanyika mafungu yafuatayo:

1- Kuna pote lililothibitisha [kwa kupitiliza].

2- Pote lingine likakanusha.

Ahl-us-Sunnah ni wenye kujitenga na mapote yote mawili. Mumaththilah ni makafiri. Mu´attwilah pia ni makafiri. Ama kuhusu Ahl-us-Sunnah wao ndio ambao wamethibitisha pasi na kufananisha, bi maana wamethibitisha sifa na majina Yake kwa njia inayolingana na Allaah. Ni uthibitishaji usiokuwa na ufananishaji. Sambamba na hilo wakamtakasa kushabihiana na viumbe Vyake, utakaso usiokuwa ndani yake na ukanushaji. Tofauti na wanavyofanya Mumaththilah na tofauti vilevile na Mu´attwilah katika Jahmiyyah, Mu´tazilah na vijukuu vyao.

Inatakikana, bali ni wajibu kwa muumini kufuata mfumo huu wa Ahl-us-Sunnah ambao ni Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wenye kuwafuata kwa wema. Ukiulizwa ni kina nani Ahl-us-Sunnah? Jibu sema kuwa ni Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na waliowafuata kwa wema ikiwa ni pamoja na Taabi´uun, waliokuja baada ya Taabi´uun, maimamu wanne na Ahl-us-Sunnah wengineo. Hawa ndio Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Mwenye kwenda kinyume nao si katika wao. Mwenye kuthibitisha [kwa kupitiliza], akafananisha au akakanusha [sifa za Allaah] basi ni katika Ahl-ul-Bid´ah. Ahl-us-Sunnah hawana lolote kuhusiana na yeye.

Uk. 44

## 26. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan VI

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Amesema (Ta´ala):*

يَا عِيسَىٰ إِنِّي مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَيَّ

*"Ee ´Iysaa! Hakika Mimi ni Mwenye kukuchukua na Mwenye kukupandisha Kwangu."* ***(03:55)***

بَل رَّفَعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ

*"Bali Allaah Alimnyanyua Kwake."* ***(04:158)***

إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ

*"Kwake Yeye linapanda neno zuri na kitendo chema hukinyanyua."* ***(35:10)***

يَا هَامَانُ ابْنِ لِي صَرْحًا لَّعَلِّي أَبْلُغُ الْأَسْبَابَأَسْبَابَ السَّمَاوَاتِ فَأَطَّلِعَ إِلَىٰ إِلَٰهِ مُوسَىٰ وَإِنِّي لَأَظُنُّهُ كَاذِبًا

*"Ee Haamaan! Nijengee mnara mkubwa ili nifikie njia. Njia za mbinguni ili nimchungulie Mungu wa Muwsaa, kwani hakika mimi namdhania ni muongo."* ***(40:36-37)***

أَأَمِنتُم مَّن فِي السَّمَاءِ أَن يَخْسِفَ بِكُمُ الْأَرْضَ فَإِذَا هِيَ تَمُورُ أَمْ أَمِنتُم مَّن فِي السَّمَاءِ أَن يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ۖ فَسَتَعْلَمُونَ كَيْفَ نَذِيرِ

*"Je, mnadhani mko [katika] amani na Aliyeko mbinguni [juu] kwamba Hatokudidimizeni ardhini, tahamaki hiyo inatikisika? Au mnadhani mko [katika] amani na Aliyeko mbinguni [juu] kwamba Hatokutumieni kimbunga [cha mawe], basi mtajua vipi [makali] maonyo Yangu."* ***(67:16-18)***

هُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۚ يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنزِلُ مِنَ السَّمَاءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا ۖ وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنتُمْ ۚ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

*"Yeye Ndiye Aliyeumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha akalingana juu ya*

*´Arshi. Anajua yanayoingia ardhini, na yatokayo humo, na yanayoteremka kutoka mbinguni, na yanayopanda humo - Naye Yu Pamoja nanyi popote mlipo. Na Allaah kwa myatendayo ni Mwenye kuyaona."* ***(57:04)***

مَا يَكُونُ مِن نَّجْوَىٰ ثَلَاثَةٍ إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ وَلَا أَدْنَىٰ مِن ذَٰلِكَ وَلَا أَكْثَرَ إِلَّا هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا ۖ ثُمَّ يُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

*"Hauwi mnong'ono wa [watu] watatu isipokuwa Yeye ni wa nne wao, na wala watano isipokuwa Yeye ni wa sita wao, na wala [hauwi mnong'ono wa] chini kuliko ya hivyo, na wala wa wengi zaidi isipokuwa Yeye Yu pamoja nao popote watakapokuwa; kisha Atawajulisha kwa yale [yote] waliyoyatenda Siku ya Qiyaamah - hakika Allaah kwa kila kitu ni Mjuzi daima."* ***(58:07)***

لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا

*"Usihuzunike, hakika Allaah Yu Pamoja nasi."* ***(09:40)***

إِنَّنِي مَعَكُمَا أَسْمَعُ وَأَرَىٰ

*"Hakika Mimi Niko pamoja nanyi, Nasikia na Naona."* ***(20:46)***

إِنَّ اللَّهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوا وَّالَّذِينَ هُم مُّحْسِنُونَ

*"Hakika Allaah Yu Pamoja na wenye taqwa na wale ambao wao ni wema."*
***(16:128)***

وَاصْبِرُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ

*"Subirini. Hakika Allaah Yu Pamoja na wanaosubiri."* ***(08:46)***

كَم مِّن فِئَةٍ قَلِيلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيرَةً بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ

*"Makundi mangapi machache yameshinda makundi mengi kwa idhini ya Allaah? Na Allaah Yu pamoja na wenye kusubiri."* ***(02:249)***

## MAELEZO

Aayah hizi zilizotajwa na mwandishi (Rahimahu Allaah):

1- Kuna zinazozungumzia kuhusu Ujuu.

2- Zingine zinahusiana upamoja.

Allaah (Jalla wa ´Alaa) amejithibitishia Mwenyewe Ujuu na kwamba yuko juu ya ´Arshi, yuko juu ya mbingu (Jalla wa ´Alaa) na kwamba anaombwa kutokea kwa juu. Ahl-us-Sunnah wameafikiana juu ya hilo. Ahl-us-Sunnah wameafikiana ya kwamba Allaah (Subhaanah) yuko juu na kwamba yuko juu ya ´Arshi na kwamba amelingana kulingana ambako kunalingana na Utukufu na Ukubwa Wake. Amesema (Subhaanah):

## *Dalili ya kwamba Allaah amelingana juu ya ´Arshi Yake*

الرَّحْمَٰنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَىٰ

**"Mwingi wa Rahmah amelingana juu ya ´Arshi." (20:05)**

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ

**"Hakika Mola wenu ni Allaah Ambaye Ameumba mbingu na ardhi katika siku sita kisha akalingana juu ya ´Arshi." (07:54)**

Kuna Aayah saba ambazo zote (Subhaanah) amethibitisha Ujuu na kwamba amelingana juu ya ´Arshi (Jalla wa ´Alaa). Ni kulingana ambako kunalingana na Utukufu Wake. Hafanani na viumbe Vyake katika kitu chochote katika sifa Zake. Ni dalili yenye kuonyesha Ujuu. Kwa ajili hii ndio maana (Jalla wa ´Alaa) amesema:

## *Dalili ya kwamba Allaah yuko juu ya viumbe Vyake kwa dhati Yake*

يَا عِيسَىٰ إِنِّي مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَيَّ

**“Ee ‘Iysaa! Hakika Mimi ni Mwenye kukuchukua na Mwenye kukupandisha Kwangu.”(03:55)**

بَل رَّفَعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ

**"Bali Allaah Alimnyanyua Kwake."(04:158)**

Bi maana ´Iysaa (´alayhis-Salaam).

إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ

**"Kwake Yeye linapanda neno zuri na kitendo chema hukinyanyua." (35:10)**

Neno "kupanda" na "kunyanyuliwa" ni dalili yenye kufahamisha Ujuu. Matendo hupandishwa na neno zuri hunyanyuliwa Kwake.

Vilevile Malaika hupanda Kwake. Amesema (Jalla wa ´Alaa):

تَعْرُجُ الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ إِلَيْهِ فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ

**"Malaika na Roho [Jibrily] wanapanda Kwake katika siku kiasi chake ni miaka khamsini elfu." (70:04)**

Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipandishwa Kwake mpaka akapita tabaka ya saba na akasikia maneno ya Mola (Jalla wa ´Alaa). Yote haya ni haki kwa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Ni wajibu kumthibitishia Allaah. Amesema (Subhaanah):

أَأَمِنتُم مَّن فِي السَّمَاءِ أَن يَخْسِفَ بِكُمُ الْأَرْضَ فَإِذَا هِيَ تَمُورُ أَمْ أَمِنتُم مَّن فِي السَّمَاءِ أَن يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ۖ فَسَتَعْلَمُونَ كَيْفَ نَذِيرِ

**"Je, mnadhani mko [katika] amani na Aliyeko mbinguni [juu] kwamba Hatokudidimizeni ardhini, tahamaki hiyo inatikisika? Au mnadhani mko [katika] amani na Aliyeko mbinguni [juu] kwamba Hatokutumieni kimbunga [cha mawe], basi mtajua vipi [makali] maonyo Yangu."(67:16-18)**

Maana ya "mbinguni" (fis-Samaa´), bi maana juu. Naye ni Allaah (Jalla wa ´Alaa). Imesemekana vilevile ya kwamba "as-Samaa´", maana yake ni zile mbingu. Kadhalika maana ya "fiy" yaani juu. Kwa hivyo maana yake inafika inakuwa juu ya mbingu. Ikisemwa kuwa "mbingu" maana yake ni juu maana yake inakuwa wazi. Hivyo inakuwa ya kwamba (Jalla wa ´Alaa) yuko juu. Vilevile ikisemwa "mbingu" maana yake ni zile mbingu zilizojengwa maana yake inakuwa ´yuko juu ya mbingu`. Kwa sababu "fiy" wakati mwingine inakuja ikiwa na maana ya "juu". Amesema (Ta´ala) kuhusu Fir´awn:

وَلَأُصَلِّبَنَّكُمْ فِي جُذُوعِ النَّخْلِ

**"Nitakusulubuni (fiy) katika mashina ya mitende." (20:71)**

Bi maana juu ya mashina ya mitende.

Vilevile amesema (Subhaanahu wa Ta´ala):

فَسِيحُوا فِي الْأَرْضِ

**"Basi tembeeni (fiy) katika ardhi." (09:02)**

Bi maana juu ya ardhi.

Kwa hivyo kusema kuwa Allaah yuko mbinguni maana yake ni kwamba yuko juu yake na Yeye (Jalla wa ´Alaa) yuko juu ya kila kitu. Haya ndio maoni ya Ahl-us-Sunnah wanasema kuwa yuko juu na kwamba yuko juu ya ´Arshi. Hili ni tofauti na watu wa Bid´ah miongoni mwa Khawaarij, Mu´tazilah, Jahmiyyah na wengineo. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amejithibitishia Mwenyewe kuwa juu na kwamba yuko juu ya ´Arshi.

Ahl-ul-Bid´ah ndio wenye kusema kuwa Allaah yuko kila mahali. Huu ni ujinga, batili na kufuru. Wanayoamini Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah katika Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wenye kuwafuata kwa wema ni kwamba Yeye (Subhaanah) ni Mwenye kusifika kuwa juu ya ´Arshi na kwamba amelingana juu yake, kwa msemo mwingine amengatika juu yake kungatika ambako kunalingana na Utukufu Wake. Hafanani na viumbe Vyake katika kitu katika sifa Zake.

Wakati Imaam Maalik bin Anas (Rahimahu Allaah), ambaye alikuwa ndiye mwanachuoni mkubwa wa al-Madiynah katika wakati wake, alipoulizwa juu ya hili akajibu kwa kusema:

"Kulingana kunajulikana. Namna haijulikani. Kuamini hilo ni wajibu. Kuuliza kuhusu hilo ni Bid´ah."

Vivyo hivyo imepokelewa kutoka kwa mwalimu wake Rabiy´ah bin Abiy ´Abdir-Rahmaan, Umm Salamah, al-Awzaa´iy, ath-Thawriy, Ishaaq bin Raahuuyah, Imaam Ahmad bin Hanbal na maimamu wengine wa Salaf.

## 27. Sifa za Allaah haziuliziwi namna, zinauliziwa maana

Kulingana kunajulikana na kwamba maana yake ni kuwa juu na kungatika. Namna haijulikani na hakuna anayejua namna zilivyo sifa Zake isipokuwa Yeye Mwenyewe (Subhaanahu wa Ta´ala). Amelingana juu ya ´Arshi bila ya namna. Hushuka kwenye mbingu ya dunia bila ya namna. Huridhia na hughadhibika bila ya namna. Huchukia bila ya namna. Atakuja siku ya Qiyaamah bila ya namna. Hivi ndivyo wanavyoamini Ahl-us-Sunnah. Hakuna anayejua namna zilivyo sifa Zake isipokuwa Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala). Ni sifa za haki na zilizothibiti. Ni wajibu kumthibitishia nazo Allaah kwa njia inayolingana Naye. Hafananishwi na viumbe Vyake kwenye kitu katika sifa Zake (Jalla wa ´Alaa). Amesema (Subhaanah):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)**

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

**"Basi msipigie mifano Allaah! Hakika Allaah Anajua nanyi hamjui."(16:74)**

Ni kama kusema kwamba anafanana na kitu kadhaa.

هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

**"Je, unamjua [mwengine] mwenye Jina kama Lake?" (19:65)**

Bi maana hakuna anayelingana Naye wala kushabihiana Naye na wala hana mwenza (Subhaanahu waTa´ala). Haya ndio maoni ya watu wa haki ambapo wanaamini kuwa yuko juu, yuko juu ya ´Arshi, amelingana juu yake kulingana ambako kunalingana na utukufu Wake na ukubwa Wake. Yeye hafananishwi na viumbe Vyake katika kulingana kwao, kushuka kwao, kucheka kwao, kukasirika kwao na sifa nyenginezo.

## 28. Upamoja wa Allaah aina mbili

Aayah za sehemu ya mwisho zote zinazungumzia upamoja ambao ni wa kimaalum (al-Ma´iyyah al-Khaasswah) na upamoja ulioenea (al-Ma´iyyah al-´Aammah). Amesema (Ta´ala):

### *a) Allaah yuko pamoja na waja Wake wote kwa ujuzi Wake*

هُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۚ يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنزِلُ مِنَ السَّمَاءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا ۖ وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنتُمْ ۚ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

**”Yeye Ndiye Aliyeumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha akalingana juu ya ´Arshi. Anajua yanayoingia ardhini, na yatokayo humo, na yanayoteremka kutoka mbinguni, na yanayopanda humo, Naye Yu Pamoja nanyi popote mlipo. Na Allaah kwa myatendayo ni Mwenye kuyaona.” (57:04)**

Allaah (Jalla wa ´Alaa) anakijua kila kitu kilicho mbinguni na ardhini, kilichopita na kitakachokuja. Yote hayo anayajua. Pamoja na hivyo Yeye anakuwa pamoja na waja Wake popote wanapokuwa. Bi maana anakuwa pamoja nao kwa ujuzi Wake na wakati huo huo yuko juu ya ´Arshi. Anakuwa pamoja nao kwa elimu Yake yenye kuwazunguka isiyofichikana na kitu. Amesema (Ta´ala):

لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

**"... ili mjue kwamba Allaah juu ya kila kitu ni Muweza na kwamba Allaah Amekwishakizunguka kila kitu kwa ujuzi Wake." (65:12)**

إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

**"Hakika Allaah kwa kila kitu ni Mjuzi." (08:75)**

مَا يَكُونُ مِن نَّجْوَىٰ ثَلَاثَةٍ إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ وَلَا أَدْنَىٰ مِن ذَٰلِكَ وَلَا أَكْثَرَ إِلَّا هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا ۖ ثُمَّ يُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

**"Hauwi mnong'ono wa [watu] watatu isipokuwa Yeye ni wa nne wao, na wala watano isipokuwa Yeye ni wa sita wao, na wala [hauwi mnong'ono wa] chini kuliko ya hivyo, na wala wa wengi zaidi isipokuwa Yeye Yu pamoja nao popote watakapokuwa; kisha Atawajulisha kwa yale [yote] waliyoyatenda Siku ya Qiyaamah - hakika Allaah kwa kila kitu ni Mjuzi."(58:07)**

Amemalizia Aayah hii kwa ujuzi kwa lengo ili msomaji na msikilizaji ajue kuwa kinachokusudiwa ni elimu na wakati huo huo yuko juu ya ´Arshi (Jalla wa ´Alaa) na kwamba hafichikani na kitu (Jalla wa ´Alaa).

### *b) Allaah yuko pamoja na waja Wake wema kiujuzi, kwa kuwanusuru na kwa kuwapa nguvu*

Hali kadhalika inahusiana na upamoja wa kimaalum:

لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا

**"Usihuzunike, hakika Allaah Yu Pamoja nasi."(09:40)**

Haya yalisemwa na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kumwambia Abu Bakr as-Swiddiyq (Radhiya Allaahu ´anh) wakati walipokuwa pangoni.

إِنَّنِي مَعَكُمَا أَسْمَعُ وَأَرَىٰ

**"Hakika Mimi Niko pamoja nanyi, Nasikia na Naona."(20:46)**

Wanaambiwa Muusa na Haaruun (´alayhimaas-Salaam).

وَاصْبِرُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ

**"Subirini. Hakika Allaah Yu Pamoja na wanaosubiri."(08:46)**

كَم مِّن فِئَةٍ قَلِيلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيرَةً بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ

**"Makundi mangapi machache yameshinda makundi mengi kwa idhini ya Allaah? Na Allaah Yu pamoja na wenye kusubiri."(02:249)**

Aayah zote hizi ni zenye kufahamisha upamoja ambao ni maalum ambapo anakuwa pamoja na mawalii Wake, wenye kumtii na Mitume Wake kwa kuwazunguka kielimu, kinusura na kuwapa nguvu.

Ama kuhusu upamoja wa kijumla unahusiana na kukizunguka kila kitu kielimu na kwamba hafichikani na chenye kufichikana na kwamba Yeye ndiye mwenye kuwaendesha na kuwapeleka.

Upamoja wa kimaalum unakuwa na Ujuzi pamoja vilevile na kuwanusuru mawalii Wake na kuwahami. Kama Alivyosema kupitia ndimi ya Mtume Wake alipomwambia Swahabah wake pindi walipokuwa pangoni:

لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا

**"Usihuzunike, hakika Allaah Yu Pamoja nasi."(09:40)**

Akamwambia Muusa na Haaruun (´alayhimaas-Salaam) walipokuwa mbele ya Fir´awn. Allaah aliwahami kutokana na shari yake:

إِنَّنِي مَعَكُمَا أَسْمَعُ وَأَرَىٰ

**"Hakika Mimi Niko pamoja nanyi, Nasikia na Naona."(20:46)**

Hali kadhalika viumbe wote Yuko pamoja nao kwa ujuzi Wake inayokijua kila kitu. Anazijua siri zao na yale wanayonong´onezana na wakati huo huo yuko juu ya ´Arshi. Elimu Yake imekizunguka kila kitu. Anajua na kuona mdudu mchungu mweusi katika usiku wenye giza kingi. Anajua jinsi yanavyoenda maji ya mito na bahari na vilivyo ndani yavyo. Anajua vyote vilivyomo chini ya ardhi na vinavyohadithiwa na mioyo. Vyote hivyo hakuna kinachofichikana Kwake (Subhaanahu wa Ta´ala). Amesema (Jalla wa ´Alaa):

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُو مِنْهُ مِن قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ

**"Na hushughuliki katika jambo lolote na wala husomi humo chochote katika Qur-aan, na wala hamtendi ʻamali yoyote isipokuwa Tunakuwa Mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo." (10:61)**

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالصَّابِئِينَ وَالنَّصَارَىٰ وَالْمَجُوسَ وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا إِنَّ اللَّهَ يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ

**"Hakika wale walioamini, na ambao Mayahudi, na Wasabai [waabudiao nyota], na Manaswara, wa Majusi [waabudiao moto], na wale wanaoshirikisha; hakika Allaah Atahukumu baina yao Siku ya Qiyaamah. Hakika Allaah juu ya kila kitu ni Mwenye kushuhudia." (22:17)**

لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

**"... ili mjue kwamba Allaah juu ya kila kitu ni Muweza na kwamba Allaah Amekwishakizunguka kila kitu kwa ujuzi Wake." (65:12)**

إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

**"Hakika Allaah juu ya kila kitu ni Mjuzi." (08:75)**

وَمَا تَحْمِلُ مِنْ أُنثَىٰ وَلَا تَضَعُ إِلَّا بِعِلْمِهِ

**“Na mwanamke yeyote yule habebi [mimba] na wala hazai isipokuwa kwa ujuzi Wake.”(35:11)**

Elimu Yake imewazunguka viumbe. Ujuzi Wake maalum uko pamoja na mawalii Wake. Anazijua hali za viumbe Wake maalum na wengineo. Anayajua yatayokuja katika zama za mwisho. Anayajua yatayokuja siku ya Qiyaamah. Anayajua yaliyopita katika zama za kale. Yote hayo anayajua. Bali anayajua na ameyazunguka (Jalla wa ´Alaa).

Ni wajibu kumthibitishia nayo (Subhaanahu wa Ta´ala) na sambamba na hilo kumtakasa kushabihiana na viumbe Vyake kwenye kitu katika sifa Zake (Jalla wa ´Alaa). Haya ndio maoni ya watu wa haki ambao ni Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.

## 29. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan VII

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Amesema (Ta´ala):*

وَمَنْ أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ حَدِيثًا

*"Na nani mkweli zaidi katika maneno kuliko Allaah?"* ***(04:87)***

وَمَنْ أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ قِيلًا

*"Na nani aliye mkweli zaidi kwa kauli kuliko Allaah?"* ***(04:122)***

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ

*"Na Atakaposema Allaah: "Ee 'Iysaa mwana wa Maryam!"* ***(05:116)***

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا

*"Na limetimia Neno la Mola wako kwa kweli na uadilifu."* ***(06:115)***

وَكَلَّمَ اللَّهُ مُوسَىٰ تَكْلِيمًا

*"Na bila shaka Allaah Alimsemesha Muwsaa maneno moja kwa moja."* ***(04:164)***

مِّنْهُم مَّن كَلَّمَ اللَّهُ

*"Miongoni mwao [yuko] aliyesemeshwa na Allaah."* ***(02:253)***

وَلَمَّا جَاءَ مُوسَىٰ لِمِيقَاتِنَا وَكَلَّمَهُ رَبُّهُ

*"Na alipokuja Muwsaa katika pahala pa miadi yetu na Mola wake Akamsemesha."* ***(07:143)***

وَنَادَيْنَاهُ مِن جَانِبِ الطُّورِ الْأَيْمَنِ وَقَرَّبْنَاهُ نَجِيًّا

*"Na Tukamwita kutoka upande wa kulia wa mlima na Tukamkurubisha kuzungumza naye kwa siri."* ***(19:52)***

وَإِذْ نَادَىٰ رَبُّكَ مُوسَىٰ أَنِ ائْتِ الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

*"Na Mola wako Alipomwita Muwsaa [kumwambia]: "Nenda kwa watu madhalimu."* ***(26:10)***

وَنَادَاهُمَا رَبُّهُمَا أَلَمْ أَنْهَكُمَا عَن تِلْكُمَا الشَّجَرَةِ

*"Na Mola wao Akawaita [wote wawili na kuwaambia]: "Je, kwani Mimi Sikukukatazeni mti huo."****(07:22)***

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ مَاذَا أَجَبْتُمُ الْمُرْسَلِينَ

*"Na Siku Atakapowaita na kusema: "Mliwajibu nini Mitume?"* ***(28:65)***

وَإِنْ أَحَدٌ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ اسْتَجَارَكَ فَأَجِرْهُ حَتَّىٰ يَسْمَعَ كَلَامَ اللَّهِ

*"Na ikiwa mmoja wa washirikina akikuomba umlinde, basi mlinde mpaka asikie Maneno ya Allaah."* ***(09:06)***

وَقَدْ كَانَ فَرِيقٌ مِّنْهُمْ يَسْمَعُونَ كَلَامَ اللَّهِ ثُمَّ يُحَرِّفُونَهُ مِن بَعْدِ مَا عَقَلُوهُ وَهُمْ يَعْلَمُونَ

*"Na hali lilikuwa kundi miongoni mwao linasikia Maneno ya Allaah kisha wakayapotosha baada ya kuyaelewa na hali wanajua."* ***(02:75)***

يُرِيدُونَ أَن يُبَدِّلُوا كَلَامَ اللَّهِ ۚ قُل لَّن تَتَّبِعُونَا كَذَٰلِكُمْ قَالَ اللَّهُ مِن قَبْلُ

*"Wanataka kubadilisha Maneno ya Allaah. Sema [uwaambie]: "Hamtotufuata! Hivyo ndivyo Alivyosema Allaah kabla"."* ***(48:15)***

وَاتْلُ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِن كِتَابِ رَبِّكَ ۖ لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِهِ

*"Na soma uliyoletewa Wahy katika Kitabu cha Mola wako. Hakuna awezaye*

*kubadilisha Maneno Yake.”* ***(18:27)***

إِنَّ هَٰذَا الْقُرْآنَ يَقُصُّ عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَكْثَرَ الَّذِي هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ

*”Hakika hii Qur-aan inawasimulia wana wa Israaiyl mengi ambayo wao wanakhitilafiana nayo.”* ***(27:76)***

وَهَٰذَا كِتَابٌ أَنزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ

*”Na hiki Kitabu Tumekiteremsha kilichobarikiwa.”* ***(06:155)***

لَوْ أَنزَلْنَا هَٰذَا الْقُرْآنَ عَلَىٰ جَبَلٍ لَّرَأَيْتَهُ خَاشِعًا مُّتَصَدِّعًا مِّنْ خَشْيَةِ اللَّهِ

*”Lau Tungeliiteremsha hii Qur-aan juu ya mlima, basi ungeliuona unanyenyekea na wenye kupasukapasuka kutokana na kumuogopa Allaah.”* ***(59:21)***

وَإِذَا بَدَّلْنَا آيَةً مَّكَانَ آيَةٍ ۙ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يُنَزِّلُ قَالُوا إِنَّمَا أَنتَ مُفْتَرٍ ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ قُلْ نَزَّلَهُ رُوحُ الْقُدُسِ مِن رَّبِّكَ بِالْحَقِّ لِيُثَبِّتَ الَّذِينَ آمَنُوا وَهُدًى وَبُشْرَىٰ لِلْمُسْلِمِينَ وَلَقَدْ نَعْلَمُ أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُ بَشَرٌ ۗ لِّسَانُ الَّذِي يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَعْجَمِيٌّ وَهَٰذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُّبِينٌ

*”Na Tunapobadilisha Aayah mahala pa Aayah nyingine, na Allaah Anajua Anayoyateremsha, [makafiri] husema: “Hakika wewe ni mzushi.” - bali wengi wao hawajui. Sema: Roho Takatifu [Jibriyl] ameiteremsha kutoka kwa Mola wako kwa haki ili Awathibitishie walo walioamini na ni uongofu na bishara kwa Waislamu. Na Sisi hakika tunajua kwamba wanasema: "Yuko mtu anayemfundisha. Lugha ya huyo wanaye muelekezea ni ya kigeni na hii ni lugha ya Kiarabu bayana.”* ***(16:101-103)***

## MAELEZO

Aayah zote hizi tukufu ni zenye kubainisha na kuthibitisha sifa za Allaah (Jalla wa ´Alaa). Kumeshatangulia sehemu ya Aayah. Hizi ni zenye kubainisha maneno ya Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Allaah alisema, anasema na atasema:

## *Dalili ya Maneno na Kuzungumza kwa Allaah*

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ

**″Na Atakaposema Allaah: "Ee 'Iysaa mwana wa Maryam!" (05:116)**

وَمَنْ أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ قِيلًا

**″Na nani aliye mkweli zaidi kwa kauli kuliko Allaah?″ (04:122)**

وَمَنْ أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ حَدِيثًا

**″Na nani mkweli zaidi katika maneno kuliko Allaah?″(04:87)**

يُرِيدُونَ أَن يُبَدِّلُوا كَلَامَ اللَّهِ

**″Wanataka kubadilisha Maneno ya Allaah." (48:15)**

وَكَلَّمَ اللَّهُ مُوسَىٰ تَكْلِيمًا

**″Na bila shaka Allaah Alimsemesha Muwsaa maneno moja kwa moja.″(04:164)**

Aayah kuhusiana na hili ni nyingi zinazothibitisha maneno, wito na kunong´oneza:

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ

**″Na Siku Atakayowaita... " (28:62)**

وَقَرَّبْنَاهُ نَجِيًّا

**″... na Tukamkurubisha kuzungumza naye kwa siri.″(19:52)**

Hakika Yeye (Subhaanah) alizungumza na anazungumza pale anapotaka. Aliita na anaita pale anapotaka. Anamzungumzisha amtakaye katika waja Wake kama alivyomzungumzisha Muusa (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) na atawazungumzisha walioko Peponi. Vilevile alimzungumzisha Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) usiku aliyopandishwa. Yote haya yalitokea.

Hakika Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) anakijua kila kitu na hakuna kinachofichikana Kwake (Jalla wa ´Alaa).

Qur-aan imeteremshwa na *Wahy* ukateremka kwa Mitume (´alayhimus-Salaam). Yeye yuko juu (Jalla wa ´Alaa). Ameteremsha Kitabu Chake kutoka juu. Amesema (Ta´ala):

## *Dalili kwamba Qur-aan imeteremshwa kutoka kwa Allaah*

قُلْ نَزَّلَهُ رُوحُ الْقُدُسِ مِن رَّبِّكَ بِالْحَقِّ

**"Sema: Roho Takatifu [Jibriyl] ameiteremsha kutoka kwa Mola wako kwa haki." (16:102)**

Hakika Yeye (Subhaanah) yuko juu. Ameteremsha Vitabu Vyake Tawraat, Injiyl, Qur-aan na Zabuur. Vyote vimeteremshwa kutoka kwa Allaah. Yote haya ni wajibu kumthibitishia Allaah na kwamba ndio maneno ya kweli kabisa kutoka kwa viumbe Wake (Subhaanahu wa Ta´ala). Kadhalika inatakiwa kuamini kwamba Qur-aan ni uongofu kwa watu, kwamba ameiteremsha kwa lugha ya kiarabu na kinawasimulia wana wa Israaiyl mengi ambayo walikuwa wakitofautiana. Yote haya ni haki ambayo ni wajibu kuyaamini na kuamini yale yote yaliyoelezwa na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuhusu maneno Yake, wito Wake, Kauli Yake, uteremshwaji wa Kitabu Chake na Vitabu vya Mitume wengine (´alayhimus-Salaam).

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni wenye kumthibitishia Allaah sifa hizi kwa njia inayolingana na utukufu Wake na kwamba Alisema na Anasema, Alizungumza na Anazungumza, Alinong´ongeza na Ananong´oneza, Alizungumza kwa siri na Anazungumza kwa siri pindi anapotaka na kwa namna anayotaka (Subhaanahu wa Ta´ala).

## *Allaah anazungumza pale anapotaka*

Kuhusiana na maneno ya wanafalsafa ya kwamba maneno ni ya kale ni batili. Alizungumza na anazungumza pale anapotaka. Alimzungumzisha Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) usiku wa Mi´raaj katika wakati

wake. Alimzungumzisha Mtume Wake Muusa (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) katika wakati wake. Atazungumza na watu siku ya Qiyaamah katika wakati wao. Alizungumza na Aadam (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) katika wakati wake. Atazungumza na watu wa Peponi katika wakati wao. Ni Mwenye kuzungumza (Subhaanahu wa Ta´ala) siku zote pale anapotaka. Kama alivyozungumza hapo kale pia hivi sasa ni Mwenye kuzungumza. Hakuna chenye kumzuia na kufanya hivo (Jalla wa ´Alaa). Anazungumza pale anapotaka. Hutaka pale anapotaka. Huamrisha pale anapotaka. Hukataza pale anapotaka. Hakuna mwenye kumzuia kufanya hivo (Subhaanahu wa Ta´ala).

## 30. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Qur-aan VIII

*Amesema (Ta´ala):*

وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ

*”[Kuna] nyuso siku hiyo zitanawiri. Zikimtazama Mola wake.”* ***(75:22-23)***

عَلَى الْأَرَائِكِ يَنظُرُونَ

*”Kwenye makochi [ya fakhari] wakitazama.”* ***(83:23)***

لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ

*”Kwa wale waliofanya wema watapata [jazaa ya] Pepo na zaidi.”* ***(10:26)***

لَهُم مَّا يَشَاءُونَ فِيهَا وَلَدَيْنَا مَزِيدٌ

*”Watapata humo wayatakayo na Kwetu kuna yaliyo ziada.”* ***(50:35)***

Mlango huu umekuja katika Kitabu cha Allaah (Ta´ala) sehemu nyingi. Yule mwenye kuizingatia Qur-aan na huku anatafuta uongofu wake, basi itambainikia Njia ya haki.

**MAELEZO**

Amesema (Jalla wa ´Alaa):

### *Dalili kwamba waumini watamuona Mola wao Aakhirah*

وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ

**”[Kuna] nyuso siku hiyo zitanawiri." (75:22)**

Nyuso zitanawiri na kung´ara.

إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ

**"Zikimtazama Mola wake." (75:23)**

Zitamtazama.

عَلَى الْأَرَائِكِ يَنظُرُونَ

**"Kwenye makochi [ya fakhari] wakitazama." (83:23)**

لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ

**"Kwa wale waliofanya wema watapata [jazaa ya] Pepo na zaidi." (10:26)**

Neno "ziada" maana yake ni kuangalia uso wa Allaah (Jalla wa ´Alaa). Yote haya ni haki. Hakika Yeye (Subhaanah) atawatazama waja Wake na wao watamtazama siku ya Qiyaamah watapokuwa Peponi. Yote haya ni haki. Mlango huu katika Qur-aan umezungumziwa sana. Kadhalika katika Hadiyth Swahiyh umezungumziwa sana. Mwenye kuizingatia Qur-aan na Sunnah basi atakuta hilo liko wazi katika Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kuona kuwa vyote viwili vinamthibitishia sifa Allaah (´Azza wa Jall) ikiwa ni pamoja na ujuzi, uwezo, maneno, ujuu, radhi, ghadhabu, cheko na sifa za Allaah (Jalla wa ´Alaa) nyenginezo. Hivyo ni wajibu kumthibitishia nazo Allaah kwa njia inayolingana Naye (Subhaanahu wa Ta´ala). Inatakiwa kuzipitisha kama zilivyokuja pasi na kuzipotosha, kuzikanusha, kuziwekea namna na kuzilinganisha. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaona kuwa mlango huu ni mmoja na kwamba inatakiwa kuthibitisha ya kuwa ni haki na maana yake vilevile ni haki. Pamoja na hivyo hakuna anayejua namna zilivyo isipokuwa Yeye peke yake (Subhaanahu wa Ta´ala). Sambamba na hilo inatakiwa kutambua na kuamini kuwa hazifanani na sifa za viumbe:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye**

**kuona." (42:11)**

Kama ambavyo dhati ya Allaah (Jalla wa ´Alaa) haifanani na dhati za viumbe, vilevile sifa Zake hazifanani na sifa za viumbe. Majina na sifa Zake zote ni haki. Ni wajibhu kumthibitishia navyo Allaah kwa njia inayolingana na Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Hivi ndivyo alivyosema Maalik, Sufyaan ath-Thawriy, Ibn ´Uyaynah, Imaam Ahmad bin Hanbal, Ishaaq bin Raahuuyah, Imaam ash-Shaafi´iy na wengineo katika maimamu wa Uislamu. Mlango wao ni mmoja. Mlango ni mmoja: ni wajibu kuthibitisha Aayah na Hadiyth kuhusu sifa kama zilivyokuja kwa njia inayolingana na Allaah (Jalla wa ´Alaa) pasi na kupotosha, kukanusha, kuzifanyia mamna na kufananisha. Bali ni haki zimethibiti kwa Allaah (´Azza wa Jall). Sifa za Allaah hazifanani na sifa za viumbe Wake (Subhaanahu wa Ta´ala).

## 31. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Sunnah I

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Sunnah ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndio yenye kuifasiri Qur-aan na kuiweka wazi, kuithibitisha na kuja na maana mpya na hukumu [ambazo hazikuja katika Qur-aan]. Vilevile ni wajibu kuamini yale Mtume aliyomsifu kwayo Mola Wake (´Azza wa Jall) kutokana na zile Hadiyth Swahiyh ambazo wamezikubali watu wa maarifa, kwa mfano maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):*

*"Huteremka Mola Wetu katika mbingu ya dunia kila usiku pale kunapobaki theluthi ya mwisho ya usiku na Kusema: "Ni nani mwenye kuniomba nimjibie? Ni nani mwenye kuniuliza nimpe? Ni nani mwenye kuniomba msamaha nimsamehe?"*[15]

*"Allaah Hufurahi sana kwa Tawbah ya mja Wake muumini anapotubia, kuliko furaha ya mmoja wenu kwa kupata kipando chake... "*[16]

*"Allaah Anawacheka watu wawili ambapo mmoja wao kamuua mwenzake. Halafu wote wawili wanaingia Peponi."*[17]

*"Anastaajabu Mola Wetu kwa kukata tamaa waja Wake licha ya mabadiliko Yake ya hali zao yako karibu. Huwatazama mnapokuwa katika hali ngumu na wenye kukata tamaa. Huanza kucheka kwa kuwa Anajua kuwa faraja yenu iko karibu."*[18]

---

[15] al-Bukhaariy (7494) na Muslim (758).

[16] al-Bukhaariy (6308) na (2744).

[17] al-Bukhaariy (2826) na Muslim (1890).

[18] Ahmad (4/11) na Ibn Maajah (181). Katika mlolongo wa wapoezi wake kuna udhaifu. Katika mlolongo wa wapokezi wake amekuja Wakiy´ bin Hadas. Imaam al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) amesema kuwa ni mdhaifu katika "Sunan Ibn Maajah". Hata hivyo Hadiyth iliyopokelewa na Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh): "Allaah (´Azza wa Jalla) Hustaajabu kwa huyu na huyu... " ni Swahiyh. Tazama "Swahiyh al-Bukhaariy" (4889)).

*"Haitoacha Jahannam kutupwa ndani yake [watu na mawe] nayo inasema "Je, kuna zaidi?", mpaka Mola Aliyetukuka Aweke Mguu Wake kisha pawe sawa. Hapo ndio itasema "Inatosha! Inatosha!""*[19]

*"Allaah (Ta´ala) Atasema: "Ee Aadam!" Atajibu: "Ninaitikia wito Wako na nakuomba unifanye ni mwenye furaha na Kunisaidia." Kisha Atanadi kwa Sauti: "Hakika Allaah Anakuamrisha utoe moja katika kizazi chako Motoni.""*[20]

**MAELEZO**

Hadiyth hizi sita ni kama Aayah zilizo kabla yake. Ni kama jinsi Qur-aan inavyofahamisha kuthibitisha sifa na majina kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) na kwamba Yeye (Jalla wa ´Alaa) anaitwa kwa majina mazuri kabisa na anasifika vilevile kwa sifa kuu. Kama ambavyo imekuja katika Qur-aan kadhalika imekuja katika Sunnah.

Hakika ya Sunnah Swahiyh za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) zinaifasiri Qur-aan, kuibainisha, kuithibitisha na kuja na maana na hukumu mpya. Qur-aan imetoa ushahidi juu ya hili. Amesema (Jalla wa ´Alaa):

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ

**"Hakika waumini [wa kweli] ni wale waliomwamini Allaah na Mtume Wake... " (24:62)**

أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ

**"Mtiini Allaah na mtiini Mtume." (04:59)**

وَالنَّجْمِ إِذَا هَوَىٰ مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ

**"Naapa kwa nyota inapotua. Hakupotea sahibu yenu na wala hakukosea. Na wala hatamki kwa matamanio yake. Hayo [ayasemayo] si chochote isipokuwa**

[19] al-Bukhaariy (4850) na Muslim (2846).

[20] al-Bukhaariy (3348) na Muslim (222).

**ni *Wahy* unaofunuliwa." (53:01-04)**

Kama ambavyo kumekuja Aayah zenye kuzungumzia sifa na majina ya Allaah na Sunnah imefanya vivyo hivyo. Yaliyothibiti katika Sunnah Swahiyh hukumu yake ni kama ile iliyothibiti katika Qur-aan. Kwa hivyo itakuwa ni wajibu kumthibitishia nayo Allaah na kuamini kuwa ni sifa na majina ya Allaah kwa njia inayolingana Naye (Subhaanah) pasi na kupotosha, kukanusha, kuzifanyia namna na kulinganisha. Mlango na hukumu ni moja. Yaliyokuja katika Sunnah Swahiyh hukumu yake ni kama yaliyokuja katika Qur-aan. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaonelea kuwa yote ni sawa sawa. Kwa mfano maneno yake Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

## *Dalili ya kwamba Allaah Huteremka katika mbingu ya chini*

"Huteremka Mola Wetu katika mbingu ya dunia kila usiku pale kunapobaki theluthi ya mwisho ya usiku na Kusema: "Ni nani mwenye kuniomba nimjibie? Ni nani mwenye kuniuliza nimpe? Ni nani mwenye kuniomba msamaha nimsamehe?"

Ahl-us-Sunnah wanamthibitishia Allaah sifa ya ushukaji huu. Ni ushukaji unaolingana na Allaah. Hafanani na viumbe Wake katika ushakaji Wake. Kiumbe yeye kwa mfano hushuka kutoka juu na kwenda chini na kutoka juu ya mlima na kwenda chini. Lakini hata hivyo ushukaji wa Allaah sio kama ushukaji wa kiumbe. Kadhalika neno la Allaah sio kama neno la kiumbe, wito wa Allaah sio kama wito wa kiumbe na maneno ya Allaah sio kama maneno ya kiumbe. Sifa za Allaah ni zenye kulingana Naye na Yeye ndiye Mwenye kumuitikia muombaji:

"Ni nani mwenye kuniomba nimjibie? Ni nani mwenye kuniuliza nimpe? Ni nani mwenye kuniomba msamaha nimsamehe?"

Hakika Yeye ni Mwingi wa kutoa na ni Mkarimu (Subhaanahu wa Ta´ala). Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu. Ni wajibu kumthibitishia Allaah sifa hizi kwa njia inayolingana Naye. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

### *Dalili ya Kucheka kwa Allaah*

"Allaah Anawacheka watu wawili ambapo mmoja wao kamuua mwenzake. Halafu wote wawili wanaingia Peponi."

Ni kucheka kunakolingana na Allaah. Hashabihiani na viumbe Vyake katika sifa zao na kucheka kwao. Bali sifa za Allaah zinalingana Naye na zinahusiana Naye (Jalla wa ´Alaa). Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

### *Dalili ya Kustaajabu kwa Allaah*

"Anastaajabu Mola Wetu kwa kukata tamaa waja Wake licha ya mabadiliko Yake ya hali zao yako karibu... "

Bi maana mambo kubadilika. Mtu wakati mwingine anaweza kukata tamaa kutokana na njaa kali pamoja na kuwa faraja ya Allaah iko karibu.

"... Huwatazama mnapokuwa katika hali ngumu na wenye kukata tamaa. Huanza kucheka kwa kuwa Anajua kuwa faraja yenu iko karibu."

Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

### *Dalili kuwa maneno ya Allaah ni ya Herufi na Sauti*

"Allaah (Ta´ala) Atasema: "Ee Aadam!" Atajibu: "Ninaitikia wito Wako na nakuomba unifanye ni mwenye furaha na Kunisaidia." Kisha Atanadi kwa Sauti: "Hakika Allaah Anakuamrisha utoe moja katika kizazi chako Motoni.""

Hapa kuna uthibitisho wa sauti kwa Allaah na kwamba Yeye (Subhaanah) ana sauti yenye kusikika. Sauti hiyo waliisikia Malaika, Muusa (´alayhis-Salaam) na aliisikia vilevile Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) usiku wa Israa´.

Maneno Yake (Ta´ala):

"Hakika Allaah Anakuamrisha utoe moja katika kizazi chako Motoni."

Imekuja katika Hadiyth nyingine:

"Miongoni mwa [watu] elfu moja [kutabaki] mia tisa tisini na tisa."

Idadi hii ndio itatolewa Motoni. Hakuna atayeokoka katika idadi elfu moja isipokuwa mtu mmoja tu na mia tisa tisini na tisa watabakizwa Motoni. Hii inaonyesha ni khatari kubwa iliyoje itakuwepo. Kwa ajili hii ndio maana (Jalla wa ´Alaa) amesema:

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ

**"Na wengi wa watu hawatoamini japokuwa utatilia hima." (12:103)**

وَإِن تُطِعْ أَكْثَرَ مَن فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ

**"Na kama ukiwatii wengi walioko ulimwenguni, watakupoteza na njia ya Allaah." (06:116)**

وَلَقَدْ صَدَّقَ عَلَيْهِمْ إِبْلِيسُ ظَنَّهُ

**"Na kwa yakini Ibliys alisadikisha dhana yake juu yao." (34:20)**

Pindi Maswahabah waliposikia kuhusu jambo hili ya kwamba katika watu elfu moja kutatolewa mmoja, jambo hili liliwawia zito kwao. Ndipo (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akawaambia katika ukamilifu wa Hadiyth:

"Msikhofu! Hawa mia tisa tisini na tisa ni katika Ya´juu na Ma´juuj. Miongoni mwenu kuna mmoja tu katika Ummah wa Muhammad mbali na Ya´juuj Na Ma´juuj."

Hii ni dalili yenye kuonyesha kuwa wengi wataoingia Motoni ni katika Ya´juuj na Ma´juuj. Hawa ni watu waovu kabisa ambao watajitokeza katika zama za mwisho. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa salla):

### *Dalili ya Mguu wa Allaah*

"Haitoacha Jahannam kutupwa ndani yake [watu na mawe] nayo inasema "Je, kuna zaidi?", mpaka al-Jabbaar aweke ndani yake Mguu Wake."

Katika upokezi mwingine imekuja:

"... Mguu Wake kisha pawe sawa. Hapo ndio itasema "Inatosha! Inatosha!"[21]

Hapa kuna uthibitisho wa mguu. Inatakiwa kuthibitisha mguu kwa njia inayolingana na Allaah. Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona, ana mkono na mguu. Zote hizi ni sifa zinazolingana Naye. Hashabihiani na viumbe katika sifa Zake. Hafanani nao katika usikizi Wake, uoni Wake, mkono Wake, mguu Wake, kucheka Kwake na nyenginezo. Kucheka kwa Allaah na kusikia Kwake kunalingana Naye na upande mwingine sifa za viumbe zinalingana nao. Amesema (Ta´ala):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." **(42:11)**

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye." (112:04)**

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

**"Basi msipigie mifano Allaah! Hakika Allaah Anajua nanyi hamjui."(16:74)**

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanasema namna hii kuhusu sifa zote. Mlango wake ni mmoja. Hili ni tofauti na Jahmiyyah, Mu´tazilah, Ashaa´irah na wengineo walioziharibu sifa za Allaah. Jahmiyyah wanakanusha majina na sifa za Allaah vyote viwili. Mu´tazilah wanakanusha sifa na wakati huo huo wamethibitisha majina matupu yasiyokuwa na maana. Ashaa´irah na mapote mengine wamekanusha baadhi na wakati huo huo wakathibitisha nyenginezo.

Usawa ni kuthibitisha majina na sifa zote za Allaah zilizokuja katika Qur-aan na Sunnah. Yale sahihi yaliyopokelewa kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni kama mfano wa yale yaliyokuja katika Qur-aan. Ni

[21] al-Bukhaariy (4850) na Muslim (2846).

wajibu kumthibitishia nayo Allaah kwa njia inayolingana Naye bila ya kupotosha, kukanusha, kuzifanyia namna na kulinganisha. Inatakiwa kuyathibitisha katika mpaka wa Kauli Yake (Subhaanah):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)**

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Na wala hana yeyote anayefanana [kulingana] Naye." (112:04)**

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ

**"Basi msimpigie mifano!" (16:74)**

Vilevile Hadiyth isemayo:

### *Dalili ya Kufurahi kwa Allaah*

"Allaah Hufurahi sana kwa Tawbah ya mja Wake muumini anapotubia, kuliko furaha ya mmoja wenu kwa kupata kipando chake... "

Kufurahi kwa Allaah kunalingana na Allaah. Anafurahi lakini hata hivyo sio kama wanavyofurahi viumbe. Anaridhia lakini lakini sio kama wanavyoridhia viumbe. Anakasirika lakini lakini sio kama wanavyokasirika viumbe.

Hadiyth hii inahusiana na mtu aliyempoteza ngamia wake na alikuwa jangwani amelala chini ya mti na huku anasubiri tu mauti yamfike. Tahamaki akamuona ngamia wake amesimama juu ya kichwa chake. Akasema kutokana na wingi wa furaha:

"Ee Allaah! Hakika wewe ni mja wangu na mimi ndiye Mola Wako." Alikosea kutokana na wingi wa furaha.""

Allaah (Subhaanah) ni mwenye furaha zaidi juu ya tawbah ya mja Wake kuliko mtu huyu. Pamoja na kuwa Yeye ndiye ambaye amemtunukia tawbah hii. Lakini pamoja na hivyo anaifurahia kutoka kwa mja Wake. Allaah (Jalla wa ´Alaa) ndiye ambaye amemtunukia na kumuwafikisha nayo.

## 32. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Sunnah II

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa salam):*

*"Hakuna yeyote katika nyinyi isipokuwa Mola Wake Atamsemeza. Kutakuwa hakuna baina yake na baina Yake mwenye kutarjumu."*[22]

*Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuhusu* Ruqyah *ya mgonjwa:*

*"Mola Wetu ni Allaah Ambaye Yuko juu ya mbingu, Limetakasika Jina Lako. Amri Yako iko mbinguni na ardhini. Teremsha Rahmah yako katika ardhi kama jinsi Rahmah Yako iko mbinguni. Tusamehe madhambi yetu makubwa na madogo. Wewe ni Mola wa wazuri. Teremsha Rahmah katika Rahmah Yako na dawa katika Dawa Yako kwa huyu mwenye maumivu."*[23]

*Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):*

*"Je, hamniamini na mimi nimeaminiwa na Aliye juu ya mbingu?"*[24]

*"… na ´Arshi iko juu ya maji, na Allaah Yuko juu ya ´Arshi, Naye Anajua yale mliyomo."*[25]

*Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kumwambia kijakazi:*

*"Yuko wapi Allaah?" Akasema: "Mbinguni." Kisha akamuuliza: "Mimi ni nani?" Akasema: "Wewe ni Mtume wa Allaah." Akasema: "Muache huru, hakika ni muumini."*[26]

---

[22] al-Bukhaariy (7443) na Muslim (1016)

[23] Abuu Daawuud (3892), an-Nasaa´iy (10876), al-Haakim (1/344) na (3/218) na wengine.

[24] al-Bukhaariy (4351) na Muslim (1064).

[25] Abuu Daawuud (3451). Imaam al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) kasema kuwa ni dhaifu katika kitabu cha Ibn Abiy ´Aasim "Kitaab-us-Sunnah" (577).

*"Kiwango bora cha Imani ni wewe ujue kuwa Allaah Yuko pamoja na wewe popote ulipo."*[27]

*"Anaposimama mmoja wenu katika Swalah, asiteme mate mbele yake wala kuliani kwake, kwani hakika Allaah Yuko mbele Yake. Badala yake [ateme] kushotoni kwake au chini ya mguu wake."*[28]

## MAELEZO

Hizi ni sehemu ya Hadiyth ambazo zimepokelewa kuhusu sifa. Baadhi ya sifa hizi zimekwishatangulia. Lengo la mwandishi (Rahimahu Allaah) ni kutaja sehemu katika Aayah na Hadiyth zilizothibiti kuhusu sifa ili muislamu apate kujua yaliyoko nyuma yake. Ametaja jumla ya Aayah na Hadiyth zilizothibiti kuhusu majina na sifa za Allaah na kwamba Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaamini yale mambo yanayotolewa dalili na majina na sifa hizo. Wanazipitisha kama zilivyokuja pasi na kuzipotosha, kuzikanusha, kuzifanyia namna na kuzilinganisha. Ahl-us-Sunnah hawazipingi kama wanavyofanya Jahmiyyah na Mu´tazilah. Hawazifasiri kwa kupindisha maana kama wanavyofanya baadhi ya Maaturiydiyyah, Ashaa´irah na wengineo. Wanazipitisha kama zilivyokuja. Sambamba na hilo wanaziamini, wanazithibitisha na wanaitakidi yale yenye kufahamishwa na majina na sifa hizo na wakati huo huo wanamtakasa Allaah kufanana na viumbe Wake. Ahl-us-Sunnah hawaonelei ukanushaji wala ufananizi. Ni Ayaah na Hadiyth vilivyothibiti na maana yake ni sahihi. Ndani yavyo hamna ufananizi, ushabihishaji wala ukanushaji. Miongoni mwazo ni maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhiwa salam):

---

[26] Muslim (537).

[27] Abuu Nu´aym (6/124). Katika isnadi kuna udhaifu. Katika isnadi kumekuja Nu´aym bin Hamaad. Imaam al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) kasema kuwa ni mdhaifu katika "Dhwa´iyf al-Jaami´ as-Swaghiyr" (1100).

[28] al-Bukhaariy (406) na Muslim (547).

## *Dalili ya Kuzungumza kwa Allaah*

“Hakuna yeyote katika nyinyi isipokuwa Mola Wake Atamsemeza. Kutakuwa hakuna baina yake na baina Yake mwenye kutarjumu... "

Bi maana mkati kati.

"Atazame kuliani mwake asione jengine isipokuwa yale aliyoyatanguliza, kushotoni mwake asione jengine isipokuwa yale aliyoyatanguliza na atazame mbele yake asione jengine isipokuwa Moto ukimkabili. Hivyo basi, uogopeni Moto ijapokuwa kwa kipande cha tende. Asiyekipata basi angalau [azungumze] neno zuri."

Hii ni dalili yenye kuonyesha kuwa kuzungumzishwa itakuwa kwa watu wote siku ya Qiyaamah.

“Hakuna yeyote katika nyinyi isipokuwa Mola Wake Atamsemeza... "

Lakini hata hivyo waovu watazungumzishwa kwa maneno yenye kuwadhuru na ya kuwaghadhibikia. Upande mwingine wema watazungumzishwa kwa maneno yenye kuwafurahisha.

## *Dalili ya kwamba Allaah yuko juu*

Amesema (´alayhis-Swalaatu was-Salaam):

“Je, hamniamini na mimi nimeaminiwa na Aliye juu ya mbingu?”[29]

Bi maana yuko juu.

“Mola Wetu ni Allaah Ambaye Yuko juu ya mbingu, Limetakasika Jina Lako. Amri Yako iko mbinguni... "

Bi maana iko juu.

“Mola Wetu ni Allaah Ambaye Yuko juu ya mbingu, Limetakasika Jina Lako."

[29] al-Bukhaariy (4351) na Muslim (1064).

Bi maana juu.

"Teremsha Rahmah yako... "

Hii ni dalili yenye kuonyesha Ujuu.

Maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"´Arshi iko juu ya maji, na Allaah Yuko juu ya ´Arshi, Naye Anajua yale mliyomo."

Haya ni kama mfano wa yale yaliyotangulia katika Kauli Yake (Ta´ala):

الرَّحْمَٰنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَىٰ

*"Mwingi wa Rahmah amelingana juu ya ´Arshi."* ***(20:05)***

## 33. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Sunnah III

Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

### *Dalili kwamba Allaah yuko mbele ya mswalaji*

"Anaposimama mmoja wenu katika Swalah, asiteme mate mbele yake wala kuliani kwake, kwani hakika Allaah Yuko mbele Yake. Badala yake [ateme] kushotoni kwake au chini ya mguu wake."

Allaah yuko juu ya ´Arshi na wakati huo huo yuko mbele ya mwenye kuswali. Hakuna kipingamizi. Hakika Allaah yuko pamoja nasi popote tunapokuwa. Amesema (Ta´ala):

وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنتُمْ

**"Naye Yu pamoja nanyi popote mlipo." (57:04)**

### *Dalili ya Allaah kuwa kila mahali kwa ujuzi Wake*

"Kiwango bora cha Imani ni wewe ujue kuwa Allaah Yuko pamoja na wewe popote ulipo."

Yeye yuko pamoja naye kwa ujuzi Wake na wakati huo huo yuko juu ya mbingu kwa dhati Yake (Jalla wa ´Alaa). Yuko juu na wakati huo huo yuko pamoja nasi kwa kutuzunguka kielimu (Jalla wa ´Alaa). Yeye (Subhaanah) yuko juu ya ´Arshi na juu ya viumbe wote na wakati huo huo ujuzi Wake uko kila mahali. Hakuna chochote asichokijua kutokana na ujuzi Wake (Jalla wa ´Alaa). Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema katika kisa cha Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akiwa pamoja na as-Swiddiyq (Radhiya Allaahu ´anh) pindi (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliposema ilihali wamo pangano:

لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا

**"Usihuzunike, hakika Allaah Yu Pamoja nasi." (09:40)**

Vilevile amesema katika kisa cha Muusa na Haaruun (´alayhimaas-Swalaatu was-Salaam):

قَالَ لَا تَخَافَا ۖ إِنَّنِي مَعَكُمَا أَسْمَعُ وَأَرَىٰ

**"Hakika Mimi Niko pamoja nanyi, Nasikia na Naona." (20:46)**

وَاصْبِرُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ

**"Na subirini. Hakika Allaah Yu Pamoja na wanaosubiri." (08:46)**

Huu ni upamaja wa kimaalum na ulioenea:

وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنتُمْ

**"Naye Yu pamoja nanyi popote mlipo." (57:04)**

Ni wajibu kwa waislamu kuyatambua mambo haya ya kwamba Allaah yuko pamoja na viumbe Wake kwa kuwazunguka kielimu. Kadhalika kwamba yuko pamoja na mawalii Wake kwa kiujuzi, kuwaangalia, kuwahifadhi na kuwajali (Subhaanahu wa Ta´ala) na wakati huo huo yuko juu ya ´Arshi (Subhaanahu wa Ta´ala) na juu ya viumbe wote. Amesema (Ta´ala):

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ

**"Hakika Mola wenu ni Allaah Ambaye Ameumba mbingu na ardhi katika siku sita kisha akalingana juu ya ´Arshi." (07:54)**

Yeye (Jalla wa ´Alaa) yuko juu ya ´Arshi na ujuzi Wake umeenea kila mahali (Subhaanahu wa Ta´ala).

Ni wajibu kwa kila muislamu ambaye ´ibaadah ni yenye kumuwajibikia kuitakidi ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ikiwa ni pamoja na kuamini kuwa Allaah yuko juu na amelingana juu ya ´Arshi, hakuna chochote

kinachofichikana Kwake na ujuzi Wake umewazunguka waja Wake popote wanapokuwa.

## 34. Sifa na majina ya Allaah yaliyothibiti katika Sunnah IV

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:*

*"Allaah Ndiye Mola wa mbingu hizi saba na ardhi na Ndiye Mola wa ´Arshi kubwa. Mola Wetu na Mola wa kila kitu. Mpasuaji wa mbegu na kokwa na Ambaye Umeteremsha Tawraat, Injiyl na Qur-aan. Najikinga Kwako na shari ya nafsi yangu na shari ya kila kiumbe kiovu ambacho wewe una utawala juu yake. Wewe ni wa Mwanzo na hakuna kabla Yako kitu. Na Wewe ni wa Mwisho na hakuna baada Yako kitu. Na Wewe ni wa Juu na hakuna juu Yako kitu. Na wewe ni wa Karibu na hakuna kinachojificha Kwako. Nilipitie deni langu na nitajirishe na ufakiri wangu."*[30]

*Na maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuwaambia Maswahabah pindi waliponyanyua sauti zao kwa Dhikr:*

*"Enyi watu! Zihurumieni nafsi zenu! Kwani hakika hamumuombi ambaye ni kiziwi wala asiyekuwepo. Hakika Yule mnayemwomba ni Mwenye Kusikia Mwenye kuona na Aliye karibu. Hakika yule mnayemwomba Yuko karibu na mmoja wenu kuliko shingo ya mpando wenu."*[31]

*"Hakika nyinyi mtamuona Mola Wenu kama mnavyouona* mwezi *usiku wa mwezi mng'aro – hamtosongamana katika kumuona. Hivyo ikiwa mnaweza kuswali kabla ya jua kuchomoza na jua kuzama, basi fanyeni hivyo."*[32]

*Tazama Hadiyth hizi na mfano wake ambapo anaelezea Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuhusu Mola Wake. Hakika al-Firqat-un-Naajiyah, Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, wanaamini hayo kama jinsi wanavyoamini Aliyojielezea Allaah katika Kitabu Chake, bila ya Tahriyf, Ta´twiyl, Takyiyf wala Tamthiyl.*

---

[30] Muslim (2713).

[31] al-Bukhaariy (4205) na (6384) na Muslim (2704).

[32] al-Bukhaariy (554) na (574) na Muslim (633).

*Bali wao wako kati kwa kati baina ya mapote ya Ummah, kama jinsi Ummah ulivyo kati kwa kati baina ya Ummah zingine.*

*Wako kati kwa kati katika mlango wa Sifa za Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) – baina ya Ahl-ut-Ta´twiyl wanaokanusha Jahmiyyah na Ahl-ut-Tamthiyl wanaofananisha Mushabbihah.*

*Wako kati kwa kati katika mlango wa Matendo ya Allaah (Ta´ala) – baina ya Qadariyyah na Jabriyyah.*

*Hali kadhalika katika mlango wa Tishio la Allaah – baina ya Murji-ah na Wa´iydiyyah miongoni mwa Qadariyyah na wengineo.*

*Hali kadhalika katika mlango wa Imani na majina ya Dini – baina ya Haruuriyyah na Mu´tazilah, Murji-ah na Jahmiyyah.*

*Hali kadhalika kuhusiana na Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) – kati ya Rawaafidhw na Khawaarij.*

**MAELEZO**

Mwandishi (Rahimahu Allaah) anasema kuhusu Hadiyth zingine ambazo zimetaja kuhusu sifa ikiwa ni pamoja na Hadiyth ifuatayo:

### *Dalili ya Sifa mbalimbali za Allaah*

"Allaah Ndiye Mola wa mbingu hizi saba na ardhi na Ndiye Mola wa ´Arshi kubwa. Mola Wetu na Mola wa kila kitu. Mpasuaji wa mbegu na kokwa na Ambaye Umeteremsha Tawraat, Injiyl na Qur-aan. Najikinga Kwako na shari ya nafsi yangu na shari ya kila kiumbe kiovu ambacho wewe una utawala juu yake. Wewe ni wa Mwanzo na hakuna kabla Yako kitu. Na Wewe ni wa Mwisho na hakuna baada Yako kitu. Na Wewe ni wa Juu na hakuna juu Yako kitu. Na wewe ni wa Karibu na hakuna kinachojifichika Kwako. Nilipitie deni langu na nitajirishe na ufakiri wangu."

Katika Hadiyth hii kubwa ambayo ameipokea Muslim ndani yake mna sifa aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na kwamba yuko juu ya ´Arshi, yuko juu ya mbingu,

Mola wa ardhi, mteremshaji wa Tawraat, Injiyl na Qur-aan. Zote hizi zinatoa dalili kuonyesha Ujuu Wake (Subhaanahu wa Ta´ala) na kwamba kutoka Kwake ndiko kunateremka kila kitu. Kutoka Kwake kunateremka maamrisho na *Wahy* ilihali yuko juu ya ´Arshi (Jalla wa ´Alaa). Yuko juu ya viumbe vyote (Subhaanahu wa Ta´ala).

Vilevile mambo yote yako mikononi Mwake na anayaendesha vile anavyotaka (Subhaanahu wa Ta´ala). Yeye ndiye wa Mwanzo na hakuna kabla Yake kitu, wa Mwisho na hakuna kitu baada Yake, wa Juu na hakuna kitu juu Yake na wa Karibu na hakuna kinachofichikana Kwake, kama ilivyokuja katika Qur-aan tukufu:

هُوَ الْأَوَّلُ وَالْآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

**"Yeye Ndiye wa Mwanzo na wa Mwisho na Aliye juu na Aliye Karibu, Naye kwa kila kitu ni Mjuzi."(57:03)**

Yeye ndiye wa Mwanzo na hakuna kitu kabla Yake, wa Mwisho na hakuna kitu baada yake, Yeye ni wa daima, mkamilifu na hakuacha kutokuwepo (Subhaanahu wa Ta´ala). Kwa msemo mwingine hakuna chochote kilichomtangulia na hafikiwi na kitu kukosekana. Yeye ni wa daima siku zote. Yeye ni wa Juu ambaye yuko juu ya viumbe vyote. Kwa msemo mwingine ni kwamba hakuna kitu kilicho juu Yake. Yeye ndiye wa Juu kabisa, aliye juu ya ´Arshi Yake. ´Arshi ndio sakafu ya viumbe. Yeye ni wa Karibu na hakuna kinachojificha Kwake. Kwa msemo mwingine hakuna Anachohitajia na Yeye anazijua hali za waja Wake na anayajua yaliyomo ndani ya vifua vyao. Katika du´aa hii mna njia ya kuomba kulipiwa deni na kujitosheleza na ufakiri.

## *Dalili kwamba waumini watamuona Mola wao Aakhirah*

Kadhalika kuhusiana na Hadiyth ya Kuonekana:

"Hakika nyinyi mtamuona Mola Wenu siku ya Qiyaamah kama mnavyoona jua wazi wazi pasi na mawingu na kama mnavyouona mwezi usiku wa mwezi mng'aro – hamtosongamana katika kumuona."[33]

Bi maana mtamuona wazi wazi kabisa. Kuona ni ziada ambayo haihitajii msongamano. Kitu kidogo kuna uwezekano watu wakasongamana na kuambizana wakitazame kwa ajili ya kutoonekana kwake vizuri. Ama kuhusiana na Kuonekana Kwake (Subhaanah) kutakuwa wazi wazi kabisa kama mfano wa linavyoonekana jua pasi na mawingu. Kutakuwa hakuna haja ya kusongamana, kubanana na rabsha. Kila mmoja atamuona akiwa yuko sehemu yake bila ya kupata usumbufu.

## *Dalili ya Kusikia na Kuona kwa Allaah*

Vilevile kuhusiana na Hadiyth pale ambapo walinyanyua sauti zao akawaambia:

"Enyi watu! Zihurumieni nafsi zenu! Kwani hakika hamumuombi ambaye ni kiziwi wala asiyekuwepo."

Hapa amewabainishia (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) ya kwamba Yeye (Subhaanah) anayasikia maneno na du´aa za waja Wake. Kwa hivyo hahitajii mtu kunyanyua sauti inayopingana na Shari´ah. Kunyanyua sauti kunatakiwa iwe kwa wastani. Kwa ajili hii ndipo akasema kuwaambia:

"Hamumuombi ambaye ni kiziwi wala asiyekuwepo."

Walikuwa ni wenye kunyanyua sauti zao. Ndipo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akawaamrisha wasifanye hivyo ambapo wanapitiliza katika unyanyuaji. Isipokuwa tu wakati wa Talbiyah. Hili ni jambo ambalo limevuliwa. Kuna dalili zenye kuonyesha kuwa inatakiwa kunyanyua sauti. Ama kuhusu kusema "Allaahu Akbar" inatakiwa iwe kwa sauti ya wastani na isiwe kwa kunyanyua sauti sana. Kwani hamumuombi ambaye ni kiziwi wala asiyekuwepo. Yeye yuko juu ya ´Arshi na wakati huo huo yuko pamoja na waja

[33] al-Bukhaariy (4581) na Muslim (183).

Wake kwa njia ya kwamba anazisikia sauti na maneno yao (Jalla wa ´Alaa). Amesema (Ta´ala):

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ

**"Na watakapokuuliza waja Wangu kuhusu Mimi, basi Mimi ni Aliye karibu - Naitikia du'aa ya muombaji anaponiomba." (02:186)**

## *Dalili ya Allaah kuwa Karibu na waja Wake*

Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Hakika yule mnayemwomba Yuko karibu na mmoja wenu kuliko shingo ya mpando wenu."[34]

Yeye (Subhaanah) yuko karibu na hahitajii mtu akapindukia kwa sauti wakati wa Dhikr. Aombe kwa sauti ya kusikika kidogo kwa njia ya kumdhukuru Allaah na si kwa njia ya kwamba Allaah anahitajia hilo. Anaponyanyua sauti yake kidogo ni kwa njia ya Dhikr na kudhihirisha kumdhukuru Allaah (Jalla wa ´Alaa). Ni kama pale ambapo watu wanapodhihirisha sauti zao wakati wa Talbiyah. Lengo ni kudhihirisha kumdhukuru Allaah (´Azza wa Jall). Vinginevyo ni kwamba Yeye (Subhaanah), ya siri na yaliyojificha, anasikia sauti za waja hata kama watanong´oneza. Hakuna chochote kinachofichikana Kwake. Yeye ni Mwenye kusikia na yukaribu, anazisikia sauti zao hata kama watanong´oneza. Kama ambavyo anazijua hali zao hata kama watazificha. Hakuna chochote kinachojificha Kwake (Jalla wa ´Alaa).

Ni wajibu kwa muumini kumuamini Allaah na kwamba Yeye (Subhaanah) ni Mwenye kusikia na yukaribu, anajua hali za waja Wake, anasikia sauti zao na anajua maombi yao na hakuna chochote chenye kujificha Kwake (Jalla wa ´Alaa) pamoja na kuwa kwa wakati huo huo yuko juu ya ´Arshi na juu ya viumbe wote (Subhaanahu wa Ta´ala). Hii ndio ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Ni tofauti na ´Aqiydah ya Ahl-ul-Bid´ah.

[34] al-Bukhaariy (4205) na (6384) na Muslim (2704).

## Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, watu wa kati kwa kati

**Wako kati kwa kati katika mlango wa Sifa za Allaah... -** ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni ´Aqiydah iliyonyooka na ilio kati kwa kati katika mlango huu na mingine. Wako kati kwa kati kuhusiana na Allaah. Kama ambavyo Ummah huu uko kati kwa kati baina ya nyumati zingine basi Ahl-us-Sunnah wako kati kwa kati katika mlango huu pale ambapo wanamthibitishia Allaah sifa na majina Yake pasi na upotoshaji, ukanushaji, kuziwekea namna na kuzilinganisha. Kwa msemo mwingine wanazipitisha kama zilivyokuja na hawazipotoshi, kuzikanusha na kuzilinganisha sifa za Allaah na sifa za viumbe Wake, kama wanavyofanya Jahmiyyah na Mu´tazilah.

**Hakika al-Firqat-un-Naajiyah, Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, wanaamini hayo... -** Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wao wanazithibitisha uthibitisho usiokuwa na ufananishaji na wakati huo huo wanamtakasa Allaah kufanana na viumbe Vyake utakaso usiokuuwa na ukanushaji. Uthibitishaji wa sifa na majina ya Allaah hauhitajii kufananisha kama ambavyo utakaso vilevile hauhitajii ukanushaji. Bali wanasema kuwa wao wanamthibitishia Allaah sifa na majina kwa njia inayolingana Naye pasi na upotoshaji, ukanushaji, kuyawekea namna na kuyafananisha.

### *Kati ya Jahmiyyah na Mushabbihah*

**Wako kati kwa kati katika mlango wa Sifa za Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala)... -** Wako kati kwa kati inapokuja katika mlango wa sifa na majina ya Allaah baina ya *Ahl-ut-Ta´twiyl* ambao ni Jahmiyyah na *Ahl-ut-Tashbiyh* ambao ni *Mushabbihah.*

Kuhusu Jahmiyyah wanakanusha sifa na majina ya Allaah. Mushabbihah wao wanayathibitisha, lakini pamoja na hivyo wanasema kuwa Mkono wa Allaah ni kama mkono wangu, Sauti ya Allaah ni kama sauti yangu, Mguu wa Allaah ni kama mguu wangu. Wanafananisha sifa za Allaah na za viumbe. Huu ni uovu mkubwa kabisa. Ni kufuru na upotevu. Wako kati kwa kati baina ya *Ahl-ut-Ta´twiyl* ambao ni Jahmiyyah na *Ahl-ut-Tamthiyl Mushabbihah.*

## *Kati ya Qadariyyah na Jabriyyah*

**Wako kati kwa kati katika mlango wa Matendo ya Allaah (Ta´ala)...** - Ahl-us-Sunnah vilevile wako kati kwa kati inapokuja katika mlango wa matendo ya Allaah baina ya Wa´iydiyyah na Qadariyyah. Wanathibitisha matendo ya Allaah na kwamba ni haki. Yeye (Jalla wa ´Alaa) hushuka katika mbingu ya dunia kila usiku, atajionyesha kwa waja Wake siku ya Qiyaamah mpaka waweze kuona uso Wake mtukufu kama unavyoonekana mwezi wazi wazi pasi na kuwepo mawingu (Subhaanahu wa Ta´ala). Huridhia, hughadhibika, huamrisha, hukataza, huumba na huruzuku. Matendo Yake (Subhaanahu wa Ta´ala) ni kitu kimethibiti. Tofauti na Jahmiyyah ambao ni Mu´attwilah na Mu´tazilah wenye kusema kuwa inatakiwa kuthibitisha majina na si sifa. Wanasema kuwa majina ya Allaah yathibitishwe matupu bila ya maana.

## *Kati ya Murji-ah na Wa´iydiyyah*

**Hali kadhalika katika mlango wa Tishio la Allaah... -** Kadhalika wako kati kwa kati inapokuja katika sifa za Allaah baina ya Wa´iydiyyah ambao wanasema kuwa matishio ya Allaah ni lazima yatekelezwe na Murji-ah wenye kuyaondosha matendo [katika imani] na wanaonelea kuwa mja anachotakiwa ni kutamka na kuamini pasi na kuleta matendo kwa kuwa sio katika imani. Wa´iydiyyah ambao ni Mu´tazilah wao wanategemea makemeo ya Allaah na wasema kuwa mtenda dhambi kubwa atadumishwa Motoni endapo atakufa juu ya maasi. Upande mwingine wa Murji-ah wao wanasema kuwa hakuna kitu chenye kuidhuru imani kwa sababu wanaona kuwa matendo hayaingii katika imani. Wanaonelea mtu akitamka na kusadikisha inatosheleza.

Ahl-us-Sunnah wao wanaonelea kuwa imani ni kutamka, kuleta matendo na kuamini na vilevile maasi yanaidhuru imani. Lakini hata hivyo hayawajibishi kudumishwa Motoni, kama wanavyosema Mu´tazilah. Kadhalika hayamfanyi mtu akakufuru, kama wanavyosema Khawaarij. Lakini maasi yanaidhuru na kuidhoofisha. Kuachana na maasi na kutubu kwayo kunaifanya imani kuwa kamilifu.

## *Kati ya Haruuriyyah na Mu´tazilah, na Murji-ah na Jahmiyyah*

**Hali kadhalika katika mlango wa Imani na majina ya Dini... -** Aidha Ahl-us-Sunnah wako kati kwa kati baina ya Wa´iydiyyah ikiwa ni pamoja na Mu´tazilah na Khawaarij vilevile na baina Murji-ah. Khawaarij wanasema imani ni kutamka, kufanya matendo na kuamini, lakini haizidi na wala haipungui. Vilevile Wa´iydiyyah wakiwemo Mu´tazilah wanasema kuwa imani ni kutamka, kufanya matendo na kuamini, lakini haizidi na wala haipungui. Mwenye kufa juu ya maasi anakuwa ni miongoni mwa watu wa Motoni na atadumishwa humo milele. Khawaarij wametofautinaa na Mu´tazilah kwa kuona kuwa ni kafiri na wakati huo huo ni katika watu wa Motoni.

Kuhusiana na Ahl-us-Sunnah wao wako kati kwa kati katika hayo. Wanasema kuwa maasi yanaipunguza imani, lakini hayamfanyi mtu akakufuru. Isipokuwa tu pale mtu atapoyahalalisha. Lakini [ikibidi mtu kuingia] hatodumishwa Motoni milele tofauti na wanavyoonelea Khawaarij na Mu´tazilah.

## *Kati ya Raafidhwah na Khawaarij*

**Hali kadhalika kuhusiana na Maswahabah wa Mtume... -** Ahl-us-Sunnah vilevile wako kati kwa kati inapohusiana na Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) baina ya Raafidhwah na Khawaarij. Raafidhwah wamevuka mipaka na Khawaarij wamezembea. Khawaarij wamewapiga vita Maswahabah na wakakufurisha wengi katika wao. Ama Raafidhwah wao wamevuka mipaka kwa watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Kuhusiana na Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wao wanawatakia radhi Maswahabah wote (Radhiya Allaahu ´anhum), wanaamini kuwa wote ni waadilifu na kwamba wao ndio viumbe bora wa Allaah baada ya Mitume (´alayhimus-Swalatu was-Salam). Jengine ni kwamba wanajitenga mbali na mwenendo wa Rawaafidhwah ambao wamepetuka mipaka kwa ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) na watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na (Radhiya Allaahu ´anhum). Ahl-us-Sunnah hawavuki mipaka na hawazembei.

Wao wako upande wa Maswahabah kwa kuwatakia radhi, wanaamini kuwa wao ndio viumbe bora baada ya Mitume na Manabii (´alayhimus-Swalatu was-Salam) na wanaamini kuwa wao ndio viumbe bora kabisa wa Ummah huu. Pamoja na yote haya hawavuki mipaka kwao kama walivyofanya Raafidhwah kwa ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) na watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) pale ambapo wanawaomba pamoja na Allaah na wanadai kuwa wamekingwa na kukosea. Yote haya si sahihi. Raafidhwah wamevuka mipaka na kupotea. Raafidhwah na wao wamezembea inapokuja katika haki ya Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) na hawakuthibitisha uadilifu wao.

Ahl-us-Sunnah wao wamethibitisha uadilifu wa Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) na fadhila zao na kwamba wao ndio viumbe bora baada ya Mitume (´alayhimus-Swalatu was-Salaam). Lakini hata hivyo wameenda kinyume na Raafidhwah katika kuchupa kwao mipaka. Hawakuvuka mipaka kwa ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) wala kwa watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Badala yake wanawatakia radhi, wanawaombea msamaha na wanaonelea mwenye kufuata haki miongoni mwa watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndiye mwema na wanatarajia mema kwake.

## 35. Msimamo wa Ahl-us-Sunnah kwa Ahl-ul-Bayt na ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh)

Aidha Ahl-us-Sunnah wanaonelea kuwa ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) ni kama Maswahabah wengine wote, kwamba yeye ni khaliyfah wa nne ana fadhila zake na kwamba yeye ni mmoja miongoni mwa wale Maswahabah kumi waliobashiriwa Pepo. Pamoja na yote haya hawapitilizi kwake, hawamuombi pamoja na Allaah, hawasemi kuwa amekingwa na kukosea na wala hawasemi kuwa yeye ndiye alikuwa ni mwenye kustahiki utume na kwamba Jibriyl (´alayhis-Salaam) alifanya usaliti. Yote haya ni batili. Lakini wanaona kuwa ni miongoni mwa Maswahabah wabora na wema (Radhiya Allaahu ´anhum). Pamoja na yote haya hawavuki mipaka kwao, hawavuki mipaka kwa Faatwimah (Radhiya Allaahu ´anhaa), al-Hasan na al-Husayn (Radhiya Allaahu ´anhumaa) na wengineo. Bali wanaonelea kuwa yule mwenye kufuata haki miongoni mwa watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndiye ambaye ana sifa za waumini, anastahiki kuombewa na kutakiwa radhi. Lakini hata hivyo hawavuki mipaka kwao. Wanazitambua fadhila zao, kwamba wao ndio waislamu bora kabisa na wana nafasi yenye kujulikana mbele ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.

## 36. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah kuhusu Ujuu wa Allaah

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Na katika yale tuliyotaja katika kumuamini Allaah, kunaingia kuamini yale Aliyoelezea Allaah katika Kitabu Chake, yaliyopokelewa kwa njia nyingi kutoka kwa Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na yale waliyokubaliana kwayo Salaf wa Ummah:*

*Ya kwamba Yeye (Subhaanah) Yuko juu ya mbingu Zake, juu ya ´Arshi yake na ametengana na viumbe Vyake. Na Yeye (Subhaanah) Yuko pamoja nao popote wanapokuwa na Anajua wanayoyafanya, kama Alivyojumuisha baina ya hayo katika Kauli Yake:*

هُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۚ يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنزِلُ مِنَ السَّمَاءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا ۖ وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنتُمْ ۚ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

*"Yeye Ndiye Aliyeumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha Akalingana juu ya ´Arshi. Anajua yanayoingia ardhini, na yatokayo humo, na yanayoteremka kutoka mbinguni, na yanayopanda humo - Naye Yu Pamoja nanyi popote mlipo. Na Allaah kwa myatendayo ni Mwenye kuyaona."* ***(57:04)***

*Na Kauli Yake "Naye Yu Pamoja nanyi popote mlipo" haina maana ya kwamba Amechanganyika na viumbe Vyake. Lugha haidharurishi hilo na linakwenda kinyume na yale waliyokubaliana kwayo Salaf wa Ummah na linakwenda kinyume na umbile Alililoliumbia kwalo uumbaji. Mwezi ni Ishara katika Ishara za Allaah na ni katika Kiumbe Chake kidogo. Uko mbinguni daima na unakuwa pamoja na msafiri na asiyekuwa msafiri popote anapokuwa.*

*Na Yeye (Subhaanah) Yuko juu ya ´Arshi. Anaona viumbe Vyake, Anawalinda, Ana ujuzi juu yavyo na yasiyokuwa hayo katika maana ya Uola Wake. Maneno yote haya ambayo Allaah Ameyataja – ya kwamba Yuko juu ya ´Arshi na kwamba Yuko pamoja nasi – ni haki kwa uhakika wake na wala hayahitajii Tahriyf, lakini yanatakiwa kulindwa na misingi isiyokuwa na maana ya udanganyifu, kwa mfano kudhania ya kwamba udhahiri wa Kauli Yake* ***"Fiys-Salmaa"*** *(Mbinguni) maana yake kwamba Yuko mbinguni na*

*mbingu ima inambeba au iko juu Yake. Hili ni batili kwa Ijmaa´ ya wanachuoni na watu wa Imani. Hakika ya Allaah, Kursiy Yake imeenea mbingu na ardhi na Yeye Ndiye Anayezuilia mbingu na ardhi zisiondoke. Anazuia mbingu kwa Amri Yake Anafanya zisianguke kwenye ardhi isipokuwa kwa idhini Yake. Na ni katika Ishara Zake kusimama kwa mbingu na ardhi kwa Amri Yake:*

وَمِنْ آيَاتِهِ أَن تَقُومَ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ بِأَمْرِهِ

*"Na katika alama Zake, ni kwamba mbingu na ardhi zimesimama kwa amri Yake."* ***(30:25)***

**MAELEZO**

Huu ni mlango muhimu sana katika kitabu hichi. Unaenda sambamba na yale yaliyotangulia katika kitabu. Anasema (Rahimahu Allaah):

"Na katika yale tuliyotaja katika kumuamini Allaah, kuamini kuwa Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) yuko juu ya mbingu, juu ya ´Arshi na ametengana na viumbe Vyake."

Haya yamethibiti kwa dalili ya Qur-aan, Sunnah na maafikiano ya Salaf wa Ummah. Salaf wa Ummah wote (Rahimahumu Allaah) ni wenye kuamini kuwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) yuko juu ya mbingu zote na yuko juu ya ´Arshi na ametengana na viumbe Vyake.

**Ametengana na viumbe Vyake -** Maana yake ni kwamba hakuna kitu katika viumbe Vyake kilichoko kwenye dhati Yake na kadhalika hakuna kitu katika dhati Yake kilichoko kwenye viumbe Vyake. Ametengana nao. ´Abdullaah bin al-Mubaarak na wengineo wamesema:

"Tunamtambua Mola wetu ya kwamba yuko juu ya mbingu zote, juu ya ´Arshi Yake na ametengana na viumbe Vyake. Lakini elimu Yake iko kila mahali."[35]

Kadhalika ndivyo wanavyosema Salaf wengine wote (Rahimahumu Allaah) ya kwamba Allaah (Subhaanah) yuko juu ya mbingu zote na juu ya ´Arshi na ujuzi

[35] Ameipokea ´Abdullaah bin Ahmad katika "as-Sunnah" (44), uk. 13, ad-Daarimiy katika "ar-Radd ´alaa al-Jahmiyyah" (67), uk. 47, Ibn Battwah katika "al-Ibaanah" (2528) (02/148).

Wake uko kila mahali. Hakuna mgongano kati ya ueneaji wa ujuzi Wake na kuwa Kwake juu. Hakika Yeye (Subhaanah) yuko juu ya ´Arshi na wakati huo huo ujuzi Wake uko kila mahali na umekizunguka kila kitu. Anakijua kila kitu. Ameoanisha hayo mawili katika maneno Yake (Subhaanah):

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۖ مَا يَكُونُ مِن نَّجْوَىٰ ثَلَاثَةٍ إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ وَلَا أَدْنَىٰ مِن ذَٰلِكَ وَلَا أَكْثَرَ إِلَّا هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا ۖ ثُمَّ يُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

**"Je, huoni kwamba Allaah Anajua yale yote yaliyomo mbinguni na yale yote yaliyomo ardhini? Hauwi mnong'ono wa [watu] watatu isipokuwa Yeye ni wa nne wao, na wala watano isipokuwa Yeye ni wa sita wao, na wala [hauwi mnong'ono wa] chini kuliko ya hivyo, na wala wa wengi zaidi isipokuwa Yeye Yu pamoja nao popote watakapokuwa; kisha Atawajulisha kwa yale [yote] waliyoyatenda Siku ya Qiyaamah - hakika Allaah kwa kila kitu ni Mjuzi daima." (58:07)**

Ameanza Aayah hii kwa kutaja ujuzi na akaimalizia kwa kutaja ujuzi. Hiyo ni dalili yenye kuonyesha kuwa ujuzi sio Ujuu. Ujuzi Wake ni wenye kukizunguka kila kitu na ni jambo limethibiti kwa dalili ya Qur-aan, Sunnah na maafikiano ya Salaf wa Ummah huu. Vilevile kuwa Kwake juu ya ´Arshi ni jambo limethibiti kwa dalili ya Qur-aan na Sunnah. Hakuna mgongano kati ya hayo mawili.

**Na Yeye (Subhaanah) Yuko juu ya ´Arshi. Anaona viumbe Vyake, Anawalinda... -** Inatakiwa kumtakasa na dhana mbovu kama mtu kufikiria kuwa mbingu inambeba, iko juu Yake au ni Mwenye haja nayo. Sivyo hivyo. Yeye ndiye ambaye amezisimamisha mbingu na ´Arshi. Amesema (Ta´ala):

إِنَّ اللَّهَ يُمْسِكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ أَن تَزُولَا

**"Hakika Allaah Anazuia mbingu na ardhi zisitoweke." (35:41)**

وَمِنْ آيَاتِهِ أَن تَقُومَ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ بِأَمْرِهِ

**"Na katika alama Zake ni kwamba: mbingu na ardhi zimesimama kwa amri Yake." (30:25)**

Viumbe vyote vimesimama kwa ajili Yake (Jalla wa ´Alaa). Yeye ndiye Mwenye kuvizuia, Yeye ndiye Mwenye kuviendesha na Yeye ndiye ameviumba. Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) yuko juu ya ´Arshi Yake na juu ya viumbe vyote.

**Maneno yote haya ambayo Allaah Ameyataja – ya kwamba Yuko juu ya ´Arshi... -** Kuhusu Yeye kuwa pamoja na sisi na kuwa Kwake juu ya ´Arshi ni haki juu ya uhakika wake. Ni jambo lisilohitajia kupotoshwa na wala isifikiriwe kuwa amechanganyika na viumbe Vyake kama wanavyosema Mu´tazilah, Jahmiyyah na mapote mengine yanayokanusha sifa za Allaah. Hakika (Subhaanah) yuko juu ya ´Arshi na ujuzi Wake uko kila mahali. Kwa msemo mwingine anakijua kila kitu kilicho mbinguni na ardhini.

Muumini anatakiwa kufuata ´Aqiydah hii kubwa iliyothibiti kwa Qur-aan na Sunnah. Hii ndio ´Aqiydah ambayo Salaf wa Ummah katika Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na waliokuja baada yao wamekubaliana kwayo ya kwamba kitendo cha Allaah kuwa juu hakipingani na kuwa kwake pamoja na viumbe Vyake (al-Ma´iyyah) na kuwazunguka Kwake kiujuzi. Ujuu ni kitu na kukizunguka Kwake kila kitu kiujuzu ni kitu kingine. Hakuna chochote chenye kumpita katika elimu Yake, si mbinguni wala ardhini pamoja na kuwa yuko juu ya ´Arshi na juu ya viumbe vyote (Subhaanahu wa Ta´ala):

لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

**"... ili mjue kwamba Allaah juu ya kila kitu ni Muweza na kwamba Allaah Amekwishakizunguka kila kitu kwa ujuzi Wake." (65:12)**

إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

**"Hakika Allaah kwa kila kitu ni Mjuzi." (08:75)**

إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**"Hakika Allaah juu ya kila kitu ni Muweza." (02:20)**

وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ مُّقْتَدِرًا

**"Na Allaah daima juu ya kila kitu ni Mwenye Uwezo wa juu kabisa." (18:45)**

## 37. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya Qur-aan na kwamba haikuumbwa

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Katika hayo kunaingia vile vile kuamini ya kwamba Yuko karibu na viumbe Vyake na ni Mwenye Kuwajibu, kama Alivyojumuisha baina ya hayo katika Kauli Yake:*

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ

*"Na watakapokuuliza waja Wangu kuhusu Mimi, basi Mimi niko karibu na Naitikia maombi ya muombaji anaponiomba. Basi waniitikie Mimi na waniamini Mimi wapate kuongoka."* ***(02:186)***

*Na kauli yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuwaambia Maswahabah waliponyanyua sauti zao kwa Dhikr:*

*"Enyi watu! Zihurumieni nafsi zenu! Kwani hakika hamumuombi ambaye ni kiziwi wala asiyekuwepo. Hakika Yule mnayemwomba ni Mwenye Kusikia Mwenye kuona na Aliye karibu. Hakika yule mnayemwomba Yuko karibu na mmoja wenu kuliko shingo ya mpando wenu."*

*Na yaliyotajwa katika Kitabu na Sunnah kuhusu Ukaribu Wake na Kuwa Kwake pamoja, hayapingani na yaliyotajwa kuhusu kuwa Kwake juu ya viumbe, kwa kuwa Yeye (Subhaanah) hakuna kitu mfano Wake katika Sifa Zake zote. Naye Yuko juu kabisa kwa Ukaribu Wake na Yuko Karibu kwa Ukuu Wake.*

*Katika kumuamini Allaah na Vitabu Vyake kunaingia kuamini ya kuwa Qur-aan ni Maneno ya Allaah, imeteremshwa na haikuumbwa. Uteremsho wake umeanza kutoka Kwake na Kwake itarudi. Allaah Kaongea Kwayo Kauli ya kihakika. Qur-aan hii iliyoteremshwa kwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni Maneno ya Allaah ya kihakika na sio maneno ya mwengine. Na wala haijuzu kusema ya kwamba ni hikaaya au ibara ya Maneno ya Allaah, bali wanapoisoma watu au kuiandika kwenye misahafu, kwa kufanya hivyo haijatoka kuwa Maneno ya Allaah ya kihakika. Kwani hakika*

*Maneno yananasibishwa na yule aliyeyatamka mwanzo, na si kwa yule aliyeyawakilisha (kuyafikisha). Hivyo ni Maneno ya Allaah; herufi na maana yake. Maneno ya Allaah sio herufi bila ya maana na wala sio maana bila ya herufi.*

**MAELEZO**

**Katika hayo kunaingia vile vile kuamini ya kwamba Yuko karibu na viumbe Vyake... -** Mwandishi (Rahimahu Allaah) amebainisha kuwa kunaingia katika kumuamini Allaah, majina na sifa Zake kuamini pia ya kwamba Yeye yukaribu na ni mwenye kuitikia (Subhaanahu wa Ta´ala). Yeye yuko juu ya ´Arshi. Hili halipingani na kuwa Kwake karibu na mwenye kuitikia (Subhaanahu wa Ta´ala). Yeye yuko juu kabisa kwa Ukaribu Wake na yuko Karibu kwa Ukuu Wake kama alivyosema mwandishi. Yeye yukaribu na ni mwenye kuitikia na wakati huo huo yuko juu (Subhaanahu wa Ta´ala). Yuko juu ya ´Arshi, juu ya mbingu zote na juu ya viumbe vyote. Kwa jili hii amesema (Ta´ala):

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ

**"Na watakapokuuliza waja Wangu kuhusu Mimi, basi Mimi niko karibu na Naitikia maombi ya muombaji anaponiomba. Basi waniitikie Mimi na waniamini Mimi wapate kuongoka."(02:186)**

Hakika (Subhaanah) yuko karibu kwa mwenye kumuomba na ni Mwenye kuwaitikia waja Wake hekima Yake ikionelea kufanya hivyo. Maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Hakika yule mnayemwomba Yuko karibu na mmoja wenu kuliko shingo ya mpando wenu."

ilikuwa pale alipowasikia baadhi ya Maswahabah zake wananyanyua sauti zao safarini ndipo akawaambia:

"Hakika hamumuombi ambaye ni kiziwi wala asiyekuwepo. Hakika Yule mnayemwomba ni Mwenye Kusikia Mwenye kuona na Aliye karibu. Hakika yule mnayemwomba Yuko karibu na mmoja wenu kuliko shingo ya mpando wenu."

Katika upokezi mwingine imekuja:

"Hakika Yule mnayemwomba ni Mwenye Kusikia, Mwenye kuona na Yuko karibu. Hakika Yuko karibu na mmoja wenu kuliko shingo ya mpando wenu."

Pamoja na kuwa (Subhaabah) yuko juu ya ´Arshi halipingani kitu na kuwa Kwake karibu, Mwenye kutikia na anasikia du´aa ya mwenye kumuomba. Yeye ndiye Mwenye kusikia du´aa, yuko karibu kwa kuitikia ni Mwenye kusikia na kuitikia (Subhaanahu wa Ta´ala). Amekariri hilo katika Aayah nyingi ambapo amejisifu ya kwamba ni Mwenye kusikia, anazisikia siri na minong´onezo na hakuna kinachojifichika Kwake (Jalla wa ´Alaa). Vivyo hivyo katika Hadiyth. Yaliyotajwa kuhusu kuwepo Kwake juu hakupingani kitu na kuwepo Kwake karibu na pamoja na viumbe. Yeye yuko pamoja na waja Wake kwa ujuzi Wake na kuwaona:

وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنتُمْ

**"Naye Yu pamoja nanyi popote mlipo." (57:04)**

Vilevile yuko pamoja na mawalii Wake kwa ujuzi Wake, kuwahifadhi, kuwanusuru na kuwapa nguvu (Subhaanahu wa Ta´ala).

Ni wajibu kwa kila muumini mwanaume na mwanamke kuamini hilo na kwamba Yeye ni Mwenye kusikia na yuko karibu. Uwepo Wake (Jalla wa ´Alaa) juu ya ´Arshi haupingani kitu na kuwakaribia Kwake waja Wake na kuzisikia Kwake du´aa zao (Jalla wa ´Alaa). Yeye ni Mwenye kusikia na yukaribu na wakati huo huo yuko juu na ni Mkuu (Jalla wa ´Alaa). Amesema (Ta´ala):

وَلَا يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا ۚ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ

**"Wala hakumchoshi kuvihifadhi viwili hivyo. Na Yeye ndiye Aliye juu, na ndiye Mkuu." (02:255)**

إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ

**"Kwake Pekee linapanda neno zuri na amali njema Hukipa hadhi." (35:10)**

**Katika kumuamini Allaah na Vitabu Vyake kunaingia kuamini ya kuwa Qur-aan... -** Katika kumuamini Allaah ni pamoja vilevile na kuamini kuwa Qur-aan ni Maneno ya Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Katika kuamini Vitabu vya Allaah ni pamoja na kuamini vilevile kwamba Qur-aan ni Kitabu kilichoteremshwa kwa mja na Mtume Wake ambaye ndiye Nabii wa mwisho, Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Qur-aan ni maneno ya Allaah, sawa herufi na maana yake. Ni wajibu kuamini kuwa ni maneno ya Allaah na imeteremshwa haikuumbwa. Imeanza kutoka Kwake na Kwake itarudi. Pale inapoandikwa kwenye misahafu, inaposomwa na inapohifadhiwa haipingani na kuwa ni maneno ya Allaah. Imehifadhiwa kwenye vifua, imeandikwa kwenye misahafu na inasikiwa na masikio. Pamoja na haya yote bado ni maneno ya Allaah (´Azza wa Jall), sawa herufi na maana yake.

**Na wala haijuzu kusema ya kwamba ni hikaaya au ibara ya Maneno ya Allaah... -** Haijuzu kusema kuwa Qur-aan ni hikaaya au ni ibara ya maneno ya Allaah kama wanavyosema Ashaa´irah na Kullaabiyyah na wengineo. Qur-aan ni maneno ya Allaah herufi na maana yake na sio ibara wala hikaaya ya maneno ya Allaah. Ni maneno ya Allaah kwa dhati yake. Maneno Yake (Ta´ala):

اللَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ

**"Allaah, hakuna mungu wa haki ila Yeye - Aliyehai daima, Msimamizi wa kila kitu." (02:255)**

ni maneno ya Allaah.

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

**"Sifa njema na shukurani zote ni za Allaah, Mola wa walimwengu." (01:01)**

ni maneno ya Allaah.

وَلَا يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا

**"Wala hakumchoshi kuvihifadhi viwili hivyo." (02:255)**

ni maneno ya Allaah.

**Maneno ya Allaah sio herufi bila ya maana... -** Kila Aayah na kila neno yote hayo ni maneno ya Allaah, kuanzia mwanzo wake mpaka mwisho wake, sawa herufi na maana yake. Maneno ya Allaah sio harefi pasi na maana na wala sio maana pasi na herufi.

اللَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ

**"Allaah, hakuna mungu wa haki ila Yeye - Aliyehai daima, Msimamizi wa kila kitu." (02:255)**

Haya ni maneno ya Allaah.

Kadhalika maana yake kuhusiana na uhai, kuyasimamia Kwake mambo, kuyalinda na kuyahifadhi Kwake mambo yote haya ni maneno ya Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

قُلْ مَن يَكْلَؤُكُم بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ مِنَ الرَّحْمَٰنِ

**"Sema: "Nani [awezaye] kukulindeni usiku na mchana kutokana na [adhabu ya] Mwingi wa Rahmah?"" (21:42)**

إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ

**"Kwake Yeye linapanda neno zuri na kitendo chema hukinyanyua." (35:10)**

فَالْحُكْمُ لِلَّهِ الْعَلِيِّ الْكَبِيرِ

**"Basi [leo] hukumu ni ya Allaah Pekee, Aliye juu, Mkubwa kabisa." (40:12)**

إِنَّهُ سَمِيعٌ قَرِيبٌ

**"Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Yu karibu." (34:50)**

إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

**"Hakika Allaah ni Mwenye kusikia, Mjuzi." (02:181)**

وَأَنَّ اللَّهَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

**"Allaah ni Mwenye huruma mno, Mwenye kurehemu." (24:20)**

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaonelea kuwa yote haya, sawa herufi na maana yake, ni maneno ya Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

## 38. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya kuonekana Allaah Aakhirah

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Kunaingia vilevile katika yale tuliyoyataja kumuamini Allaah, Vitabu Vyake, Malaika Wake na Mitume Wake, ni pamoja na:*

*Kuamini ya kwamba waumini watamuona siku ya Qiyaamah kwa macho yao kama wanavyoona jua kwenye anga lililo wazi bila ya mawingu, na hali kadhalika kama wauonavyo mwezi usiku wa mwezi mng'aro – hawatosongamana katika kumuona. Watamuona (Subhaanah) nao watakuwa katika uwanja wa Qiyaamah na kisha watamuona baada ya kuingia Peponi kwa namna Atakayoipenda Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).*

*Katika kuamini Siku ya Aakhirah kunaingia:*

*Kuamini yote aliyoelezea Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) juu ya yatakayokuwa baada ya mauti. Wanaamini mitihani ya ndani ya kaburi, adhabu ya kaburi na neema zake. Ama mitihani yake, hakika watu watapewa mitihani kwenye makaburi yao. Kila mtu ataulizwa: "Ni nani Mola wako? Ni ipi dini yako? Na ni nani Mtume wako?*

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ

*"Allaah Huwathibitisha wale walioamini kwa kauli thabiti katika uhai wa dunia na Aakhirah."* ***(14:27)***

*Waumini watasema: "Allaah ndio Mola Wangu, Uislamu ndio Dini yangu na Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndio Mtume wangu." Ama wenye mashaka watasema: "Aah! Aah! Sijui. Nilisikia watu wanasema kitu na mimi nikakisema." Hivyo atapigwa chuma cha Moto na atapiga kelele ya juu kabisa ambayo itasikiwa na viumbe vyote isipokuwa binaadamu. Na lau binaadamu aingeliisikia, basi angelizimia.*

*Baada ya mtihani huu, kuna ima neema au adhabu mpaka kitaposimama Qiyaamah kikubwa. Roho zitarudishwa miilini. Qiyaamah ambacho Allaah (Ta´ala) Kaelezea katika*

*Kitabu Chake na kupitia ulimi wa Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wakakubaliana juu ya hilo Waislamu, kitasimama. Watu watatoka ndani ya makaburi yao, wakiwa peku, uchi, wasiotahiriwa, wasimame mbele ya Mola wa walimwengu. Jua litajongezwa karibu yao na jasho zao zitafikia vinywa vyao. Mizani itapima na yapimwe matendo ya waja.*

فَمَن ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَـٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ وَمَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَـٰئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ فِي جَهَنَّمَ خَالِدُونَ

*"Basi yule ambaye mizani yake itakuwa nzito, hao ndio wenye kufaulu. Na yule ambaye mizani yake itakuwa khafifu, basi hao ni wale ambao imekhasirika nafsi zao, [watakuwa] katika [Moto wa] Jahannam ni wenye kudumu."* ***(23:102-103)***

*Madaftari yataenezwa ambayo ndani yake kumeandikwa matendo. Kuna ambao watapewa madaftari yao kwa mkono wa kulia, na kuna ambao watapewa madaftari yao kwa mkono wa kushoto au nyuma ya mgongo wao, kama Alivyosema (Subhaanahu wa Ta´ala):*

وَكُلَّ إِنسَانٍ أَلْزَمْنَاهُ طَائِرَهُ فِي عُنُقِهِ ۖ وَنُخْرِجُ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ كِتَابًا يَلْقَاهُ مَنشُورًا اقْرَأْ كِتَابَكَ كَفَىٰ بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيبًا

*"Na kila mtu Tumemuambatanishia majaaliwa ya 'amali zake shingoni mwake. Na Tutamtolea Siku ya Qiyaamah kitabu atakachokikuta kimekunjuliwa. [Ataambiwa]: "Soma kitabu chako! Nafsi yako inakutosheleze leo kukuhesabia dhidi yako."* ***(17:13-14)***

*Allaah Atawafanyia hesabu viumbe na Atamhifadhi mja Wake muumini halafu atayakubali madhambi yake, kama ilivyokuja katika Kitabu na Sunnah. Kuhusu makafiri, hawatohesabiwa hesabu kwa njia hiyo hiyo ya matendo mema na mabaya kupimwa, kwa kuwa hawana mema yoyote. Badala yake matendo yao yatahesabiwa na watakuja kujua hilo, wayakubali na wawajibike nayo.*

## MAELEZO

Mlango huu unazungumzia juu ya waumini kumuona Mola Wao. Imetangulia kwa sura ya jumla ya kwamba waumini wanaamini yale yote aliyoelezea Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuhusu Pepo na Moto, Malaika, madaftari, mizani, kufanyiwa hesabu, malipo na mengineyo kuhusiana

na mambo ya Aakhirah. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaamini yote haya kwa njia ya ujumla.

**Kunaingia vilevile katika yale tuliyoyataja... -** Miongoni mwa hayo vilevile kunaingia kuamini ya kwamba waumini watamuona Mola Wao siku ya Qiyaamah. Haya ni miongoni mwa maelezo kuhusu siku ya Qiyaamah ya kwamba waumini watamuona Mola Wao siku ya Qiyaamah. Amesema (Rahimahu Allaah):

"... kwa macho yao."

Ina maana ya kwamba watamuona kwa macho yao wazi wazi pasi na kuwepo ugumu wala utata. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Hakika nyinyi mtamuona Mola Wenu kama mnavyouona mwezi usiku wa mwezi mng'aro – hamtosongamana katika kumuona. Vilevile kama mnavyoona jua wazi pasina kuwepo mawingu."

## *Makafiri watazuiwa na kumuona Allaah*

Kuhusu makafiri hawatomuona. Bali watazuiawa. Amesema (Subhaanah):

كَلَّا إِنَّهُمْ عَن رَّبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّمَحْجُوبُونَ

**"Hapana! Hakika wao siku hiyo watawekewa kizuizi [wasimuone] Mola wao." (83:15)**

Bi maana siku ya Qiyaamah.

Kuhusu waumini watamuona mara mbili:

**Mosi:** Watamuona kwenye uwanja muono ambao utakuwa ni maalum kwao pasi na wengineo wataokuwa wamesimama uwanjani.

**Pili:** Watamuona namna anavyotaka (Subhaanahu wa Ta´ala) Peponi katika nyakati ambazo atawaondoshea pazia ya Uso Wake mtukufu. Peponi watakuwa na nyakati maalum ambazo wanamuona. Kila mmoja atamuona katika nyakati mbali mbali kutegemea na nafasi alionayo.

**Katika kuamini Siku ya Aakhirah kunaingia... -** Miongoni mwa misingi ya Ahl-us-Sunnah vilevile ni kuamini yale yote aliyoelezea Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ikiwa ni pamoja vilevile na mambo ya Aakhirah, Pepo, Moto, kufanyiwa hesabu na malipo. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanaamini yote haya.

Kadhalika inatakiwa kuamini adhabu na neema ya kaburi. Ahl-us-Sunnah wanaamini hayo. Tofauti na Ahl-ul-Bid´ah. Ahl-us-Sunnah wanaamini adhabu na neema ya kaburi, kwamba watu watahojiwa ndani ya makaburi yao ambapo wataulizwa juu ya Mola, dini na Mtume Wao. Allaah huwathibitisha wale walioamini kwa kauli thabiti duniani na Aakhirah na madhalimu huwadhalilisha. Amesema (Subhaanah):

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ۖ وَيُضِلُّ اللَّهُ الظَّالِمِينَ ۚ وَيَفْعَلُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ

**"Allaah Huwathibitisha wale walioamini kwa kauli thabiti katika uhai wa dunia na Aakhirah na Allaah Huwaacha kupotoka madhalimu. Na Allaah Anafanya Atakavyo." (14:27)**

Muumini yeye atajibu kwa kusema kwamba Mola Wake ni Allaah, Uislamu ndio dini yake na Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndio Mtume Wake.

Ama yule mwenye shaka na kafiri watasema kuwa hawajui. Hili linahusu mnafiki na kafiri. Huyu ni yule mnafiki ambaye alikuwa akidhihirisha Uislamu ilihali ni kafiri na kafiri wa wazi. Hawa ndio ambao watajibu kusema kuwa hawajui na kwamba walikuwa wakiwasikia watu wakisema kitu na wao wanasema. Atapigwa chuma cha moto na ukelele mkubwa ambao utasikia kila kiumbe isipokuwa mwanaadamu. Lau mwanaadamu angelisikia ukelele huo basi angelizimia.

**Baada ya mtihani huu, kuna ima neema au adhabu mpaka kitaposimama Qiyaamah kikubwa... -** Baada ya hapo ndipo kutasimama Qiyaamah kikubwa. Haya yatatokea baada ya mtihani [wa ndani ya kaburi ambapo] mwanaadamu huwa ima katika neema au adhabu. Muumini anakuwa katika neema ambapo roho yake inawekwa Peponi. Kafiri roho yake inawekwa Motoni. Amesema (Subhaanah) kuhusu watu wa Fir´awn walioko Motoni:

النَّارُ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَعَشِيًّا ۖ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ الْعَذَابِ

**"Wanadhihirishiwa Moto asubuhi na jioni na Siku itakayosimama Qiyaamah [itasemwa]: "Waingizeni watu wa Fir'awn katika adhabu kali kabisa." (40:46)**

Hapa ndipo kitakuwa kimesimama Qiyaamah kikubwa na watu watoke ndani ya makaburi yao peku, uchi na bila ya kutahiriwa. Allaah atawafufua hali ya kuwa amewarudishia miili yao. Watakuwa kama walivyoumbwa mara ya kwanza:

**Peku -** Bi maana pasi na viatu.

**Uchi -** Bi manaa hawatokuwa na mavazi.

**Wasiotahiriwa -** Bi maana watakuwa hawakutahiriwa.

Watasimama kwenda kwa Mola wa walimwengu na Allaah (Jalla wa ´Alaa) atawafanyia hesabu viumbe. Mizani itawekwa na matendo ya waja yapimwe. Yule ambaye mizani yake itakuwa na uzito huyo ndiye mwenye furaha. Ama yule ambaye mizani yake itakuwa khafifu huyo ndiye mwangamivu.

**Madaftari yataenezwa ambayo ndani yake kumeandikwa matendo... -** Madaftari yatagawanywa na kusambazwa kati yao. Kuko ambao watapokea madaftari yao kwa mikono ya kulia na wengine watapokea madaftari yao kwa mikono ya kushoto au nyuma ya migongo yao, kama ilivyobainishwa katika Qur-aan.

**Kuhusu makafiri, hawatohesabiwa hesabu...** - Kuhusiana na makafiri hawatofanyiwa hesabu kwa njia ya mema na maovu yao kupimwa. Kwa sababu makafiri hawana mema yoyote. Lakini hata hivyo yatadhibitiwa matendo yao, wayakubali na halafu walipwe kwayo. Kwa msemo mwingine watatupwa Motoni. Matendo yao yatadhibitiwa, wayakubali na wayakiri. Baada ya hapo watupwe Motoni. Amesema (Ta´ala):

وَسِيقَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ جَهَنَّمَ زُمَرًا

**"Na wataendeshwa wale waliokufuru kuelekea [Moto wa] Jahannam makundi-makundi." (39:71)**

Itakuwa ni kundi baada ya kundi. Haya ni kutokamana na matendo yao machafu na kumkufuru kwao Allaah (´Azza wa Jall).

Ama watu wa Peponi wataingizwa Peponi kukirimiwa kikundi baada ya kutoka kwenye kiwanja cha hesabu na baada ya kupita juu ya Njia na kupitia kisimamo kirefu watachosimamishwa. Hapo ndipo sasa wataingizwa Peponi kwa kila mmoja kuwekwa nafasi yake stahiki. Yeye atakuwa anaijua nafasi yake kutokea duniani. Hivyo wataziendea nafasi zao ambazo Allaah amewaandalia baada ya kupitia hatua kadhaa zitatajwa huko mbeleni Allaah akitaka.

Tunachotaka kusema ni kwamba haya ndio mambo ya siku ya Qiyaamah. Ni siku nzito. Siku moja ni sawa na miaka elfu khamsini. Itakuwa ni siku nzito kwa makafiri na nyepesi kwa waumini. Amesema (Ta´ala):

أَصْحَابُ الْجَنَّةِ يَوْمَئِذٍ خَيْرٌ مُّسْتَقَرًّا وَأَحْسَنُ مَقِيلًا

**"Watu wa Jannah Siku hiyo wako katika makazi bora ya kutulia na mahali pazuri kabisa pa kupumzikia." (25:24)**

Watu wa Peponi watakuwa sehemu zao za starehe Peponi na watu wa Motoni watakuwa sehemu zao Motoni.

Hesabu itafanywa na Mola Wako (Jalla wa ´Alaa), ambaye ni al-Hakiym na al-´Adl (Mwenye hekima na Mwadilifu), hadhulumu punje hata kidogo. Amesema (Subhaanah):

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۖ وَإِن تَكُ حَسَنَةً يُضَاعِفْهَا وَيُؤْتِ مِن لَّدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا

**"Hakika Allaah Hadhulumu uzito wa atomu. Na ikiwa ni [‘amali] nzuri Huizidisha na Hutoa kutoka Kwake ujira mkuu." (04:40)**

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا ۖ وَإِن كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ خَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا ۗ وَكَفَىٰ بِنَا حَاسِبِينَ

**"Na Tutaweka mizani za uadilifu Siku ya Qiyaamah; basi haitodhulumiwa nafsi yoyote ile kitu chochote kile. Na japokuwa ni uzito wa mbegu ya hardali, Tutaileta. Na inatosheleza Kwetu kuwa Wenye kuhesabu." (21:47)**

فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ

**"Basi yule atakayetenda kheri [hata kama ni] uzito wa chembe ya atomu basi ataiona, na yule atakayetenda shari uzito wa chembe ya atomu basi ataiona." (99:07:08)**

Mtu akitoa swadaqah ya pesa moja, tonge moja au tende moja kumpa fakiri inakuwa atomu nyingi na kuwa na uzito mkubwa. Vipi kwa mwenye kutoa mapesa na mapesa na chakula kingi? Bila shaka atalipwa kwayo endapo atakuwa ni mwenye kumtakasia ´ibaadah yake Allaah:

فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ

**"Basi yule atakayetenda kheri [hata kama ni] uzito wa chembe ya atomu basi ataiona, na yule atakayetenda shari uzito wa chembe ya atomu basi ataiona." (99:07:08)**

Imepokelewa vilevile kutoka kwa Ibn ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) ya kwamba alitoa swadaqah ya punje ya zabibu ambapo akaulizwa uzito wake. Akasema:

"Punje hii itakuwa na uzito wa atomu kiasi gani."[36]

Ninacholenga ni kwamba mtu asidharau swadaqah hata kama itakuwa kidogo. Muhimu atoe kiasi na uwezo wake. Atoe pesa moja, pesa mbili, tonge ya chakula ampe mwombaji, tende moja, tende mbili na kadhalika.

Nimeshatangulia kukuelezeni kisa hichi zaidi ya mara moja ya kwamba kuna mwanamke alikuja kwenye nyumba ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuomba akiwa na watoto wawili wakike. ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) anasema kuwa hawakupata nyumbani isipokuwa tende tatu peke yake. Akachukua zile tende tatu na kumpa yule mwombaji. Yule mwanamke akampa kila msichana tende moja na ile ya tatu akaichukua ili aile yeye. Lakini hata hivyo na ile tende ya tatu akawa amewagawia nayo wale watoto wakike wawili

[36] Ni kutoka kwa ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) na sio Ibn ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anh). Ameipokea Ibn ´Abdil-Barr katika "al-Mustadrak" (1881) (08/602).

na yeye hakula kitu. ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) anaelezea kuwa kitendo kile kikamfurahisha. Pindi alipokuja Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) nikamweleza ambapo akasema:

"Hakika Allaah (Subhaanah) amemuwajibishia [mwanamke huyo] Pepo."[37]

Hili ni kutokana na huruma huu aliokuwa nao juu ya wasichana wake na akawagawia tende zote na yeye hakula kitu. Hii ni dalili yenye kuonyesha kuwa kutoa swadaqah, hata kama itakuwa kwa kitu kidogo, ilimradi mtu ameitoa kwa nia nzuri, ndani yake ina kheri nyingi.

Kilicho muhimu ni mtu atoe swadaqah kwa kile kitachowezekana. Mwenye uwezo wa pesa mia moja, elfu moja, pesa moja, tende moja, tonge ya chakula, nguo na mfano wa haya mtu atoe swadaqah.

فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ

**"Basi mcheni Allaah muwezavyo." (64:16)**

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا ۖ وَإِن كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ خَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا ۗ وَكَفَىٰ بِنَا حَاسِبِينَ

**"Na Tutaweka mizani za uadilifu Siku ya Qiyaamah; basi haitodhulumiwa nafsi yoyote ile kitu chochote kile. Na japokuwa ni uzito wa mbegu ya hardali, Tutaileta. Na inatosheleza Kwetu kuwa Wenye kuhesabu." (21:47)**

[37] Muslim (2630) na al-Bukhaariy (1418).

## 39. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya Hodhi na Njia

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Katika kiwanja cha Qiyaamah kutakuwa hodhi iliyotajwa ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Maji yake ni meupe kuliko maziwa na matamu kuliko asali. Vikombe vyake ni wingi wa idadi ya nyota mbinguni na urefu na upana wake ni sawa na mwendo wa mwezi. Anayekunywa humo mara moja, hatopata kiu baada yake kamwe.*

*Njia imewekwa juu ya Jahannam na ni daraja iliyo baina ya Pepo na Moto. Watu watapita juu yake kadiri ya matendo yao. Kuna ambao watapita kama kufumba na kufumbua, wengine kama umeme, wengine kama upepo, wengine kama mpanda farasi, wengine kama mwenye kusafiri kwa ngamia, wengine kama mkimbiaji, wengine kama watembeaji, wengine kama mtambaaji na wengine watashikwa na kutupwa Motoni. Yule atakayevuka Njia ataingia Peponi. Watapoivuka watasimama kwenye daraja baina ya Pepo na Moto na kulipizana kisasi wao kwa wao. Baada ya kusafishwa, watapewa idhini ya kuingia Peponi.*

**MAELEZO**

**Katika kiwanja cha Qiyaamah kutakuwa hodhi... -** Huu ni utafiti wenye kuzungumzia kuhusu Hodhi na Njia. Hodhi hii itakuwa ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ndio ile inayoitwa al-Kawthar:

إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ

**"Hakika Sisi Tumekupa [mto wa] al-Kawthar." (108:01)**

al-Kawthar ni mto uliopo Peponi. Hodhi hii ina mifereji miwili ya al-Kawthar. Hodhi hii iko duniani ardhini. Ni Hodhi itaendewa na waumini ambao ni wafuasi wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Urefu na upana wake ni mwezi. Vikombe vyake ni sawa na idadi ya nyota mbinguni. Maji yake ni meupe sana kushinda maziwa na ladha yake ni matamu zaidi kushinda asali. Mwenye kunywa humo basi hatohisi kiu kamwe mpaka pale atapoingia Peponi. Waumini wataufikia na kunywa ndani yake. Hili linahusiana na wale wafuasi wa

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kuna watu ambao watafukuzwa. Kisha ataulizwa Mola ambapo atasema:

"Hakika hawa walibaki ni wenye kuritadi tangu ulipofarakana nao."

Kwa hivyo watazuia kuifikia. Baada ya hapo aseme (´alayhis-Swalaatu was-Salaam):

"Atokomee! Atokomee yule aliyebadilisha baada yangu!"[38]

Hii ni dalili yenye kuonyesha kuwa Hodhi hii itaendewa tu na waumini ambao wamekufa na hali ya kuwa wanamfuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wanafuata dini yake.

Kuhusu walioritadi baada ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) au wakati mwingine wowote hawa hawatoifikia Hodhi hii. Vilevile inahusiana na makafiri wengine wote hawatoweza kuifikia Hodhi hii. Wataifikia tu waumini miongoni mwa wafuasi wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Mitume wengine (´alayhimus-Swalaatu was-Salaam) nao pia watakuwa na Hodhi zao[39]. Lakini hata hivyo Hodhi yake yeye (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndio kamilifu na yenye kutimia zaidi. Watafukuzwa kwenye Hodhi yake wasiokuwa katika kizazi chake kama inavyofukuzwa ngamia geni. Hakuna watayoifikia isipokuwa tu wale waumini ambao ni wakweli. Ama walioritadi hawana fungu kwayo. Hakuna nguvu wala uwezo isipokuwa kwa Allaah. Tunamuomba Allaah sote atujaalie kuwa miongoni mwa wataoifikia.

**Njia imewekwa juu ya Jahannam... -** Njia itawekwa juu ya Moto wa Jahannam. Atayeanguka kwenye Njia hii anatumbukia Motoni. Njia hii itapitiwa juu yake na kila mwenye kuingia Peponi. Amesema (Ta´ala):

وَإِن مِّنكُمْ إِلَّا وَارِدُهَا ۚ كَانَ عَلَىٰ رَبِّكَ حَتْمًا مَّقْضِيًّا ثُمَّ نُنَجِّي الَّذِينَ اتَّقَوا وَّنَذَرُ الظَّالِمِينَ فِيهَا جِثِيًّا

[38] al-Bukhaariy (4625) na Muslim (2860)

[39] at-Tirmidhiy (2443). Ni nzuri kwa mujibu wa Imaam al-Albaaniy katika "as-Swahiyh" (1589).

**"Na hakuna yeyote miongoni mwenu isipokuwa ataufikia. Hiyo kwa Mola wako ni hukumu ya lazima kutimizwa. Kisha Tutawaokoa wale waliokuwa na taqwa na Tutawaacha madhalimu humo wamepiga magoti." (19:71-72)**

Waumini watapita na kuokoka. Wasiokuwa waumini hawatopita. Kinyume chake wataanguka Motoni.

**Kuna ambao watapita kama kufumba na kufumbua... -** Wale wataopita juu ya Njia hii kuna waumini ambao watapita kama kufumba na kufumbua. Wengine watapita kama umeme, wengine kama mpanda farasi, wengine kama upepo na wengine kama ngamia. Kila mmoja atapita juu yake kutegemea na vile matendo yake yalivyo. Vilevile kuna wengine watapita kwa kujikongoja; mara amesimama na wakati mwingine anajikwaa. Kuna wengine watapita na kutumbukizwa Motoni. Kila mmoja atapita kutegemea na matendo aliokuwa juu yake. Waumini wakweli tu ndio wataokoka. Waliosalia watatupwa Motoni. Kuna ambao utawaonja kidogo lakini hatimaye watasalimika. Kuna wengine watatumbukia humo na kuadhibiwa kwa kiwango cha madhambi yao na halafu baadaye Allaah awatoe Motoni na kuwaingiza Motoni. Hakuna atayedumishwa Motoni milele isipokuwa makafiri peke yao.

Kuhusiana na waislamu watenda madhambi wataotumbukia humo wataadhibiwa kwa muda fulani kila mmoja kwa kiasi cha madhambi yake. Kisha Allaah atawapa idhini waombezi wawaombee. Miongoni mwa watu hao ni Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambaye atawaombea halafu watolewe Motoni. Ataombea nyombezi nne. Kila uombezi Allaah atampa idadi ya watu maalum ambao watatolewa Motoni. Baada ya hapo Motoni kutabaki watu katika Ummah huu ambao hawakupata uombezi wowote. Pamoja na hivyo Allaah atawatoa humo kutokana na fadhila na huruma Wake (Subhaanahu wa Ta´ala). Atawatoa Motoni na kuwaingiza Peponi. Watawekwa kwenye mto wa uhai. Mto huo unaitwa "mto wa uhai". Wakiwekwa humo watachipuka kama inavyochipuka punje kwenye kijiwavu cha kokwa. Umbile lao likitimia ndipo wataidhinishwa sasa kuingia Peponi.

## *Uwajibu wa kujibidisha na njia za salama na uokovu*

Kwa haya muumini anapata kujua kuwa ni wajibu kwake kupupia juu ya kutafuta sababu za usalama na kwamba hili ni khatari kubwa, sawa yanayohusu Hodhi na Njia. Ni wajibu kwake kumuomba Allaah mwisho mwema. Vilevile ajitahidi kuwa na uthabiti katika haki na awe na msimamo juu yake. Sambamba na hilo atahadhari na kumuasi Allaah (´Azza wa Jall) na akimbilie kutubia. Kila mwenye kutekeleza akimbilie kutubu. Hakuna yeyote aliyekingwa na kukosea. Lakini pamoja na hivyo ni lazima kuleta tawbah. Kila atapofanya mapungufu au dhambi akimbilie kufanya tawbah.

وَالَّذِينَ إِذَا فَعَلُوا فَاحِشَةً أَوْ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ ذَكَرُوا اللَّهَ فَاسْتَغْفَرُوا لِذُنُوبِهِمْ وَمَن يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا اللَّهُ وَلَمْ يُصِرُّوا عَلَىٰ مَا فَعَلُوا وَهُمْ يَعْلَمُونَ أُولَٰئِكَ جَزَاؤُهُم مَّغْفِرَةٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَجَنَّاتٌ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ وَنِعْمَ أَجْرُ الْعَامِلِينَ

**"Na wale ambao wanapofanya machafu au wakajidhulumu nafsi zao, humdhukuru Allaah wakaomba msamaha kwa madhambi yao. Na nani anayesamehe madhambi isipokuwa Allaah. Na hawaendelei katika waliyoyafanya na wao wanajua. Hao jazaa yao ni msamaha kutoka kwa Mola wao na Pepo zipitazo chini yake mito - ni wenye kudumu humo. Uzuri ulioje ujira wa watendaji wema!" (03:135-136)**

Muumini anatakiwa kuihesabu nafsi yake siku zote, aichunge na kuipeleleza. Matendo yasimtie jeuri na kumfanya akajiaminisha. Badala yake anatakiwa kuihesabu nafsi yake na kupambana nayo. Huenda kwa kufanya hayo akasalimika.

وَالَّذِينَ يُؤْتُونَ مَا آتَوا وَّقُلُوبُهُمْ وَجِلَةٌ أَنَّهُمْ إِلَىٰ رَبِّهِمْ رَاجِعُونَ أُولَٰئِكَ يُسَارِعُونَ فِي الْخَيْرَاتِ وَهُمْ لَهَا سَابِقُونَ

**"Na ambao wanatoa vile walivyopewa na huku nyoyo zao zinakhofu kwamba hakika kwa Mola wao ni wenye kurejea. Hao wanakimbilia katika kufanya kheri nyingi; nao wao katika hayo watawatangulia [wengine]." (23:60-61)**

Ibn Abiy Mulaykah amesema:

"Nilikutana na Maswahabah thelathini wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambao wote walikuwa wanachelea unafiki juu ya nafsi zao. Hakukuwa

miongoni mwao mwenye kusema kwamba ana imani kama ya Jibriyl na Mikaaiyl."[40]

Ibraahiym bin Yaziyd at-Taymiymiy amesema:

"Sikufanya kitendo chochote isipokuwa nilichelea nisije kuwa mwongo."[41]

Lililo wajibu ni kuhadhari na mtu asijiamini na kujiona kutokana na matendo. Hakika Allaah anakubali tu kutoka kwa wachaji Allaah. Mtu apambane na nafsi yake. Atambue mapungufu na kasoro zake ili aweze kujitahidi, aijue haki na alazimiane na tawbah mpaka pale atapokutana na Mola Wake.

[40] Ameipokea al-Bukhaariy na kuiwekea taaliki (47-48)

[41] Ameipokea al-Bukhaariy na kuiwekea taaliki (47-48)

## 40. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya maombezi

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Mtu wa kwanza ambaye atafunguliwa mlango wa Pepo ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na watu wa kwanza ambao wataingia Peponi ni Ummah wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).*

*Atakuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) siku ya Qiyaamah na nyombezi tatu. Ama uombezi wa kwanza atawaombea waliosimamishwa na kusubiri wahukumiwe baada ya Aadam, Nuuh, Ibraahiym, Muusa na ´Iysa bin Maryam kutoa udhuru wa kuombea, mpaka itaishia kwake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ama uombezi wa pili atawaombea watu wa Peponi waingie Peponi – na nyombezi hizi mbili ni maalum kwake. Ama uombezi wa tatu atawaombea wale waliostahiki kuingia Motoni. Na uombezi huu ni kwake na kwa Mitume wengine, wakweli na wengineo. Atawaombea wale waliostahiki kuingia Motoni wasiingizwe na awaombee wale walioingia watolewe humo. Allaah (Ta´ala) Atawatoa ndani ya Moto watu si kwa sababu ya uombezi, bali ni kwa sababu ya fadhila na huruma Wake. Kutabaki Peponi nafasi baada ya watu walioingia na Allaah Ataumba watu maalum kwa ajili yake kisha Awaingize Peponi. Hatua hizi mbali mbali zinazokuja kuhusu Nyumba ya ´Aakhirah, hesabu na thawabu, Pepo na Moto.*

*Ufafanuzi zaidi wa hilo umetajwa katika Vitabu vilivyoteremshwa kutoka mbinguni na Aathaar ya elimu iliyopokelewa kutoka kwa Mitume. Na katika elimu iliyorithiwa kutoka kwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), katika hayo kuna yanayokinaisha na kutosheleza, yule mwenye kutafuta atapata.*

**MAELEZO**

Mwandishi (Rahimahu Allaah) anasema:

Mtu wa kwanza ambaye atafunguliwa mlango wa Pepo ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)."

Ndiye Mtume wetu (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Allaah (Jalla wa ´Alaa) ameamrisha asifunguliwe yeyote kabla yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Yeye ndiye mtu wa kwanza atayefunguliwa mlango wake na kubisha hodi. Mlinzi wa Pepo atamwambia kwamba niliamrishwa nisimfungulie yeyote kabla yako (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

**Mtu wa kwanza ambaye atafunguliwa mlango wa Pepo ni Muhammad... -** Ummah wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndio utakuwa wa kwanza kuingia Peponi. Baada ya Mitume Ummah bora ni wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ummah wa kwanza miongoni mwa nyumati utaoingia Peponi na ulio bora baada ya Mitume (´alayhimus-Swalaatu was-Salaam) ni Ummah wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

## *Nyombezi tatu za Mtume (´alayis-Salaam)*

**Atakuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) siku ya Qiyaamah na nyombezi tatu... -** Yeye (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) atakuwa na nyombezi tatu:

**Mosi:** Uombezi mkubwa juu ya wataokuwa wamesimamishwa uwanjani ili wahukumiwe na kufanyiwa hesabu. Haya yatakuwa baada ya Mitume wengine kuomba udhuru; Aadam, Nuuh, Ibraahiym, Muusa na ´Iysaa mwana wa Maryam. Pindi kisimamo kitakuwa kizito kwa watu watamwendea Aadam (´alayhis-Swalaatu was-Salaam). Watasema kumwambia:

"Ee Aadam! Hakika wewe ndiye kiumbe cha kwanza. Allaah amekuumba kwa Mkono Wake, akakupulizia roho, Malaika wakakusujudia na akakufunza majina ya kila kitu. Hivyo tunakuomba utuombee kwa Mola Wako. Hivi kweli huoni tuliyomo? Hivi kweli huoni hali ilipofikia?"

Bi maana matatizo na magumu.

Aseme (´alayhis-Swalaatu was-Salaam):

"Mimi siistahiki. Hakika Mola Wangu ameghadhibika leo ghadhabu ambayo hajapatapo kughadhibika kabla yake na hatoghadhibika mfano wake baada ya leo."

Baada ya hapo atataja makosa yake ya kwamba alikula kwenye mti. Alitubu kwa kosa hili, lakini hata hivyo haya ni kutokana na unyenyekevu wa hali ya juu

walionao Mitume, khofu na imani yao kamilifu (´alayhimus-Swalaatu was-Salaam). Atawaambia:

"Nendeni kwa Nuuh."

Halafu wataenda kwa Nuuh (´alayhimis-Swalaatu was-Salaam) na kumwambia:

"Wewe ndiye Mtume wa kwanza uliyetumwa katika ardhi."

Bi maana Mtume wa kwanza baada ya kutokea shirki kati yao. Watamwambia:

"Hakika Allaah amekwita kuwa ni "mja mwenye kushukuru. Hivi kweli huoni hali tuliyomo? Tuombee kwa Mola Wako. Hakika Mola Wangu ameghadhibika leo ghadhabu ambayo hajapatapo kughadhibika kabla yake na hatoghadhibika mfano wake baada ya leo."

Atawaambia jinsi alivyoomba du´aa dhidi ya Ummah wake ambapo awaambie:

"Nendeni kwa Ibraahiym. Watapoenda kwa Ibraahiym awaambie vivyo hivyo. Hakika Mola Wangu ameghadhibika leo ghadhabu ambayo hajapatapo kughadhibika kabla yake na hatoghadhibika mfano wake baada ya leo." Awaambia jinsi alivyosema uongo mara tatu:

إِنِّي سَقِيمٌ

**"Hakika mimi ni mgonjwa." (37:89)**

بَلْ فَعَلَهُ كَبِيرُهُمْ هَـٰذَا

**"Bali amefanya hayo hili [sanamu] kubwa lao." (21:63)**

Halafu atawaambia waende kwa Muusa. Waende kwa Muusa (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) ambapo atawaambia vivyo hivyo. Hakika Mola Wangu ameghadhibika leo ghadhabu ambayo hajapatapo kughadhibika kabla yake na hatoghadhibika mfano wake baada ya leo. Mimi niliua nafsi ambayo sikuamrishwa kuiua. Hivyo nendeni kwa ´Iysaa (´alayhis-Swalaatu was-Salaam). Waende kwa ´Iysaa na kumwambia: "Tuombee kwa Mola Wako ambapo atawataka udhuru na kuwaambia kama walivyosema wa kabla yake. Hakika

Mola Wangu ameghadhibika leo ghadhabu ambayo hajapatapo kughadhibika kabla yake na hatoghadhibika mfano wake baada ya leo. Hivyo nendeni kwa Muhammad, kwani yeye ni mja ambaye amesamehewa madhambi aliyoyatanguliza na yaliyoko mbele. Wataenda kwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambapo atasema:

"Mimi ndiye mwenye kuistahiki. Mimi ndiye mwenye kuistahiki. Baada ya hapo aende kwa Mola  Wake asujudu chini ya  ´Arshi mbele ya Mola Wake. Amsifu kwa himdi kubwa ili Allaah amruhusu. Kisha baada ya hapo aambiwe:

"Ee Muhammad! Inua kichwa chako, sema utasikizwa, omba utapewa na shufaia utapewa uombezi. Halafu awaombee waliosimamishwa uwanjani ili wahukumiwe"."

**Pili:** Atawaombea watu wa Peponi ili waingizwe Peponi.

**Tatu:** Atawaombea watu walioingia Motoni kwa sababu ya madhambi na maasi yao baada ya Allaah kuwaadhibu awaondoshe Motoni. Atawaombea mara nne (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kila mara atapoombea watatolewa kundi la watu. Haya yametajwa katika "as-Swahiyh"[42].

**Ama uombezi wa tatu atawaombea wale waliostahiki kuingia Motoni... -** Mitume, waumini na watu wa kawaida na wao pia wataombea, kama alivyosema mwandishi. Ufafanuzi juu ya yatayopitika siku ya Qiyaamah ni mambo mazito.

**Allaah (Ta´ala) Atawatoa ndani ya Moto watu si kwa sababu ya uombezi... -** Watabaki Motoni baadhi ya wapwekeshaji ambao hawakupata uombezi. Hawa ni wale watenda madhambi waliokuwa wakimuabudu Allaah peke yake ambao wameingia Motoni kwa sababu ya madhambi yao. Hata hivyo Allaah (Jalla wa ´Alaa) atawatoa Motoni kwa fadhila na huruma Wake pasi na uombezi wa yeyote. Hawa ndio wataokuwa wamebaki Motoni na watakuwa wameungua na Moto. Baada ya hapo watawekwa kwenye mto wa uhai na wachipuke kama inavyochipuka punje kwenye kokwa lake. Litapotimia umbile lao Allaah atawaingiza Peponi kwa fadhila na huruma Wake (Subhnaanahu wa Ta´ala).

[42] al-Bukhaariy (6565) na Muslim (192).

Hakuna yeyote ambaye alikuwa anamuabudu Allaah peke yake ambaye atabaki Motoni. Wataobaki tu ni makafiri ambao Allaah amewafaradhishia kudumu humo milele. Amesema (Ta´ala):

كَذَٰلِكَ يُرِيهِمُ اللَّهُ أَعْمَالَهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ ۖ وَمَا هُم بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ

**"Hivyo ndivyo Allaah Atakavyowaonyesha 'amali zao kuwa ni majuto juu yao na wala hawatokuwa wenye kutoka Motoni." (02:167)**

كُلَّمَا خَبَتْ زِدْنَاهُمْ سَعِيرًا

**"Kila ukififia Tunawazidishia [Moto wa] *Sa'iyraa*." (17:97)**

فَذُوقُوا فَلَن نَّزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا

**"Basi onjeni [malipo yenu], kwani Hatutokuzidishieni chochote isipokuwa adhabu." (78:30)**

يُرِيدُونَ أَن يَخْرُجُوا مِنَ النَّارِ وَمَا هُم بِخَارِجِينَ مِنْهَا ۖ وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّقِيمٌ

**"Watataka kutoka katika Moto lakini wao si wenye kutoka kamwe humo, na watapata adhabu ya kudumu." (05:37)**

وَهُمْ يَصْطَرِخُونَ فِيهَا رَبَّنَا أَخْرِجْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ

**"Nao watapiga mayowe humo [watasema]: "Mola wetu! Tutoe tutende mema mbali na ya yale tulokuwa tukitenda... "**

Bi maana duniani. Allaah (´Azza wa Jall) awaambie:

أَوَلَمْ نُعَمِّرْكُم مَّا يَتَذَكَّرُ فِيهِ مَن تَذَكَّرَ وَجَاءَكُمُ النَّذِيرُ ۖ فَذُوقُوا فَمَا لِلظَّالِمِينَ مِن نَّصِيرٍ

**"Je, kwani Hatukukupeni umri wa kukumbuka mwenye kukumbuka humo? Na alikujieni mwonyaji. Basi onjeni [adhabu], kwani madhalimu hawana yeyote yule wa kuwanusuru." (35:37)**

Hii ndio itakuwa hali yao na mwisho wao. Ni adhabu kali - tunamuomba Allaah afya. Wataadhibiwa milele kwenye Moto usiokatika na hawatotolewa humo na ni Moto ambao hautozima.

**Ufafanuzi zaidi wa hilo umetajwa katika Vitabu vilivyoteremshwa... -** Kuhusiana na ufafanuzi juu ya siku ya Qiyaamah, mizani, hali za mizani na uzito wake, namna ambavyo madaftari pia yatapimwa na mengineyo yote haya yametajwa katika Qur-aan na katika Hadiyth ambazo ni Swahiyh. Mwenye kuyataka kwa kina anaweza kuyapata. Tunamuomba Allaah usalama. Hakuna uwezo wala nguvu isipokuwa kwa Allaah.

## 41. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya Qadar

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*al-Firqat-un-Naajiyah, Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, wanaamini Qadar kheri na shari yake.*

*Kuamini Qadar kumegawanyika katika daraja mbili na kila daraja ina mambo mawaili.*

*Daraja ya kwanza:*

*Kuamini ya kwamba Allaah (Ta´ala) Alijua kwa Elimu Yake ya milele – ambayo Anasifiwa kwayo milele na daima – ambayo viumbe watafanya, na Akajua hali zao zote kuhusiana na utiifu na maasi, riziki zao na umri wa maisha yao. Kisha Akayaandika Allaah katika Ubao uliohifadhiwa makadirio ya viumbe. Kitu cha kwanza Alichoumba Allaah ni kalamu. Akaiambia: "Andika!" Ikasema: "Niandike nini?" Akasema: "Andika yatayokuwepo mpaka siku ya Qiyaamah."[43]*

*Yaliyomfika mtu hayakuwa ni yakumkosa, na yaliyomkosa hayakuwa ni yakumsibu – [wino wa] kalamu umekauka na sahifu zimefungwa. Kama Alivyosema (Subhaanahu wa Ta´ala):*

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ فِي كِتَابٍ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

*"Je, huelewi kwamba Allaah Anajua yale yote yaliyomo katika mbingu na ardhi? Hakika hayo yamo katika Kitabu. Hakika hayo kwa Allaah ni sahali."* ***(22:70)***

*Na Akasema (Ta´ala):*

مَا أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن قَبْلِ أَن نَّبْرَأَهَا ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

*"Hakuna msiba wowote unaokusibuni katika ardhi au katika nafsi zenu isipokuwa umo katika Kitabu kabla Hatujaumba [huo msiba]. Hakika hayo kwa Allaah ni*

[43] Ahmad (5/317), Abuu Daawuud (4700), at-Tirmidhiy (2155) na (3319). Imaam al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) amesema kuwa ni Swahiyh katika kitabu cha Ibn Abiy ´Aaswim "Takhrij-us-Sunnah" (102-105).

*sahali.”* ***(57:22)***

*Makadirio haya yanafuata Elimu Yake (Subhaanah), yanakuja katika mahali kwa jumla na kwa ufafanuzi. Kaandika kwenye Ubao uliohifadhiwa Atakayo.*

*Baada ya Kuumba kipomoko, kabla ya kukipulizia roho, Hukitumia Malaika na huamrisha maneno mane. Huambiwa: “Andika riziki yake, umri wa maisha yake, matendo yake na kama atakuwa na maudhiko au mwenye furaha”. Makadirio haya walikuwa wakiyakanusha al-Ghulaat al-Qadariyyah mwanzoni na wanayakanusha (hata) leo japokuwa ni wachache.*

*Daraja ya pili:*

*Utashi wa Allaah (Ta´ala) unaoendelea na Uwezo Wake wa kina. Ina maana kuamini ya kwamba Atakayo Allaah, huwa, na Asiyotaka, hayawi. Yenye kufanya harakati na yaliotulia yalioko mbinguni na ardhini hayawi isipokuwa kwa Matakwa ya Allaah (Subhaanah). Hakukuwi katika Ufalme Wake kile Asichokitaka. Na Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) ni Muweza wa kila jambo, sawa yalioko na yasiokuwepo. Hakuna kimechoumbwa katika ardhi wala mbinguni isipokuwa, Allaah (Subhaanah) ndio Kakiumba. Hakuna Muumbaji mwengine badala Yake wala Mola asiyekuwa Yeye. Pamoja na hayo, Kawaamrisha waja kumtii Yeye na kuwatii Mitume Wake na Akakataza Kumuasi. Naye (Subhaanah) Anawapenda wachaji Allaah, wenye kufanya wema na waadilifu. Yuko radhi na wale walioamini na kufanya mema. Hawapendi makafiri na wala Hawaridhii wenye kufanya maasi. Na wala Haamrishi machafu. Haridhii kutoka kwa waja Wake kufuru na wala hapendi ufisadi. Na waja ndio wenye kutenda kihakika na Allaah ndio Ameumba matendo yao.*

*Muumini na kafiri, mchaji Allaah na mtena dhambi, mwenye kuswali na mwenye kufunga, wote hawa ni waja. Waja wana uwezo na matakwa katika kufanya kwao matendo yao. Allaah Amewaumba na Ameumba vilevile uwezo wao na matakwa yao. Kama Alivyosema (Ta´ala):*

لِمَن شَاءَ مِنكُمْ أَن يَسْتَقِيمَ وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

*”Kwa yule atakaye miongoni mwenu anyooke. Na hamtotaka isipokuwa Atakaye Allaah,*

*Mola wa walimwengu.”* ***(81:28-29)***

*Aina hii ya Qadar wanaikanusha al-Qadariyyah wote; ambao Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amewaita kuwa ni:*

*“Waabudu moto wa Ummah huu.”*[44]

*Na upande mwingine, katika wale wanaothibitisha Qadar, wamechupa mipaka kwa hilo, mpaka wakakanusha uwezo wa mja na utashi wake na wakamtoa [mja] katika Matendo ya Allaah na hukumu Yake iliyo juu ya hekima na ustawi Wake.*

MAELEZO

Utafiti huu ni miongoni mwa tafiti zenye faida zaidi na zenye kujumuisha. Ni tafiti yenye faida kubwa kuhusiana na Qadar. Mwandishi (Rahimahu Allaah) ameifanyia utafiti na kuiweka wazi kama alivyofanya hivyo pia Ibn-ul-Qayyim (Rahimahu Allaah) katika "Shifaa´ al-´Aliyl fiy Masaa-il al-Qadhwaa´ wal-Qadar wal-Hikmah wat-Ta´liyl". Mwandishi hapa amebainisha kuhusiana na Qadar ubainifu ambao ni wenye kutosheleza na mzuri kabisa.

**al-Firqat-un-Naajiyah, Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, wanaamini Qadar... -** Miongoni mwa misingi ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah na sifa za Firqat-un-Naajiyah ni pamoja vilevile na kuamini Qadar kheri na shari yake. Firqat-un-Naajiyah inaamini Qadar kheri na shari yake kwa sura zake zote.

**Kuamini Qadar kumegawanyika katika daraja mbili... -** Kuna daraja mbili za kuamini Qadar na kila daraja ina mambo mawili. Kuamini Qadar ndani yake kunahitajia mambo mane ambayo yanaitwa "daraja nne". Mwenye kuyakamilisha basi amekamilisha kuamini Qadar.

**Ngazi ya kwanza:** Ujuzi. Mtu aamini ya kwamba Allaah aliyajua mambo yote.

**Ngazi ya pili:** Uandishi.

**Ngazi ya tatu:** Utashi. Anayotaka Allaah huwa, na asiyotaka hayawi.

[44] Abuu Daawuud (4691) na al-Haakim (1/85). Imaam al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) kasema kuwa ni Hasan katika kitabu cha Ibn Abil-´Izz al-Hanafiy ”Sharh al-´Aqiydah at-Twahaawiyyah” (284).

**Ngazi ya nne:** Uumbaji. Mtu aamini ya kwamba Allaah ndiye Muumbaji wa kila kitu na kwamba Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) ndiye ameumba kila kitu. Hana mshirika katika kuumba na kuyaendesha mambo. Hizi ndio ngazi za Qadar. Ni ngazi nne. Mtu aamini ujuzi wa Allah juu ya mambo na kwamba ujuzi Wake umeyazunguka mambo yote. Amesema (Ta´ala):

إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

**"Hakika Allaah kwa kila kitu ni Mjuzi." (08:75)**

لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

**"... ili mjue kwamba Allaah juu ya kila kitu ni Muweza na kwamba Allaah Amekwishakizunguka kila kitu kwa ujuzi Wake." (65:12)**

Hii ni elimu ya milele. Kwa msemo mwingine hakuacha hata siku moja kusifika na elimu hii. Elimu yake haifichikani na chochote:

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُو مِنْهُ مِن قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ

**"Na hushughuliki katika jambo lolote na wala husomi humo chochote katika Qur-aan, na wala hamtendi ʻamali yoyote isipokuwa Tunakuwa Mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo." (10:61)**

Mambo yote yaliyopo duniani na Aakhirah ni yenye kujulikana Kwake. Hakuna kinachofichikana Kwake (Jalla wa ´Alaa).

Kadhalika mambo haya yameandikwa. Pamoja na kuwa aliyajua akayaandika vilevile. Amesema (Ta´ala):

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ فِي كِتَابٍ ۚإِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**"Je, hujui kwamba Allaah Anajua yale yote yaliyomo katika mbingu na ardhi? Hakika hayo yamo katika Kitabu. Hakika hayo kwa Allaah ni mepesi." (22:70)**

مَا أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن قَبْلِ أَن نَّبْرَأَهَا ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**"Hakuna msiba wowote unaokusibuni katika ardhi au katika nafsi zenu isipokuwa umeandikwa katika Kitabu kabla Hatujauumba [huo msiba]. Hakika hayo kwa Allaah ni mepesi." (57:22)**

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Allaah amekadiria makadirio ya viumbe kabla ya kuumba mbingu na ardhi kwa miaka elfu khamsini na ´Arshi Yake ilikuwa juu ya maji."

Ameandika kila kitu kwenye Ubao uliohifadhiwa.

Daraja ya kwanza ya Qadar ndani yake kunaingia ngazi mbili:

**a)** Ujuzi.

**b)** Uandishi.

Daraja ya pili ndani yake kunaingia mambo mawili:

**a)** Utashi.

**b)** Uumbaji.

Matakwa ya Allaah ni yenye kutekelezwa. Anayotaka Allaah huwa na asiyotaka hayawi. Yeye ndiye Muumbaji wa kila kitu (Jalla wa ´Alaa). Amesema (Ta´ala):

وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Na hamtotaka isipokuwa Atake Allaah, Mola wa walimwengu." (81:29)**

اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ

**"Allaah Ndiye Muumbaji wa kila kitu." (13:16)**

Hakika Yeye (Subhaanah) aliyajua mambo, akayaandika na akayaumba. Anayotaka Allaah huwa na asiyotaka hayawi.

**Na waja ndio wenye kutenda kihakika... -** Waja ni wenye kutenda kihakika. Matendo wanayofanya yananasibishwa kwao. Mja ni mwenye kuswali, mwenye kufunga, mwenye kuhiji, mwenye kuzini, mwenye kuiba, yeye ndiye mwenye kuuza na kununua, mwenye kuoa na kutaliki. Allaah (Subhaanah) ndiye amewaumba na akaumba vilevile matendo yao. Amesema (Ta´ala):

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ

**"Na hali Allaah Amekuumbeni na yale mnayoyatenda." (37:96)**

**Naye (Subhaanah) Anawapenda wachaji Allaah...** - Hakika Allaah (Subhaanah) anawapenda wachaji Allaah, watenda wema na waadilifu. Hawi radhi na watenda dhambi, hawapendi makafiri, haridhii juu ya waja wake kufuru na hapendi ufisadi. Anapenda kheri na watu wake, anachukizwa na shari na watu wake. Yeye anapenda imani na uchaji Allaah na wakati huo huo anachukia ufisadi, kufuru na upotevu. Kila mmoja ni mwenye kusahilishiwa kwa yale aliyoumbwa kwa ajili yake. Pindi Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) waliposikia hivi kwamba ikiwa mambo ni hivyo na matendo yao yameshaandikwa wakamuuliza Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) iko wapi basi haja ya kutenda? Akawaambia (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Tendeni! Hakika kila mmoja ni mwenye kuwepesishiwa kwa yale aliyoumbiwa kwa ajili yake. Wenye furaha watawepesishiwa kutenda mambo ya watu wenye furaha. Kuhusiana na waangamivu watawepesishiwa kutenda matendo ya waangamivu."[45]

**Makadirio haya walikuwa wakiyakanusha al-Ghulaat al-Qadariyyah... -** Hapo zamani Qadariyyah waliopindukia walikuwa wakipinga daraja ya kwanza ambayo ni elimu ya Allaah. Baada ya hapo wakajirejea kwa hilo. Leo wanaopinga hilo ni idadi ya watu wachache, kama ambavyo amesema mwandishi (Rahimahu Allaah). Hili ni kuhusiana na elimu ya Allaah juu ya kuyajua mambo na kuyaandika.

[45] al-Bukhaariy (4945) na Muslim (2647)

**Aina hii ya Qadar wanaikanusha al-Qadariyyah wote... -** Qadariyyah wengi wanapinga daraja ya pili ambayo inahusiana na Allaah kuyaumba mambo na kwamba matakwa Yake ni yenye kutekelezwa. Miongoni mwao ni Mu´tazilah na wengineo. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amewaita wao kuwa ni:

"Waabudu moto wa Ummah huu."

Waabudu moto ndio wenye kusema ya kwamba ulimwengu una waungu wawili:

**a)** Nuru. Huyu ndiye mwenye kuumba mambo mazuri.

**b)** Giza. Huyu ndiye mwenye kuumba mambo mabaya.

Kadhalika watu hawa ni miongoni mwa ambao wamewashirikisha viumbe katika matendo yao na kusema ya kwamba viumbe ndio wenye kuumba matendo yao na kwamba matendo wayafanyayo hayakukadiriwa kwao. Wanasema kuwa wao wenyewe ndio wenye kuyafanya na Allaah hakuyaumba. Haya ni kutokana na ujinga na upotevu wao. Miongoni mwao kunaingia pia Mu´tazilah na Qadariyyah wakanushaji. Kusema kwao hivi ina maana wamemkadhibisha Allaah na Mtume Wake. Kwa ajili hiyo wamekuwa makafiri.

**Na upande mwingine, katika wale wanaothibitisha Qadar, wamechupa mipaka... -** Miongoni mwa Qadariyyah kuna wenye kuitwa Jabriyyah. Humo kunaingia pia Jahmiyyah na wenye kufanana nao wenye kusema kwamba mja ni mwenye kutenzwa nguvu na hana uwezo wala khiyari ya kutenda. Bali ametenzwa nguvu. Watu hawa wamepotea. Nao ni Jahmiyyah wenye kukanusha sifa za Allaah. Wamekusanya kati ya kukanusha sifa za Allaah na imani ya kutenzwa nguvu ambapo wanaamini kuwa mja ametenzwa nguvu na hawezi kutenda kwa khiyari. Mapote yote haya yamepotea kuanzia Jahmiyyah, Mu´tazilah, Qadariyyah wakanushaji na Shiy´ah al-Imaamiyyah kwa sababu na wao ni Mu´tazilah wenye kukanusha Qadar.

**Makadirio haya yanafuata Elimu Yake (Subhaanah)... -** Qadar ina ufafanuzi. Kuna Qadar iliyotangulia ambapo kumekadiriwa mambo ikiwa ni pamoja na kipomoko tumboni mwa mama yake, makadirio yanayokuwa kwenye usiku wenye cheo, makadirio yaliyotokea pindi alipoumbwa Aadam na Allaah akagusa

kizazi chake kwenye mgongo wake. Haya ni makadirio ya ufafanuzi. Makadirio ya umri wa maisha, makadirio ya mwaka katika usiku wenye cheo na makadirio ya kila siku yote ni uufafanuzi wa Qadar iliyotangulia na yanarejea katika ile Qadar iliyotangulia. Kipomoko wala kiumbe kingine hakina namna ya kujitoa katika yaliyoandikwa kwenye Qadar iliyotangulia. Kwa ajili hii pindi Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) walipomuuliza Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ikiwa makazi yetu yamekwishajulikana ima Peponi au Motoni ni kwa nini basi tufanye matendo? Akawajibu kwa kuwaambia:

"Tendeni! Hakika kila mmoja ni mwenye kuwepesishiwa kwa yale aliyoumbiwa kwa ajili yake. Wenye furaha watawepesishiwa kutenda mambo ya watu wenye furaha. Kuhusiana na waangamivu watawepesishiwa kutenda matendo ya waangamivu." Halafu akasoma maneno Yake (Ta´ala):

إِنَّ سَعْيَكُمْ لَشَتَّىٰ فَأَمَّا مَنْ أَعْطَىٰ وَاتَّقَىٰ وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَىٰ فَسَنُيَسِّرُهُ لِلْيُسْرَىٰ وَأَمَّا مَن بَخِلَ وَاسْتَغْنَىٰ وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَىٰ فَسَنُيَسِّرُهُ لِلْعُسْرَىٰ

**"Hakika juhudi zenu bila ya shaka ni mbalimbali. Basi yule anayetoa na akawa na taqwa na akasadikisha lililo jema, basi Tutamuwepesishia kwa mepesi. Ama yule afanyaye ubakhili na [anayejidhania kuwa] amejitosheleza na akakadhibisha lililo jema, basi Tutamuwepesishia kwa magumu". (92:04-10)**

Huu ni utafiti mkubwa ambao unatakiwa kuhifadhiwa na kudhibitiwa kwa sababu unaenda kinyume na mapote yote ya Bid´ah na upotevu. Kwa I´tiqaad hii mtu anakuwa ni mwenye kwenda kinyume na mapote yote ya Bid´ah na upotevu ikiwa ni pamoja na Qadariyyah wakanushaji na Jabriyyah. Wote utakuwa ni mwenye kwenda kinyume nao na wewe utakuwa ni mwenye kuitakidi I´tiqaad ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum).

## 42. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya imani

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Katika misingi ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni kuwa:*

*Dini na Imani ni kauli na matendo. Kauli ya moyo na ulimi, na matendo ya moyo na ulimi na viungo vya mwili. Imani inazidi kwa utiifu na inashuka kwa maasi. Pamoja na hivyo, wao hawawakufurishi waislamu kwa kutenda maasi na madhambi makubwa, kama wanavyofanya Khawaarij, bali udugu wa Imani bado upo pamoja na kuwa kwa maasi. Kama Alivyosema (Subhaanahu wa Ta´ala) katika Aayah ya kisasi:*

فَمَنْ عُفِيَ لَهُ مِنْ أَخِيهِ شَيْءٌ فَاتِّبَاعٌ بِالْمَعْرُوفِ

*"Na anayesamehewa na nduguye kwa lolote basi kufuatilizwa kwake kuwe kwa wema naye alipe kwa wema."* ***(02:178)***

*Na Akasema (Subhaanah):*

وَإِن طَائِفَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ اقْتَتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا ۖ فَإِن بَغَتْ إِحْدَاهُمَا عَلَى الْأُخْرَىٰ فَقَاتِلُوا الَّتِي تَبْغِي حَتَّىٰ تَفِيءَ إِلَىٰ أَمْرِ اللَّهِ ۚ فَإِن فَاءَتْ فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَأَقْسِطُوا ۖ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ

*"Na mataifa [au makundi] mawili ya Waumini yakipigana, basi suluhisheni baina yao. [Lakini] mojawapo likikandamiza jengine, basi lipigeni [vita] lile linalokandamiza mpaka lielemee kwenye amri ya Allaah. Likishaelemea, basi suluhisheni baina yao kwa uadilifu na fanyeni haki - hakika Allaah Anapenda wafanyao haki. Hakika Waumini ni ndugu, basi suluhisheni baina ya ndugu zenu."* ***(49:09-10)***

*Hawapingi Imani ya Muislamu mtenda madhambi moja kwa moja na wala hawasemi kuwa atadumishwa Motoni milele, kama wanavyosema Mu´tazilah, bali Muislamu mtenda madhambi anaingia pia katika Imani. Kama ilivyo katika Kauli Yake (Ta´ala):*

فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ

*"Basi [aliyeua] aachilie huru mtumwa muumini."* ***(04:92)***

*Na wakati mwingine yawezekana akawa haingii katika Imani kamilifu. Kama ilivyo katika Kauli Yake (Ta´ala):*

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا

*”Hakika waumini ni wale ambao anapotajwa Allaah nyoyo zao zinajaa khofu [na hushtuka] na wanaposomewa Aayah Zake huwazidishia iymaan.”* ***(08:02)***

*Na kauli yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):*

*“Hazini mwenye kuzini pindi anapozini hali ya kuwa ni muumini, na wala haibi mwenye kuimba pindi anapoiba hali ya kuwa ni muumini, na wala hanywi pombe pindi anapokunywa hali ya kuwa ni muumini, na hapori mwenye kupora pindi anapopora kitu chenye thamani, jambo ambapo linafanya watu kumwangalia kwa ajili ya hilo, hali ya kuwa ni muumini.”*[46]

*Tunasema: “Ni muumini mwenye Imani pungufu” au “Ni muumini akiwa na Imani yake, mtenda dhambi kwa dhambi yake kubwa.” Kwa hali hiyo hapewi Imani kamilifu na wala haikanushwi moja kwa moja.*

## MAELEZO

**Katika misingi ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni... -** Utafiti huu ni mkubwa na ni miongoni mwa I´tiqaad za Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Wanasema kuwa imani ni maneno na vitendo. Maneno ya moyo na ulimi, matendo ya moyo na viungo vya mwili. Haya ndio wanayoamini Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Hili ni tofauti na Murji-ah, Mu´tazilah na Khawaarij. Khawaarij wanayakubali haya, lakini wanasema kuwa imani haizidi wala haipungui. Kadhalika Mu´tazilah wanasema kuwa imani haizidi wala haipungui. Wanasema kuhusu imani ima iwepo yote na ikibidi kuondoka inaondoka yote. Kwa ajili hii ndio maana wamemkufurisha mtenda madhambi na kuonelea kuwa ni mwenye kudumishwa Motoni milele. Mu´tazilah pia wamekubaliana nao juu ya hilo inapokuja katika hukumu ya Aakhirah na kwamba mtenda madhambi atadumishwa Motoni milele. Murji-ah wao wameyandosha matendo katika

[46] al-Bukhaariy (2475) na Muslim (57).

imani na kusema kuwa imani ni kutamka au kusadikisha peke yake. Mapote yote haya yaliyotajwa yamekosea na kupotea kutoka kwenye Njia.

Sahihi ni yale waliyomo Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ambapo wanasema kuwa imani ni maneno na vitendo, maneno ya moyo na ulimi, vitendo vya moyo na viungo vya mwili.

Mfano wa matendo ya moyo ni kama kumpenda Allaah, kumuogopa, kumtakasia ´ibaadah, kusadikisha, kusadikisha kwa maneno, Tasbiyh, Tahliyl na Dhikr.

Mfano wa matendo ya viungo vya mwili ni kama swalah, zakaah, swawm, hajj na Jihaad. Namna hii ndivyo wanavyoamini Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ya kwamba imani ni maneno na matendo, inazidi kwa kufanya mambo ya utiifu na inapungua kwa kufanya mambo ya maasi. Msemo wenye kusema:

"Imani ni maneno na matendo."

wanaingia ndani yake Khawaarij na Mu´tazilah. Msemo wenye kusema:

"Imani inazidi kwa kufanya mambo ya utiifu na inapungua kwa kufanya mambo ya maasi."

Mu´tazilah na Khawaarij wanatoka. Ni Radd kwao. Msemo wenye kusema:

"Imani ni maneno na matendo."

Murji-ah vilevile wanatoka.

Ni wajibu kwa muumini aamini ´Aqiydah hii na atendee kazi muqtadha yake.

**Hawapingi Imani ya Muislamu mtenda madhambi... -** Miongoni mwa ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni pamoja vilevile na kutompokonya imani muislamu mtenda dhambi ambaye anajinasibisha na Uislamu. Hawaonelei vilevile kuwa atadumishwa Motoni milele. Khawaarij ndio wanampokonya imani yote. Mu´tazilah wanaonelea kuwa atadumishwa Motoni milele. Muislamu mtenda dhambi anaingia katika imani. Kwa mfano Kauli Yake (Ta´ala):

فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ

**”Basi [aliyeua] aachilie huru mtumwa muumini.” (04:92)**

وَعَلَى الثَّلَاثَةِ الَّذِينَ خُلِّفُوا حَتَّىٰ إِذَا ضَاقَتْ عَلَيْهِمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ وَضَاقَتْ عَلَيْهِمْ أَنفُسُهُمْ وَظَنُّوا أَن لَّا مَلْجَأَ مِنَ اللَّهِ إِلَّا إِلَيْهِ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوبُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ

**"Na [pia Allaah Akapokea tawbah] ya wale watatu waliobaki nyuma [kutokwenda vita vya Tabuwk wakajuta mno] mpaka ardhi ikadhikika kwao juu ya kuwa ni pana na zikadhikika nafsi zao, na wakatambua kwamba hakuna pa kumkimbia Allaah isipokuwa Kwake; kisha [Allaah] Akapokea tawbah yao ili watubie. Hakika Allaah Yeye Ndiye Mwingi wa kupokea tawbah, Mwenye kurehemu. Enyi mlioamini! Mcheni Allaah na kuweni pamoja na wakweli." (09:119)**

Anaingia ndani ya wito huu ambao wanazungumzishwa wale walioamini. Ama sehemu za matapo na sifa hawi mwenye kuingia. Kauli Yake (Jalla wa ´Alaa):

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا

**”Hakika waumini ni wale ambao anapotajwa Allaah nyoyo zao zinajaa khofu [na hushtuka] na wanaposomewa *Aayah* Zake huwazidishia iymaan.”(08:02)**

Kadhalika haingii katika maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

“Hazini mwenye kuzini pindi anapozini hali ya kuwa ni muumini, na wala haibi mwenye kuimba pindi anapoiba hali ya kuwa ni muumini, na wala hanywi pombe pindi anapokunywa hali ya kuwa ni muumini, na hapori mwenye kupora pindi anapopora kitu chenye thamani, jambo ambapo linafanya watu kumwangalia kwa ajili ya hilo, hali ya kuwa ni muumini.”[47]

Vilevile dalili nyenginezo mfano wa hizo.

Kwa haya inapata kujulikana ya kwamba muumini mwenye imani kamilifu haingii katika mkumbo wenye kulaumiwa. Upande mwingine muumini mwenye imani pungufu anaingia katika mkumbo wenye kulaumiwa:

“Hazini mwenye kuzini pindi anapozini hali ya kuwa ni muumini, na wala haibi mwenye kuimba... "

[47] al-Bukhaariy (2475) na Muslim (57).

Kwa sababu imani yake ni pungufu. Tunapozungumzia waumini wenye imani kamilifu waislamu watenda madhambi wanatoka humo.

Wasifu wa imani ni yule muislamu ambaye anazungumzishwa kutokana na imani yake. Hivyo muislamu mtenda dhambi kuna uwezekano akaingia katika Kauli Yake:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا

**"Enyi mlioamini." (02:104)**

إِنَّ الدِّينَ عِندَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ

**"Hakika dini mbele ya Allaah ni Uislamu." (03:19)**

Vivyo hivyo akaingia katika maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Muislamu ni ndugu ya Muislamu mwenzake."[48]

Anaingia humu muislamu mtenda dhambi na asiyekuwa mtenda dhambi. Lakini kunapotajwa imani kamilifu yenye kuambatana na matapo muislamu mtenda dhambi haingii humo. Lakini kunapotajwa imani isiyofungamanishwa muislamu mtenda dhambi anaingia humo. Kama ilivyotangulia hapo mbele kwa mfano Kauli Yake:

فَمَنْ عُفِيَ لَهُ مِنْ أَخِيهِ

**"... na anayesamehewa na nduguye kwa lolote... " (02:178)**

Muuaji ameitwa kuwa ni ndugu.

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ

**"Hakika Waumini ni ndugu." (49:10)**

Wameitwa kuwa ni ndugu pamoja na kuwa wamepigana vita.

[48] al-Bukhaariy (2442) na Muslim (2580)

Kwa ufupi ni kwamba muislamu mtenda dhambi anaingia katika imani isiyofungamanishwa:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا

**"Enyi mlioamini!" (49:11)**

وَمَن قَتَلَ مُؤْمِنًا خَطَأً فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ

**"Na atakayemuua muumini kwa kukosea basi aachilie huru mtumwa Muumin." (04:92)**

Kuna Aayah nyenginezo mfano wa hizi.

Sambamba na hilo haingii katika imani kamilifu ambayo watu wake wamesifiwa. Kwa mfano Kauli Yake (Ta´ala):

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ

**"Hakika Waumini ni wale ambao anapotajwa Allaah nyoyo zao, zinajaa khofu [na kushtuka] wanaposomewa *Aayaat* Zake huwazidishia iymaan na kwa Mola wao wanategemea. Ambao wanasimamisha Swalah na katika yale Tuliyowaruzuku hutoa." (08:02-03)**

Vilevile maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

“Hazini mwenye kuzini pindi anapozini hali ya kuwa ni muumini, na wala haibi mwenye kuimba... "

Utenda dhambi wake umefanya akakosa imani kamilifu. Mtu sampuli hii huitwa muislamu, muumini mwenye imani pungufu au pia mtu anaweza kusema kuwa ni muumini kutokana na imani alionayo na ni mtenda dhambi kutokana na dhambi yake kubwa. Hivyo anawakuwa hakupewa jina la muumini isiyofungamanishwa na wala anakuwa hakupokonywa nalo. Mtu kama huyu mtu hafai kusema kuwa ni muumini mwenye imani kamilifu kama ambavyo

haitakikani vilevile kusema kuwa sio muumini. Isipokuwa ikiwa kama mtu anakusudia kuwa sio muumini mwenye imani kamilifu.

Kwa haya wanaraddiwa Mu´tazilah na Khawaarij na mtu anabaki kuwa ni muumini kwa mujibu wa ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah inapokuja katika mlango huu mkubwa ambao wasomi wengi wamepotea kwao.

## 43. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya wakeze Mtume, Ahl-ul-Bayt na Maswahabah

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Katika misingi ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni:*

*Wenye nyoyo na ndimi zilizo salama kwa Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kama Alivyowasifia Allaah katika Kauli Yake (Ta´ala):*

وَالَّذِينَ جَاءُوا مِن بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِّلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

*”Na wale waliokuja baada yao ni wenye kusema: “Mola wetu! Tusamehe na ndugu zetu ambao wametutangulia kwa iymaan na wala Usijaalie katika nyoyo zetu mafundo kwa wale walioamini. Mola wetu! Hakika Wewe ni Mwenye huruma mno, Mwenye kurehemu.”* ***(59:10)***

*Na kumtii vilevile Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa kauli yake:*

*“Msiwatukane Maswahabah zangu! Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Lau mmoja wenu atatoa dhahabu sawa na [mlima wa] Uhud, haitofikia Mudd[49] iliotolewa nao wala nusu yake.”[50]*

*Wanayakubali yaliyokuja katika Kitabu, Sunnah na Ijmaa´ kutokana na fadhila na nafasi zao. Wanawafadhilisha waliojitolea na kupigana vita kabla ya ushindi – nayo ni suluhu ya Hudaybiyah - wao wana daraja kubwa zaidi kuliko wale ambao waliojitolea baadae na wakapigana. Na wanawatanguliza Muhaajiruun juu ya Answaar. Wanaamini ya kwamba Allaah Kawaambia wale waliopigana vita vya Badr – na walikuwa miatatu na kumi na kitu:*

---

[49] Imaam ´Uthaymiyn (Rahimahu Allaah) amesema: ”Mudd ni sawa na kama robo hivo.” (Sharh al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah (02/252) iliyochapishwa na Daar Ibn-ul-Jawziy).

[50] al-Bukhaariy (3673) na Muslim (2541).

*"Fanyeni mtakacho. Nimeshawasamehe."*[51]

*Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kasema kuwa:*

*"Hakuna yeyote kati yenu atoae bay´ah [kiapo cha usikivu na utiifu] chini ya mti atakayeingia Motoni."*[52]

*Bali Yuko radhi nao, nao wako radhi Naye na walikuwa zaidi ya elfu moja na mianne.*

*Na wanamshahidilia Pepo yule ambaye Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kamshahidilia, kama wale (Maswahabah) kumi, na Thaabit bin Qays bin Shimmaas na Maswahabah wengineo.*

*Na wanayathibitisha yale yaliyopokelewa kwa njia nyingi kutoka kwa kiongozi wa waumini ´Aliy bin Abiy Twaalib (Radhiya Allaahu ´anhu) na wengine, ya kwamba mbora wa Ummah huu baada ya Mtume wake ni Abu Bakr, kisha ´Umar, kisha ´Uthmaan na halafu ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhum), kama zilivyotolea dalili hivyo Aathaar. Hali kadhalika kama walivyokubaliana Maswahabah kumtanguliza ´Uthmaan kwa kumpa bay´ah, pamoja na kuwa baadhi ya Ahl-us-Sunnah wametofautiana kwa ´Uthmaan na ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhumaa) – baada ya kukubaliana kwao kumtanguliza Abu Bakr na ´Umar – ni nani aliyebora. Kuna baadhi ambao wamemtanguliza ´Uthmaan kisha baada ya hapo wakanyamaza au wakasema kuwa wanne ni ´Aliy. Na baadhi ya wengine wakamtanguliza ´Aliy na wengine wakasimama.*

*Lakini, mwishoni walikubaliana Ahl-us-Sunnah kumtanguliza ´Uthmaan kisha ´Aliy, hata kama masuala haya – kuhusu ´Uthmaan na ´Aliy - wengi katika Ahl-us-Sunnah wanaona kuwa sio ya msingi ambayo atahukumiwa upotevu yule atakayeyakhalifu, lakini masuala ambayo mtu atahukumiwa upotevu ni masuala ya Uongozi. Hili ni kwa sababu wanaamini ya kwamba Khaliyfah baada ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni Abu Bakr, kisha ´Umar, kisha ´Uthmaan na kisha ´Aliy (Radhiya Allaahu*

---

[51] al-Bukhaariy (3007) Muslim (2494).

[52] Abuu Daawuud (4649) na (4650), at-Tirmidhiy (3748) na (3757), Ibn Maajah (134) na wengine. Imaam al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) amesema kuwa ni Swahiyh katika "Swahiyh al-Jaamiy´ as-Swaghiyr" (4010).

*´anhum). Atayakekashifu uongozi wa mmoja katika maimamu hawa, basi ni mpotevu kuliko punda wa kufugwa.*

*Wanawapenda na kufanya urafiki na watu wa familia ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wanafuata wasia wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliposema siku ya Ghadiyr Khumm:*

*"Ninawakumbusha kwa Allaah kuhusiana na watu wa familia yangu! Ninawakumbusha kwa Allaah kuhusiana na watu wa familia yangu!"*[53]

*Kamwambia hali kadhalika mtoto wa ami yake Ibn ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) ambaye alikuwa amekuja kushtaki ya kwamba baadhi ya Quraysh wanawachukia Banuu Haashim. Akasema:*

*"Ninaapa kwa Yule ambaye Nafsi yangu iko Mkononi Mwake. Hawatoamini mpaka wawapende kwa ajili ya Allaah na kwa ukaribu wenu kwangu."*[54]

*Na amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):*

*"Allaah Kawachagua Banuu Ismaa´iyl. Na kutoka Banuu Ismaa´iyl Amechagua Kanaanah. Na kutoka Kanaanah Amechagua Quraysh. Na kutoka Quraysh Amechagua Banuu Haashim na Amenichagua mimi kutoka Banuu Haashim."*[55]

*Hali kadhalika wanawapenda na kufanya urafiki na wake za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), wao ni wamama wa waumini. Na wanaamini ya kwamba wao ndio wakeze Aakhirah, na khususan Khadiyjah (Radhiya Allaahu ´anhaa) ambaye ni mama wa watoto wake wengi. Na yeye ndiye alikuwa wa kwanza kumuamini na kumsaidia kwa kazi yake na alikuwa ni mwenye manzilah ya juu kwake.*

*Na asw-Swiddiyqah bint asw-Swiddiyq (Radhiya Allaahu ´anhumaa), ambaye Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema juu yake:*

---

[53] Muslim (2408).

[54] Ahmad katika "Fadhwaail-us-Swahaabah" (1756).

[55] Muslim (2276).

*"Ubora wa ´Aaishah kwa kulinganisha na wanawake wengine ni kama ubora wa Thariyd kulinganisha na chakula chengeni."*[56]

*Na wanajitenga mbali na njia ya Raafidhwah, ambao wanawachukia na kuwatukana Maswahabah, hali kadhalika Nawaaswib, ambao wanawaudhi watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), ima kwa kauli au matendo.*

*Na wanayanyamazia yaliyopitika baina ya Maswahabah na wanasema:*

*"Kati ya mapokezi haya yaliyopokelewa kuna ambayo ni ya uongo, na kuna ambayo yamezidishwa juu yake na kupunguzwa, na kuna ambayo yamebadilishwa kwa sura yake ya kihakika na ndani yake kuna ya sahihi ambayo wamepewa udhuru kwayo. Ima walikuwa ni wenye kujitahidi baada ya kuifikia haki wakapatia, au walikuwa ni wenye kujitahidi baada ya kuifikia haki wakakosea."*

*Wao pamoja na hivyo hawaitakidi ya kwamba kila mmoja katika Maswahabah kakingwa na dhambi kubwa au ndogo. Bali kinyume chake kuna uwezekano wakafanya dhambi kwa ujumla. Wana haki ya kutangulizwa na fadhila ambazo zinafanya wanasamehewa kwa lile wangelolifanya – ikiwa wamefanya kitu. Wanasamehewa hata madhambi ambayo yasingelisamehewa kwa mwengine yeyote baada yao, kwa kuwa wana mema mengi ambayo hana yeyote wa baada yao, na ambayo vilevile yanafuta makosa yao.*

*Kumethibiti kwa kauli ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba wao ndio karne bora na kwamba akitoa Swadaqah mmoja wao kiasi cha Mudd ina uzito zaidi kuliko inayotolewa na aliye baada yao, hata kama huyu atatoa dhahabu sawa na kiasi cha mlima wa Uhud.*

*Ikiwa mmoja wao atapitikiwa na dhambi, atakuwa ima katubia kwa dhambi hiyo, au kaleta mema ambayo yameifuta au amesamehewa kwa fadhila za kutangulia kwake, au [kasamehewa] kwa uombezi wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) – na hakuna ambaye ana haki zaidi ya uombezi wake isipokuwa wao – au kapewa mtihani kwa majaribio ya duniani ambayo yamefuta dhambi yake.*

[56] al-Bukhaariy (3770) na Muslim (2446).

*Ikiwa madhambi haya yaliyofanywa yanafanywa namna hii, vipi kwa mambo ambayo walikuwa ni wenye kujitahidi kuifikia haki? Ikiwa wamepatia wana ujira mara mbili na wakikosea wana ujira mara moja na kosa lao limesamehewa. Isitoshe, matendo mabaya yaliyofanywa na baadhi yao ni machache mno na yasiyokuwa na maana ukilinganisha na fadhila za nafasi yao na mema yao, kama kwa mfano kumuamini Allaah na Mtume Wake, na kupigana Jihaad katika njia ya Allaah, Hijrah, nusra, elimu yenye manufaa na matendo mema n.k. Yule atakayetazana historia ya Maswahabah kwa elimu na umaizi na fadhila Alizowaneemesha Allaah kwazo, basi atajua kwa yakini ya kwamba wao ndio viumbe bora baada ya Mitume. Kamwe hakupatapo kuwepo na hakutokuwepo mtu mfano wao. Wao ndio wasomi wa wasomi katika Ummah huu – ambao ndio watu bora na wa karimu kwa Allaah (Ta´ala).*

**MAELEZO**

Mlango huu ni miongoni mwa milango bora na muhimu kabisa ya kitabu hiki ambacho ni "al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah" kuhusiana na Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum). Ndani yake mna Radd kwa Raafidhwah na Nawaaswib. Vilevile ndani yake mna ubainifu wa fadhila na manzilah zao (Radhiya Allaahu ´anhum). Ni mlango mkubwa. Mwandishi amefanya vizuri kabisa kwa kuleta ibara ambazo ziko wazi na bainifu zaidi.

**Katika misingi ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah... -** Miongoni mwa ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah (Radhiya Allaahu ´anhum) ni wenye mioyo na ndimi zilizo salama kwa Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mioyo yao iko salama. Wanawapenda na kuwatakia radhi. Kwa sababu kuwapenda ni sehemu katika dini (Radhiya Allaahu ´anhum). Wao ndio wabebaji wa Shari´ah na karne bora. Kwa ajili hiyo ndio maana kuwapenda ikawa ni dini. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanawapenda kwa ajili ya Allaah na mioyo yao iko salama juu yao. Ni wenye mapenzi tele juu yao. Ndimi zao ziko salama kwa njia ya kwamba hawawatukani na wala hawawatii kasoro. Badala yake wanawatakia radhi na kuwaombea du´aa. Kwa sababu kufanya hivyo ni kumtii Allaah. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ

**"Hakika Waumini ni ndugu, basi suluhisheni baina ya ndugu zenu. Na Mcheni Allaah ili mpate kurehemewa." (49:10)**

Isitoshe wanatekeleza wasia wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambaye amesema:

"Msiwatukane Maswahabah zangu! Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Lau mmoja wenu atatoa dhahabu sawa na (mlima wa) Uhud, haitofikia Mudd iliotolewa nao wala nusu yake."

Hii ni moja katika sifa ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Ni wenye ndimi zilizo salama kwa Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wao ndio viumbe bora baada ya Mitume (´alayhimus-Swalaatu was-Salaam). Hakupatapo kuwepo na wala hakutokuwepo mfano wao (Radhiya Allaahu ´anhum).

Lililo la wajibu ni kuwapenda kwa ajili ya Allaah, kuwaombea radhi, kunyamazia mizozo iliyopitika kati yao na kuamini kuwa wao ndio karne bora.

**Na wanayathibitisha yale yaliyopokelewa kwa njia nyingi... -** Kadhalika inatakiwa kuamini ya kwamba mbora katika makhaliyfah waongofu ni asw-Swiddiyq, kisha ´Umar, kisha ´Uthmaan halafu ´Aliy. Licha ya kwamba kuna baadhi ya watu waliovutana kidogo kama inatakiwa kumtanguliza ´Uthmaan juu ya ´Aliy au kinyume chake. Lakini hatimaye Ahl-us-Sunnah walifikia kuona kuwa kuwa ´Uthmaan ndiye watatu na kwamba ´Aliy ndiye wanne. Hili linahusiana na uongozi na ubora.

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanatakiwa kuamini hivi na wajitenge mbali na mwenendo wa Raafidhwah ambao kazi yao wao ni kuwatukana Maswahabah na kuwafanyia maudhi. Vilevile wanatakiwa kujitenga mbali na mwenendo wa Nawaaswib ambao wanawaudhi watu wa nyumba ya kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa maneno na vitendo. Ahl-us-Sunnah wanatakiwa kujiepusha na tabia hii chafu.

**Na wanamshahidilia Pepo... -** Kadhalika wanamshuhudilia yule ambaye ameshahidiliwa na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) Pepo

ikiwa ni pamoja na wale Maswahabah kumi, Thaabit bin Qays bin Shammaas, ´Abdullaah bin Salaam, ´Ukkaashah bin Muhswan na wengineo ambao wameshahidiliwa na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wanatakiwa kushahidiliwa. Ambaye kumethibiti kushahidiliwa na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) anashahidiliwa.

**Wanayakubali yaliyokuja katika Kitabu, Sunnah na Ijmaa´... -** Kadhalika wanaamini yaliyothibiti kuhusu watu wa vita vya Badr ambapo waliambiwa:

"Fanyeni mtakacho. Nimeshawasamehe."

Vilevile wanaamini kuwa hatoingia Motoni yeyote ambaye alitoa kiapo cha usikivu na utiifu chini ya mti. Hii ni ile *bay´ah* ya Ridhwaan. Kwa sababu imethibiti kutoka kwake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwamba amesema:

"Hakuna yeyote kati yenu atoae *bay´ah* chini ya mti atakayeingia Motoni."

Sivyo tu, bali Allaah akateremsha kuhusu wao:

لَّقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنزَلَ السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَابَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا

**"Kwa yakini Allaah Amewawia radhi Waumini walipofungamana nawe chini ya mti, [Allaah] Alijua yale yaliyomo nyoyoni mwao, basi Akawateremshia utulivu na Akawapa ushindi wa karibu." (48:18)**

Yote haya ni katika ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.

Ni wajibu kwa watu wa imani baada yao kufuata mfumo wao na waamini kuwa Maswahabah wote ndio wabora wa Ummah na wenye fadhila zaidi.

**Na wanayanyamazia yaliyopitika baina ya Maswahabah... -** Kuhusiana na kasoro zenye kusimuliwa kutoka kwa baadhi ya Maswahabah ni chache sana ukilinganisha na kheri nyingi alizowapa Allaah, fadhila zao na matendo yao makubwa. Aliyofanya mmoja wao ima atakuwa alitubia kwayo, alifanya jema lililofuta ovu hilo, alisamehewa na fadhila za kutangulia kwake, atapata uombezi wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) - kwani wao ni wenye haki zaidi ya kupata uombezi wake - au kwa sababu ya mitihani ya maradhi na mengineyo ambayo yalifanya akasamehewa. Hivi ndivyo wanavyoonelea Ahl-

us-Sunnah wal-Jamaa´ah katika masuala haya yaliyotajwa na mwandishi (Rahimahu Allaah).

Muumini anatakiwa kuuhifadhi mlango huu vizuri na atendee kazi maana yake. Vilevile ´Aqiydah yake inatakiwa iwe imebobea ili aweze kutofautiana na Ahl-ul-Bid´ah wote ikiwa ni pamoja na Raafidhwah, Nawaaswib na wazushi wengine ambao dhana zao zimefeli au wamevuka mipaka kwa watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kama wanavyofanya Raafidhwah. Wengine dhana zao zikafeli, wakazembea kunako haki zao, kama wanavyofanya Khawaarij, Mu´tazilah na mfano wao miongoni mwa wale ambao wana maneno na matendo machafu juu ya Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kizazi chake (Radhiya Allaahu ´anhum). Tunamuomba Allaah awawie radhi na atujaalie kuwa ni miongoni mwa wenye kuwafuata kwa wema.

## 44. I´tiqaad ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya karama za mawalii

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema*:*

*Katika misingi ya Ahl-us-Sunnah ni:*

*Kusadikisha karama za mawalii na yale matukio yasiyokuwa ya kawaida ambayo Allaah Hufanya yakapitia kwao, ima katika aina mbali mbali za elimu, maono, uwezo maalum na taathira, na yaliyopokelewa kuhusu watu waliotangulia katika Suurah "al-Kahf" na kadhalika. Hali kadhalika kuhusu watu waliotangulia katika Ummah huu miongoni mwa Maswahabah, Taabi´uun na watu wa Ummah zingine zilizobaki, nayo yataendelea kuwepo mpaka siku ya Qiyaamah.*

*Katika njia ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni:*

*Kufuata mapokezi ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kwa undani na kwa uinje, na kufuata njia ya waliotangulia katika Muhaajiruun na Answaar, na kufuata wasia wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) pindi aliposema:*

*"Jilazimieni na Sunnah zangu na Sunnah za makhaliyfah wangu waongofu baada yangu. Shikamaneni nazo bara bara na ziumeni kwa magego yenu. Na tahadharini na mambo ya yakuzua! Kwani hakika kila Bid´ah ni upotevu."*

*Na wanajua ya kwamba hakika maneno ya kweli kabisa, ni Maneno ya Allaah, na uongofu bora ni wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wanayapa kipaumbele Maneno ya Allaah yatangulie mbele kabla ya maoni ya watu wengine na wanatanguliza uongofu wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kabla ya uongofu wa wengine wote. Na kwa ajili hii ndio wakaitwa "Ahl-ul-Kitaab was-Sunnah". Wanaitwa vilevile Ahl-ul-Jamaa´ah" kwa kuwa "Jamaa´ah" ni ile iliokusanyika. Na kinyume chake ni "al-Furqah"[57], hata kama lafdhi ya "al-Jamaa´ah" imekuwa ni jina la watu wote waliokusanyika.*

[57] Mgawanyiko.

*Ijmaa´ ndio msingi wa tatu unaotegemewa katika elimu na dini. Nao Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanapima kwa misingi hii mitatu mambo yote ya dini kuhusiana na maneno na matendo ya watu, sawa yaliyojificha na yaliyodhahiri. Ijmaa´ ni yale waliokubaliana Salaf as-Swaalih, kwa kuwa baada yao kulikithiri tofauti na Ummah ukagawanyika.*

MAELEZO

**Katika misingi ya Ahl-us-Sunnah... -** Miongoni mwa misingi ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, ni kama alivyosema mwandishi ambaye ni Abul-´Abbaas Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah), ni kusadikisha karama za mawalii, aliyotaja Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) juu yao na yaliyopitika baada ya hapo.

Karama ni kitu kinachofanywa na mtu kisichokuwa cha kawaida. Ni kitu kisichokuwa cha kawaida kwa viumbe wengine. Haya yanaitwa kuwa ni "karama" pale yanapofanywa na mtu miongoni mwa mawalii wa Allaah wakweli. Endapo mambo kama haya yatafanywa na wasiokuwa wao - yaani waumini wakweli - itakuwa ni uchawi na mambo ya mashaytwaan. Tofauti na yakifanywa kupitia mtu ambaye ni muumini inakuwa ni karama za mawalii.

Haitokuwa karama isipokuwa mpaka pale itapojulikana kuwa mtu amenyooka katika dini ya Allaah, kama alivyosema Shaykh (Rahimahu Allaah):

"Lau ataruka angani au akapita juu ya maji hazingatiwi kuwa ni walii."[58]

Ni lazima apimwe kwa mizani ya Qur-aan na Sunnah. Akiwa amenyooka juu ya Qur-aan na Sunnah huyo ndiye walii wa Allaah. Vinginevyo atakuwa ni katika mawalii wa shaytwaan. Amesema (´Azza wa Jall):

وَمَا كَانُوا أَوْلِيَاءَهُ ۚ إِنْ أَوْلِيَاؤُهُ إِلَّا الْمُتَّقُونَ

**"Na hawakuwa ni mawalii Wake. Hawakuwa mawalii Wake isipokuwa wenye taqwa." (08:34)**

أَلَا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ

[58] Tazama "al-Furqaan baina Awliyaa´-ir-Rahmaan wa Awliyaa´-ish-Shaytwaan", uk. 45.

**"Tanabahi! Hakika mawalii wa Allaah hawana khofu juu yao na wala hawatohuzunika. Ambao wameamini na wakawa wana taqwa." (10:62-63)**

Miongoni mwao ni pamoja vilevile na watu wa al-Kahf. Allaah aliwakirimu kusinzia [ndani ya pango] kwa miaka mia tatu na wakazidisha tisa. Baada ya hapo Allaah akawahuisha. Hii ni ishara miongoni mwa ishara za Allaah kutokana na imani na taqwa yao. Allaah aliwafanya kuwa ni alama na funzo.

Kadhalika kama ilivyopitika kwa ´Abbaad bin Bishr na Usayyid bin Hudhwayr ambao ni Maswahabah wawili watukufu waliokuwa katika zama za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Walikuwa wametoka nyumbani kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika usiku wenye giza. Ghafla kila mmoja akaangaziwa katikati yake taa lenye kumwangazia njia mpaka kila mmoja alipofika nyumbani kwa familia yake[59].

Vilevile kisa cha at-Twufayl ad-Dawsiy, ambaye alikuwa ni mkuu wa kabila la Daws, pindi alipoingia katika Uislamu watu wake walichelewa kusilimu. Ndipo akamwambia Mtume wa Allaah amuombee kwa Allaah amfanye awe na alama huenda wakaongoka. Akamuombea (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa Allaah amfanye kuwa na alama ili awaongoze kwayo watu wake. Allaah akafanya kati ya macho yake akawa na kitu mfano wa taa pale anapowaendea watu wake. Akamuomba Mola Wake aliweke kwengine mbali na uso. Ndipo Allaah akaiweka nuru hiyo [nuru] kwenye sauti yake pale anapozungumza. Allaah akawaongoza kwayo watu wake kupitia kwake na akawafanya kuwa waislamu[60].

Makusudio ni kwamba ni mambo yanayoenda kinyume na mazowea. Ikiwa mwenye kuyafanya ni mtu anayemcha Allaah na anatambulika kwa wema, basi ayafanyayo ni karama. Na ikiwa ni kinyume na hivyo, basi ayafanyayo ni katika mambo ya wachawi na mashaytwaan. Kwa haya [karama wazifanyazo mawalii] ni kwa sababu ya kufuata kwao Qur-aan na Sunnah.

---

[59] Tazama Fataawaa za Shaykh "Nuur ´alaad-Darb" (02/191-193).

[60] Abuu Na´iym al-Aswbahaaniy katika "Ma´arifat-us-Swahaabah" (11/175) (3500) na al-Bayhaqiy katika "ad-Dalaail-un-Nubuwwah (05/460) (2108).

## *Qur-aan, Sunnah kwa ufahamu wa Salaf*

**Katika njia ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni kufuata mapokezi... -** Miongoni mwa misingi ya Ahl-us-Sunnah ni kufuata mapokezi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na yale waliyokuwemo makhaliyfah waongofu. Huu ni mwenendo mmoja wapo wa Ahl-us-Sunnah. Wanafuata mfumo wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), mapokezi yake na mapokezi ya makhaliyfah wake waongofu. Hii ndio njia ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Kwa ajili hii ndio maana wanaitwa "Ahl-ul-Kitaab was-Sunnah", "Ahl-ul-Jamaa´ah". Neno "Jamaa´ah" ni mkusanyiko na kinyume chake ni al-Furqah. Wameitwa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah kwa sababu wamekusanyika katika Kitabu na Sunnah, wakayasadikisha na wakayapima mambo yao kwavyo. Hawa ndio Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Wamekusanyika katika kuiadhimisha Qur-aan na Sunnah na kuvitendea kazi. Kwa misingi hii mitatu wanayapima maneno na vitendo vyote vya watu.

Msingi wa kwanza ni Qur-aan.

Msingi wa pili ni Sunnah Swahiyh.

Msingi wa tatu ni Ijmaa´ yenye kudhibitiwa. Inahusiana na yale maafikiano ya Salaf ambayo ni ya Maswahabah Radhiya Allaahu ´anhum). Maneno na vitendo vyote vinavyofanywa na watu vinapimwa na misingi hii. Yanayoafikiana navyo yanakubaliwa na yanayoenda kinyume navyo anarudishiwa mwenye nayo. Pasi na kujali atakuwa nani.

## 45. Baadhi ya sifa tukufu za Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah

Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

*Pamoja na misingi hii wanaamrisha mema na wanakataza maovu kwa yale ambayo Shari´ah imeyawajibisha. Wanaonelea kufanya Hajj, kupigana Jihaad, Swalah ya Ijumaa na sikukuu pamoja na viongozi [watawala], ni mamoja wakiwa wema au waovu. Wanahifadhi Swalah ya Jamaa´ah na wanaona kuwapa naswaha Ummah ni katika sehemu ya Dini. Na wanaamini maana ya kauli ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):*

*"Muumini kwa muumini mwenzake ni kama jengo; upande mmoja unaupa nguvu upande mwingine."*

*Halafu (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akakutanisha baina ya vidole vyake viwili.*[61]

*Na kauli yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):*

*"Mfano wa waumini, katika kupendana kwao, na kuhurumiana kwao na kuhisiana kwao, ni kama mfano wa mwili mmoja. Wakati kiungo cha mwili kinapatwa na maumivu, mwili mzima unapatwa na homa."*[62]

*Na wanaamrisha kuwa na subira wakati wa mitihani, kuwa na shukurani wakati wa raha na kuridhia kwa shida iliyokadiriwa. Wanalingania katika tabia nzuri na matendo mema. Na wanaamini maana ya kauli yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):*

*"Muumini mwenye imani kamilifu ni yule mwenye tabia nzuri zaidi."*[63]

*Na wanahimiza uunge uhusiano na yule uliyekatana naye, na ummpe yule uliyemnyima, umsamehe yule aliyekudhulumu na kukufanyia ubaya.*

---

[61] al-Bukhaariy (6026) na Muslim (2585)

[62] al-Bukhaariy (6011) na Muslim (2586)

[63] Ahmad (2/472), Abuu Daawuud (4682) na at-Tirmidhiy (1162). Imaam al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) kasema kuwa ni Swahiyh katika "Swahiyh at-Tirmidhiy" (3/886)

*Na wanaamrisha kuwatendea wema wazazi wawili na kuwaunga ndugu, kuwatendea wema majirani, kuwafanyia wema mayatima na masikini, na wasafiri na watumwa.*

*Na wanakataza majivuno na kiburi, ukandamizaji na unyanyasaji kwa viumbe, sawa iwe kwa haki au pasi na haki.*

*Na wanaamrisha kuwa na maadili mema na wanakataza mabaya.*

*Na katika kila wanayoyasema na kuyafanya – katika haya na mengineyo – wanafuata Kitabu na Sunnah. Njia yao ni Dini ya Uislamu ambayo Allaah Amemtuma kwayo Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Lakini alipoelezea Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba Ummah wake utagawanyika mapote sabini na tatu na yote yataingia Motoni isipokuwa moja, nayo ni al-Jamaa´ah."*[64]

*Na katika Hadiyth nyingine kutoka kwake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:*

*"Ni wale ambao watakuwemo kwa mfano wa yale niliyomo mimi hii leo na Maswahabah zangu."*[65]

*wamekuwa wale wenye kushikamana bara bara na Uislamu wa wazi na msafi kabisa, ni "Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah". Na miongoni mwao kuna wakweli, mashahidi na watu wema na vilevile kuna maimamu wa uongofu na wenye kuzuia giza la kwenye mwangaza. Wana nafasi kuu na fadhila zingine tulizozitaja. Miongoni mwao kuna ´Abdaal na maimamu wa Dini ambao wamekusanyika Waislamu kwa uongofu wao.*

*Nao ni at-Twaaifah al-Mansuurah, ambao Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema kuhusu wao:*

*"Na hakitoacha kikundi katika Ummah wangu kuwa ni chenye kunusuriwa juu ya haki. Hatowadhuru wale wenye kwenda kinyume nao na kuwapinga mpaka itapofika Qiyaamah."*[66]

---

[64] Abuu Daawuud (4596), Ahmad (2/333), at-Tirmidhiy (2778). Ibn Maajah (3991) na wengine. Tazama "as-Silsilah as-Swahiyhah" (204) ya Imaam al-Albaaniy (Rahimahu Allaah).

[65] at-Tirmidhiy (2779) na al-Haakim (1/129).

[66] al-Bukhaariy (3641) na Muslim (1037).

## *Hitimisho*

*Tunamuomba Allaah Atujaalie katika wao, na wala Asizipotoe nyoyo zetu baada ya Kutuongoza na Aturehemu. Hakika Yeye Ndiye Al-Wahhaab. Na Allaah Anajua zaidi. Swalah na salaam zimwendee Muhammad, ahli zake na Maswahabah wake wote.*

**MAELEZO**

Maneno haya ambayo ameyataja mwandishi kuhusu Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni maneno mazito. Ni maneno ambayo yanapaswa kuandikwa kwa maji ya dhahabu. Inampasa kila muumini ayaamini, ayatendee kazi na ayafuate. Haya ndio maneno ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Qur-aan Tukufu na Sunnah Twaharifu imefahamisha hayo. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni wenye kusifika na kheri zote.

**Pamoja na misingi hii wanaamrisha mema... -** Wanaamrisha mema na kukataza maovu kwa mujibu wa Shari´ah. Wamefungamana na Shari´ah. Amesema (Jalla wa ´Alaa):

وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ

**"Na Waumini wanaume na Waumini wanawake ni marafiki walinzi wao kwa wao, wanaamrisha mema na wanakataza maovu." (09:71)**

**Wanaonelea kufanya Hajj... -** Wanaonelea kusimamisha swalah pamoja na Ijumaa kwa Jamaa´ah, kupigana Jihaad pamoja na viongozi, ni mamoja wawe wema au waovu. Hili ni kutokana na hekima inayopatikana katika kufanya hivi. Mzigo wa madhambi yake yako juu yake. Wanaswali pamoja naye Ijumaa na swalah za Jamaa´ah na kupigana Jihaad pamoja naye hata kama atakuwa ni mwenye kufanya baadhi ya maasi. Hivi ndivyo hali ilivyokuwa wakati wa Banuu Umayyah, Abul-´Abbaas na wengineo.

Wanaamrisha kuwatendea wema wazazi wawili, kuunga kizazi, kufanya ujirani mwema, walingania katika kuwa na tabia njema, kufanya matendo mazuri, wanahimiza kumuunga yule uliyemkata, umsamehe yule aliyekudhulumu na

ummpe aliyekunyima. Wanaamini yale aliyosema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Mfano wa waumini, katika kupendana kwao, na kuhurumiana kwao na kuhisiana kwao, ni kama mfano wa mwili mmoja. Wakati kiungo cha mwili kinapatwa na maumivu, mwili mzima unapatwa na homa."

Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Muumini kwa muumini mwenzake ni kama jengo; upande mmoja unaupa nguvu upande mwingine."

"Muumini mwenye imani kamilifu ni yule mwenye tabia nzuri zaidi."

Yote haya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni wenye kuyaamini. Katika yote wanayoyasema na kuyafanya ni wenye kufungamana na Qur-aan na Sunnah. Wao hawana malengo mengine. Bali maneno yao na matendo yao ni wenye kufungamana na Qur-aan na Sunnah. Kwa ajili hii ndio maana wakaitwa "Ahl-us-Sunnah", "Ahl-ul-Jamaa´ah na "Ahl-ul-Kitaab was-Sunnah". Si kwa jengine bali ni kwa sababu wamekusanyika, kufungamana na kushirikiana katika hayo. Wao ndio Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah na Ahl-ul-Kitaab was-Sunnah. Hivi ndivyo walivyobainisha wanachuoni.

***Na miongoni mwao kuna wakweli, mashahidi... -*** Katika wao kuna maimamu wa uongofu na elimu. Hawa ni wale waliosimama bara bara katika dini na wakajifungamanisha na Shari´ah. Wote hao wanaingia katika Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.

**Miongoni mwao kuna ´Abdaal... -** Katika wao kuna ´Abdaal. Hawa ni wale wenye kubadilishana baadhi kwa wengine. ´Abdaal ni wanachuoni ambao hawa wanawarithi wengine. Kwa maana ya kwamba anapokufa mwanachuoni huyu anakuja baada yake mwengine mpaka kifike Qiyaamah. Hii ndio hali ya Ummah huu. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Na hakitoacha kikundi katika Ummah wangu kuwa ni chenye kunusuriwa juu ya haki. Hatowadhuru wale wenye kwenda kinyume nao na kuwapinga mpaka itapofika Qiyaamah."

Katika kipindi hicho waumini wanaume na wanawake wote watakuwa wameshafariki. Kutakuwa hakukubaki isipokuwa viumbe waovu tu ndio wataosimamiwa na Qiyaamah.

Tunamuomba Allaah atujaalie sisi na nyinyi kuwa katika wao, atukinge sisi na nyinyi kutokana na shari ya nafsi zetu na uovu wa matendo yetu na ainusuru dini Yake na alinyanyue Neno Lake.

Hakuna nguvu za kufanya utiifu na kuacha maasi isipokuwa kwa msaada wa Allaah. Swalah na salaam zimwendee mja na Mtume Wake na Mtume wetu Muhammad, familia yake na Maswahabah zake.